

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Nane – Tarehe 10 Februari, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa Mwaka 2009/2010 [The Annual Report and Audited Accounts on the Activities of the Open University of Tanzania for the Financial Year 2009/2010].

MASWALI NA MAJIBU

Na. 105

Upungufu wa Maji Katika Mji wa Pangani

MHE. SALEHE A. PAMBA aliuliza:-

Mji wa Pangani ni Mji unaokuwa kwa kasi kutokana na ongezeko la watu na shughuli za kiuchumi. ongezeko hilo husababisha maji yanayosambazwa na Mamlaka ya Maji Pangani kutosheleza mahitaji ya wakazi wa Mji huo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ujazo wa maji katika Mji huo ili kukudhi mahitaji hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri MKuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salehe Ahmed Pamba, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma ya maji katika Mji wa Pangani na Vijiji vinavyoizunguka Mji huu vya Boza, Mwenbeni, Madanga, Jaira na Kimang'a hutolewa na kusimamiwa na mamlaka ya maji safi mjini. Idadi ya wakazi wanaohudumiwa na mamlaka ya maji ni 16,320 na mahitaji yao ya maji yanakadiriwa kuwa mita za ujazo 2250 kwa siku (2250m³/d) na uwezo wa mamlaka kusambaza maji kwa sasa ni mita za ujazo 1,184 kwa siku ambazo ni sawa na asilimia 52 ya mahitaji ya maji.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza adha ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Pangani, mwaka 2010/2011 Mji wa Pangani ulitumia shilingi milioni 40.0 kutoka Mamlaka ya Maji ya Mji wa Pangani kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya usambazaji maji na ununuzi wa mashine ya kusukuma maji. Idadi ya watu walionufaika na huduma hiyo wanakadiriwa kufikia 3,212. Aidha, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani kupitia Wizara ya Maji iliidhinishwa shilingi milioni 747.5 kwa ajili ya

kuboresha miundombinu ya maji katika Mji wa Pangani kwa kurudishia mabomba mapya, kuchimba visima viatatu(3) na kufunga pampu mpya za maji ikiwa ni mpango wa muda mfupi wa kutatua tatizo la maji katika Mji wa Pangani.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu wa kuondokana na tatizo la maji katika Mji wa Pangani ni kutumia maji ya mto Pangani. Halmashauri ya Wilaya imewasilisha katika Wizara ya Maji mpango wa kutumia maji ya mto Pangani ambao unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 10.6 baada ya kufanyika usanifu kupitia *Arab Consulting Engineers*. Ni matarajio kuwa mpango huu utapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la maji katika Mji wa Pangani kutokana na chanzo hiki kuwa cha uhakika zaidi.

MHE. SALEHE A. PAMBA:Mheshimiwa Spika, ahante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu hayaonyeshi hali halisi kabisa ya tatizo la maji pale Pangani. Majibu haya ni *stereotype*. Ni majibu tu ambayo yanajibiwa jibiwa tu na wataalam. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa utaratibu wa kuweka Mji wa Pangani katika *cluster* chini ya Mamlaka ya Maji ya Tanga madhumini yake ni kuwapa uwezo wa kifedha na kiutaalamu Mamlaka ya Maji ili iweze kukuwa na kwa kuwa Mamlaka ya Maji ya Mji wa Tanga haijaisaidia kabisa Mamlaka ya Maji ya Mji wa Pangani.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutoa agizo kwamba Mamlaka ya Maji ya Mji wa Tanga iende Pangani ikaangalie matatizo yote ya maji yaliyoko Pangani na kuona jinsi ya kuwasaidia na kuwaondolea kero wananchi wa Pangani?

(b) Kwa kuwa hali halisi ya maji sasa hivi ni upatikanaji wa maji ni kwa asilimia 20 tu na hii inatokana na ubovu wa mitambo hasa *pump* na kwa kuwa Mamlaka ya Maji ya Pangani ni masikini haina uwezo wa kununua pampu na tunahitaji pampu yenye thamani ya milioni 20 ili kurudisha angalau asilimia 20 ya maji kwa ajili ya watu wa Pangani. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akaisaidia Mamlaka ya Maji ya Pangani shilingi milioni 20 ili tuweze kupata *pump* na kuwapatia wananchi maji ya asilimia 65 ambayo walikuwa wanapata zamani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, kama ifuatavyo:-

Hii anayosema *stereotype* ningemsomea majibu ambayo yaliletwa hapahapa ambayoningemsomea ungezimia hapo kwenye kiti, hapo ulipo. Haya ni kwamba nimeshayakarabati sana hapa ninapokupa hii. Nikufahamishe tu kwamba 52% ndiyo inayopatikana pale Pangani. Ninasema jambo hili nina fahamu, mimi kwani nilikwenda pale, ni *dry area* kweli. Wana matatizo ya maji pale nafahamu, najua kabisa mimi siwezi kumkanushia Mheshimiwa Mbunge, lakini ningemsomea majibu ya awali ambayo nilikuwa nayo hapa, angeshangaa.

Niseme tu kwamba ni kweli kama anavyosema pana tatizo la maji pale Pangani, Mji ule ni Mji mzuri, unakuwa wa kitalii ambao ukisaidiwa pale *investment* yake pale utakuwa umeisaidia. Amesema tuzungumze na *cluster* ya Tanga na ni kweli kabisa kwamba hawa wana *fall under* Tanga, tutazungumza nao kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge, tutazungumza nao ili tuone jinsi wanaweza wakausaidia huu Mji na kama nilivyoeleza hapa chanzo cha uhakika kabisa pale Pangani ni chanzo kile kinachotokana na Mto Pangani. Sasa nimesema hapa bilioni 10.6. ukimwuliza hela anazopelekewa pale anapelekewa shilingi milioni 720 ndizo anazopelekewa pale, unazipata wapi?

Nikijibu hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu ataniuliza hivi; nimekusikia unamwambia Mheshimiwa Pamba pale kwamba utapeleka maji pale bilioni 10 unazipata wapi? Ndiyo tukaeleza haya tunayozungumza hapa. (Makofi)

Nataka nikuhakikishie hili jambo tunalichukua seriously na hata hizi milioni 20 ambazo anasema kwamba zikipatikana zitaisaidia katika mpango huu, tutazungumza na wezetu hapa, hela walizopangiwa wao ni shilingi milioni 720, tutaona jinsi ya kuwasaidia ili iwezekane ipatikane hiyo *pump* anayosema tuweze kuwasaidia.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kasi ya Mji wa Pangani inafanana sana na kasi ya ukuaji wa Mji wa Bahi, ambayo hivi karibuni miaka mitatu iliyopita ulitangazwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Bahi na tatizo kubwa la Mji wa Bahi ni maji ambayo yale yaliopo madogo ni ya chumvi hata yanaharibu maji yanayopita katika nyumba zinazoyatumia.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo sugu la upatikanaji wa maji katika Mji wa Bahi?

SPIKA: Sasa mnaona swali kama hili, Waziri alikuwa amejitanda Pangani sasa ukiwa na Bahi hivi hivi bila kutafuta pale, ukipata majibu robo ujue ndiyo hivyo hivyo, haya Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Badwel, Mbunge wa Bahi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama unavyosema ningekuwa nimejua mapema ningekuwa na zile takwimu hapa. Ninachojua kimoja tu generally na Mheshimiwa Lwenge angekuwepo hapa angetusaidia sana ni kwamba kila Wilaya imetakiwa i-identify Vijiji 10 sasa hii anayozungumzia ni Makao Makuu ya Wilaya mpya ambayo Makao Makuu nimekwenda pale ni kweli wana tatizo kubwa la maji.

Tutakwenda kuangalia katika orodha ile kujua kwamba ni kiasi gani ambacho kimepangwa pale lakini najua bado kwa vile anazungumzia Makao Makuu ya Wilaya unaweza ukahitaji namna maalum ya kuwasaidia pale ukiacha ile ambayo tunayoizungumza ambayo inasaidiwa na *World Bank*. (Makofi)

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Jiji la Mwanza ni moja ya Majiji yanayokuwa kwa kasi sana barani Afrika na inakuwa kwa asilimi 11.4 kwa mwaka, sasa maeneo mengi ya Jiji la Mwanza Vijiji kama Fumagira, Esebanda, Kalindo yalikuwa yamewekwa chini ya Halmashauri ya Jiji ku-supply maji sio chini ya MWAUWASA lakini capacity ya Halmashauri ya Jiji kupeleka maji huko Halmashauri ya Jiji haina uwezo wa kutosha kupeleka maji.

Je, kwa nini Serikali isione kwamba muda muafaka umefika yale maeneo yamekuwa sehemu ya mitaa ya Jiji la Mwanza sasa iingie kwenye system ya Jiji. Sasa kwa nini Serikali isichukue huo mzigo kutoka kwenye Halmashauri kupeleka maji salama kufika kwenye hivyo Vijiji?

SPIKA: Sawa sawa kama swali hili, hili ni swali jipya kabisa, mkipata nusu majibu mkubali tu, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Wenje, kama ifuatavyo:-

Mwanza nayo ina sensitivity yake kama anavyosema na anachosema ni kwamba lile Jiji kama Jiji lenyewe pale limeshaelemewa kwa maana ya kwamba majukumu yake yanaongeka kwa sababu sasa tumeshaonyesha kwamba ni Mwanza ni Jiji. Tunakwenda hivyo tunavyokwenda, niseme tu kwamba Mheshimiwa Wenje itakuwa ni vizuri zaidi tukakaa tukaliangalia, tukawa na takwimu tukalionona wote kwa pamoja kwamba tatizo liko wapi anachotaka kusema ni nini waondoe katika ule utaratibu. Sasa sisi Halmashauri tunazungumza na kuzingatia *D by D Decentralization by Devolution*.

Tunachofanya ni ku-devolve mambo yote kuyapeleka kule katika Halmashauri, Halmashauri zifanye. Kwa hiyo, ukirudi tena huku juu ni kama vile unaondoka tena katika jambo lile. Lakini kwa sababu ya uzito wa Mwanza anayoizungumza hapa tutaliangalia kwa pamoja tuone tunafanya nini. (Makofi)

Asilimia 20 ya Kodi Zilizofutwa Kwa Vijiji

MHE. ROSE K. SUKUM aliuliza:-

Mwaka 2002 Serikali ilifuta kodi zote za manyanyaso ambazo zilikuwa chanzo cha mapato kwa Halmashauri na badala yake iliamua kutowa fidia kwa kutoa asilimia 20 ya vyanzo vya kodi zilizofutwa ili zipelekwe kwenye ngazi ya Vijiji lakini tangu mwaka 2005/2006 hadi 2010/2011 Vijiji vya Wilaya ya Hanang havijapelekewa fidia hiyo:-

(a) Je, Halmashauri ya Hanang ilipokea kiasi gani cha fidia ya vyanzo vya kodi hizo kwa miaka yote iliyotajwa kwenye swali hili; na je kurudisha fedha hizo Vijijini ni hisani au ni agizo la Sheria?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha hakikupelekwa Vijijini ikiwa ni sehemu ya vyanzo vya mapato ya Halmashauri yatokanayo na vyanzo vya ndani?

(c) Je ni hatua gani za Kisheria zinachukuliwa dhidi ya wale walioshindwa kutekeleza matakwa ya Sheria husika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, agizo la Serikali kwa Halmashauri la kutenga 20% kwenye ngazi za msingi za mamlaka ya Serikali za Mitaa lipo kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 kwa kufuta vyanzo vya kodi zilizoonekana kwamba ni kero kwa wananchi.

Agizo hilo linazitaka Halmashauri kutenga 20% ya mapato yake na kupeleka katika ngazi za msingi za mamlaka za Serikali za Mitaa kama fidia ya vyanzo vya kodi zilizofutwa. Kwa kuzingatia hilo, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang katika kipindi cha 2005/2006 hadi 2010/2011 ilipokea fidia kiasi cha shilingi bilioni 1.4 na kupeleka shilingi milioni 33.4 katika ngazi za msingi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka ya 2005/2006 hadi 2010/2011 Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Hanang kwa vyanzo vya ndani ilikuwa shilingi 1,967,886,220/= na mapato halisi yalikuwa ni kiasi ya shilingi 1,761,938,299/=, asilimia 20 ya mapato halisi ni shilingi 352, 387,659/=. Fedha zilizopelekwa kwenye ngazi za msingi kwa kipindi hicho ni shilingi 40,511,412/=. Hivyo fedha ambazo hazikupelekwa katika ngazi za msingi za mamlaka ya Serikali za Mitaa ni shilingi 311,876,247/=.

(c) Mheshimiwa Spika, kutotekelza maagizo ya Serikali, Sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kwenda kinyume na Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 na Kanuni zake za mwaka 2003. Hatua stahiki za kinidhamu hazina budi kuchukuliwa kwa mtumishi yeyote atakayebainika kuwa na makosa ya aina hiyo. Utaratibu wa kuchukua hatua za kinidhamu imeainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 kwa kupata ushahidi unatokana na kuvunjwa au kukiukwa kwa maagizo yaliyomo katika Kanuni za usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LAFM 2009)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwasihia Waheshimiwa Wabunge ambao pia ni Wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani kwenye Halmashauri zao kusimamia kwa karibu utendaji wa Halmashauri katika kutekeleza maagizo ya Serikali ya kupeleka fedha kwenye ngazi za msingi za Serikali za Mitaa.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba wamekiuka Wilaya ya Hanang kutokupeleka hizo asilimi 20 kwenye Vijiji husika na utaratibu wa kuchukuliwa hatua za kinidhamu imeainishwa iko kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma 2002.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri haoni ni wakati muafaka sasa kuwachukulia hatua Wakurugenzi waliokiuka taratibu hizo?

(b) Je, haoni sasa kwamba shughuli za miradi za wananchi Vijijini zimekwama kutokana na matumzi mabaya ya Wakurugenzi katika Hamashauri ambazo zimekiuka taratibu hizo. Je, ukaguzi maalum unawezekana kufanyika katika Wilaya ya Hanang ili kubaini hayo matumizi mabaya, hasa kwenye miradi ya maendeleo na matumizi mengine ya fedha za Umma kuzihamishia kwenye miradi mingine?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niweke records vizuri hapa ili tuweze kuelewana kwamba tunachozungumza hapa ni nini. Ile tofauti ambayo nimeizungumzia hapa, tumeitafuta kwa sababu tulijua kwamba swali hili linaloulizwa hapa litaulizwa, tukasema hela hizi zimekwenda wapi? Anachosema 20% iliyokwenda pale je kiasi hicho kilikwenda kule, tukakuta kwamba Halmashauri katika kikao chao na nimeitisha muhtasari, muhtasari ninao ambao walikaa Baraza la Madiwani na wakaipitisha kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara zinaonyesha kwamba LAPF walipeleka shilingi milioni 108, Pili wakatamia shilingi milioni 239 kwa ajili ya tatizo la mgogoro wa ardhi uliokuwepo katika Vijiji vile vya Gawal na Waren na hii nayo nimecheki nayo nikakuta kwamba iko kule na kinachozungumzwa hapa ni kwamba u-trickle down ile 20% uipeleke kule Vijijini ndicho kinachozungumzwa hapa.

Sasa ni kweli nimetafuta, je hela hizi zilikuwa katika Bajeti na zilipangwa kwa ajili ya jambo hilo? Tukakuta kwamba hili halikuwepo lakini vikao vile vilihalalisha hivi ambavyo walikaa na nimecheki wakati huo katika majina nimekuta alikuwa ni Diwani wakati huo, alikuwa si Mbunge kama ilivyo hapa. Wote Mheshimiwa Mary Nagu, wamepitisha. Pia nikataka nijidhihirishe ni nini ambacho kinaonekana kwamba kimekiukwa hapa *and therefore nim-take to task* Mkurugenzi nikakuta kwamba huyu amefanya kazi zote na ile mihititari yote imefanyika hapa. Sasa labda kwa ajili ya faida ya Bunge lako pamoja na maelezo yote tuliopewa hapa, nimemwagiza sasa Katibu Tawala achukue hii *information* yote inayozungumzwa hapa, tulisema hatutarudia, hatutampuuza Mbunge yeyote hapa atakwenda na hii taarifa yote iliyoko hapa. Baada ya haya yote niliyosema hapa aende tu anithibitishie kwamba ilikuwa ni hivyo na baada ya hapo nitakuarifu kwamba hakukuwa na tatizo lolote au kulikuwa na tatizo lolote. Kwa wale ambao wanafanya hivyo, ambao hawakufuata hizo taratibu nilizozieleza kwanza na Mheshimiwa Augustine Mrema anafahamu, Mwenyekiti wa LAAC, mara ya kwanza kama ukimkuta mtu amekiuka, amepeleka hela mahali ambapo hazikupangwa kwenye Bajeti ambayo inapitishwa na Bunge hili, unamkata 20% na unamwambia Waziri mwenye dhamana kwamba akate na anapelekewa barua ya onyo. Mara ya pili unamkata 30% na unampeleka barua ya onyo.

Mara ya tatu unamkata *thirty percent* ya mshahara wake na unamwambia Katibu Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwamba huyu mtu tunamsimamisha kazi na madaraka yake anaondolewa pale. Huo ndiyo utaratibu tunaoutumia hapa. Hakuna mtu anaruhusiwa kubadilisha hela ambazo zimepitishwa na Wabunge hapa akapeleka kwenye sehemu nyingine bila kufuata utaratibu huu. Ataanzia kwenye Baraza la Madiwani, atakwenda *Regional Consultative Committee* pale watapitisha kwa maana ya Sekretarieti, watapeleka kwa Katibu Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa *in conjunction* na Hazina, Katibu Mkuu ndiyo walete sasa waseme kibali kimetolewa pale. Hela za zahanati hii ni za zahanati. Za barabara ni za barabara. Lakini hao ninaowazungumza hapa walifuata taratibu hizo ninazosisema na mihtasari iko tunayo Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Ahsante kwa semina. Semina inatosha, muda umetumia ni dakika 10. Sasa naenda Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, atauliza swali linalofuata.

Kupandishwa Viwango Vya Mishahara ya Walimu

MHE. SELEMANI S. JAFO aliuliza:-

Walimu kwa kipindi kirefu sasa hawajapandishwa viwango vya mishahara yao. Je, Serikali ina mpango gani wa kushughulikiwa tatizo hilo sasa kwa walimu wa Kisarawe?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleimani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mishahara ya watumishi wa Serikali wakiwemo walimu, imekuwa ikipandishwa kila mwaka kwa kuzingatia hali ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa wakati mwaka 2005, mwalimu wa daraja la IIIA alianza na mishahara kwa shilingi 74,570/= kwa sasa mwalimu wa Daraja hilo anaanza na mishahara wa Sh. 244,400/= kwa mwezi, ambalo ni ongezeko la asilimia 227.8 mwalimu mwenye stahhada (Diploma) alikuwa akianza na mishahara wa shilingi 108,800/= ambapo sasa anaanza na shilingi 325,700/= kwa mwezi, ambalo ni ongezeko la asilimia 199.4. Aidha takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2005 mwalimu mwenye shahada (Digriri) alianza kazi na mishahara wa shilingi 140,000/= na sasa mishahara wake ni shilingi 449,200 kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimi 235.14.

Mheshimiwa Spika, ikilinganishwa na nyongeza ya mishahara kwa watumishi wote wa Umma, takwimu zinaonyesha kuwa mishahara ya walimu imekuwa ikiongezwa kwa kiasi kikubwa zaidi kuliko watumishi wengine, wakati mishahara ya watumishi wengine iliongezwa kwa kati ya asilimia 5 na 12.6 kwa mwaka mishahara ya walimu iliongezwa kwa kati ya asilimia 12 na 12.4 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya si kweli kwamba walimu hawajapandishwa mishahara yao kwa kipindi kirefu.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri yaliyojaa takwimu na hekima lakini nilipenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kuna tatizo kubwa sana kwa watumishi wetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanapobadilishiwa mishahara lakini ile nyongeza ya mishahara nyingi sana huwa haiwi *reflected* kwa haraka na hili ni usumbufu mkubwa wafanya kazi hao kuwa wanawajibika kujaza fomu mbalimbali mradi mishahara yao stahili iweze kuwekwa. Je, Serikali imejipanga vipi kutatua hili kwa watumishi wetu? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa tumekuwa na wafanyakazi wengi sana wanafanya kazi katika mazingira magumu hasa kule kwangu Kisarawe kuna watu wanafanya kazi kule Kimaramisale, Dololo, Kihale ambao kazi zao wanafanya kazi katika mazingira magumu kweli kweli. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wafanya kazi hawa wanapata posho maalum ya mazingira magumu na ikiwezekana kupata vipando vya kuwawezesha kufika katika maeneo mbalimbali hasa wanapokwenda kufuatilia mishahara yao? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Kuhusu suala la watumishi kupandishwa cheo na kuchelewa kubadilishiwa mishahara kwa sasa hivi Ofisi yangu imeboresha mfumo wa mishahara na sasa hivi tumepeleka mfumo huo kwa Waajiri wote ikiwemo Halmashauri, Wizara na maeneo mbalimbali. Sasa jukumu la kuingizwa kwenye *pay role* au kuingizwa kwenye kompyuta kila Halmashauri itakuwa inafanya wenyewe. Kwa hiyo tunachofanya sisi sasa hivi ni kumaliza viporo vile ambavyo vilibaki. Lakini kwa watumishi ambao watakuwa wanapandishwa vyeo kwa sasa hivi Halmashauri zenyewe, Wizara zenyewe na Taasisi mbalimbali za Serikali watakuwa wanaingiza wenyewe, wanafanya mabadiliko kwenye kompyuta na kazi ya Ofisi yangu ni kuidhinisha tu yale marekebisho kwamba ni sahihi na kazi hiyo kama wataifanya kwa usahihi anaweza akaingiza na kufika katika Ofisi yetu kwa muda usiozidi dakika kumi.

Kuhusu suala la watumishi wanaoishi katika mazingira magumu. Ofisi yangu imepitisha sera ya motisha na maslahi katika Utumishi wa Umma na sasa hivi tunaandaa Bodi ambayo itashughulikia masuala hayo. Ni suala sasa la kila mwajiri kuangalia katika mazingira yake ni motisha zipi atoe kwa watumishi wake. Suala la vipando kwa watumishi sasa hivi Ofisi ya Rais na Serikali tumeanzisha kutoa mikopo kwa watumishi ambao yeye mwenyewe ataangalia kama ni kwa ajili ya kipando au ni kwa ajili ya masuala mengine kama ni nyumba au kama nini kulingana na mshahara wake na mikopo hiyo tumeshaanza kutoa kwa awamu ya kwanza.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa walimu wamekuwa wakidai stahili zao Serikalini, *almost* bilioni 50 zimekuwa zikidaiwa na walimu na kwa kuwa mwezi Desemba na mwezi Januari Serikali iliahidi kwamba ingemaliza hayo madai ya walimu. Je, Serikali sasa ituambie imefikia hatua gani kulipa hayo madai ya Walimu ili kuepusha taifa na migogoro isiyo ya lazima?

SPIKA: Nilikosea jina lako ni Pauline Gekul.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya walimu yale yasiyokuwa ya mishahara karibu yote sasa maeneo mengi tulishapeleka hizo pesa na zimelipwa. Yale ambayo ni madai ya mishahara na yenyewe yameanza kulipwa na ni imani yetu kwamba muda si mrefu tutakuwa tumeyakamilisha.

Na. 108

**Watumishi wa Serikali Wanaoishi Mahotelini
kwa Kukosa Nyumba za Serikali**

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI aliuliza:-

Hivi sasa Sera miradi mbalimbali ya kujenga nyumba mpya kwa ajili ya watumishi wa Serikali ikiwa ni pamoja na Mawaziri ingawa iliuzwa kwa bei nafuu nyumba walizokuwa wanakaa watumishi wake kwa madai kuwa zilikuwa chakavu hivyo ilikuwa gharama kubwa kuziendesha.

- (a) Je, ni watumishi wangapi wanaoishi hotelini na familia zao kwa kukosa nyumba za kuishi?
- (b) Je, Serikali inalipa shilingi ngapi kwa mwezi katika hoteli waliopanga watumishi hao na familia zao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, siyo utaratibu kwa watumishi wa Serikali kukaa hotelini, isipokuwa katika mazingira maalum kama vile uteuzi wa kwanza au uhamisho.

Mheshimiwa Spika, yanapotokea mazingira haya, mtumishi ana hiari kukaa hotelini kwa muda wa siku 14 ambapo Serikali humlipia gharama za malazi na chakula (*Full Board*) au malazi na kifungua kinywa (*Bed and Break Fast*) na kulipwa nusu ya posho ya kujikimu kwa muda wa siku 14 kwa mujibu wa Kanuni L.5 (2) na L.6 ya Kanuni za Kudumu (*Standing Orders*) 2009 na baada ya muda huo, anapaswa kuwa amepata nyumba ya kupanga endapo hatapatiwa nyumba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi Namba 3 wa mwaka 2010, kiongozi au mtumishi mwenye stahili ya kupatiwa nyumba na Serikali anapokosa nyumba ya Serikali, analipwa na mwajiri wake posho maalum ili aweze kulipia pango, na siyo kukaa hotelini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi sasa hakuna kiongozi wa Serikali anayeishi hotelini kwa kuwa wanahudumiwa kwa mujibu wa taratibu nilizozieleza hapo awali.

(b) Kwa kuwa viongozi wanahudumiwa na Maafisa Masuuli wanaohusika, fedha zinalipwa pale, wanapochagua kukaa hotelini kwa utaratibu nilioeleza, zinakuwa zinatoka sehemu ya matumizi ya Fungu (Vote) husika.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya watumishi wa Serikali waliouziwa nyumba walikuwa wamekaribia kustaafu na wengine walifariki dunia hata kabla hawajamaliza kulipia nyumba hizo.

Je, Serikali inaweza kutueleza ni hasara kiasi gani imepatikana kwa nyumba hizo kwa baadhi ya nyumba kushindwa kulipiwa? (Makofi)

Swali la pili, kwa kuwa uamuzi wa kuuza nyumba za Serikali kwa bei nafuu ulilalamikiwa sana na wananchi kwamba ulikuwa na dhamira ya kuwanufaisha wakubwa waliokuwa wakiishi katika nyumba hizo.

Je, ni kweli gharama ya kutunza ama kuendesha nyumba hizo zilikuwa kubwa kuliko kujenga nyumba mpya kama ambavyo Serikali inafanya hivi sasa? (Makofi)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu suala la zile nyumba kuuziwa wastaafu na watumishi wengine kufariki. Je, Serikali imepata hasara kiasi gani?

Napenda nimhakikishie kwamba hakuna hasara ambayo Serikali imeingia kwa sababu kama mtumishi amestaafu baadhi yao walilipa kutokana na mafao yao waliyoyapata kipindi kile walipostaafu. Wale ambao walifariki na zile nyumba zikashindwa kulipiwa Serikali ilizirejesha zote na hata wale ambao hawajastaafu na ambao hawajafariki kwa maeneo ambayo wameshindwa kuzilipia Serikali imezichukua, kwa hiyo Serikali haikupata hasara.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba gharama ya kuzitumza hizi nyumba ilikuwa ni kubwa na wala haikuwa hila kuwapa viongozi wakubwa nyumba zile na si kweli kwamba waliopata nyumba zile za Serikali wengi walikuwa wakubwa. Wapo baadhi yao ambao ni watumishi wa kawaida kwa sababu nyumba ziko katika madaraja mbalimbali, ambao walikuwa wanazikalia nyumba zile pia wenyewe walipata fursa hiyo ya kuweza kuuziwa nyumba. (Makofi)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali iliahidi kupitia zile nyumba walizouziwa wafanyakazi ili kuangalia zile ambazo ziko katika maeneo ya kazi ziweze kurudishwa. Na kwa kuwa hatujaona matokeo ya zoezi hilo zikiwemo nyumba za ma-OCD ambazo ziko kwenye maeneo ya kazi na nyumba za madaktari mfano madaktari wa Mkoa wa Singida ziko kwenye maeneo ya kazi kabisa ziliuzwa.

Je, Serikali inasema nini kwa kauli yake ambayo iliahidi hapa hapa ndani ya Bunge? (Makofi)

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Utumishi kwa majibu mazuri. Taarifa ya suala alilouliza Mheshimiwa Chilolo inaendana na hoja iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa aliyekuwa Mbunge Mheshimiwa Aloyce Kimaro na taarifa hiyo ilikwishatolewa kwenye Bunge hili na Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Kawambwa.

Lakini ninachotaka kumthibitishia Mheshimiwa Chilolo ni kwamba zile nyumba zote ambazo zilikuwa zimepewa kwa makosa kwa maeneo ambayo hayakustahili zimesharudishwa Serikalini na hatua ambazo zingine zinachukuliwa na Agency kupitia Sheria namba 30 ya mwaka 1997 ni pamoja na kuendelea kujenga nyumba zingine kwa ajili ya watumishi hadi sasa hivi zaidi ya nyumba 1,025 zimeshajengwa na kwa sasa hivi pia kuna plot nyingine ambapo kuna mpango wa kujenga nyumba karibu 10,000 katika nchi hii baada ya kupitishwa Sheria ya PPP.

Maeneo mbalimbali ambayo yamejengwa nyumba ni pamoja na Dodoma katika Wilaya mbalimbali kama Siha, Namtumbo na maeneo mengine mengi, Mvomero, Bahi na maeneo mengine katika nchi nzima ambapo nyumba zinaendelea kujengwa.

Nataka kuthibitisha pia kwamba suala la uuzaji wa nyumba limetokana na Tume iliyoundwa mwaka 63 iliyokuwa inaitwa Tume ya ADU na mwaka 75 iliyokuwa Tume ya Nsekela na suala la uuzaji wa nyumba limeanza tu baada ya kupata uhuru na ndiyo maana ukienda sasa hivi Magomeni utakuta palikuwa na nyumba ambazo waliuziwa wafanyakazi na watumishi.

Ukienda Moshi utakuta, ukienda Mwanza sehemu za Ghana utakuta nyumba zilizouzwa kwa wananchi. Ukienda hata Sengerema kwenye barabara ya kwenda Sengerema Sekondari kuna nyumba zilizouzwa kwa wananchi. Hili ni jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa *empowered* kwa kuwa na nyumba zao na hii ni sera halisi ya kuwa-*empower* wananchi. (Makofi)

Na. 109

Wamiliki wa Mgodini wa North Mara Kutoa Huduma za Kijamii kwa Maeneo Jirani

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE aliuliza:-

Mgodini wa dhahabu wa *North Mara* upo Wilaya ni Tarime:-

- (a) Je, mgodini huo umewanufaishaje wananchi wa eneo hilo katika kutekeleza ahadi ya kutoa huduma za afya, barabara, maji, elimu na umeme kama zilivyoonyeshwa katika mkataba?
- (b) Je, ni lini mgodini utanza ujenzi wa barabara ya kutoka mto Mara-Nyamongo-Nyamwaga hadi Tarime na kutenga eneo la kuendeleza wachimbaji wadogo wadogo?
- (c) Je, kwa nini mgodini umesitisha kulipia ada wanafunzi wa vijiji vilivyozunguka mgodini na wakati huo huo ukilipa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime USD 200,000 ni lini sasa utaongeza kiwango hicho kufikia USD 2,000,000?

SPIKA: Hiyo iko nje ya Kanuni kabisa. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mgodini wa dhahabu wa *North Mara* umechangia na kuboresha huduma za kijamii kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba iliyowekwa kati yake na vijiji vinavyozunguka mgodini huo. Mgodini ulichangia ukarabati na upanuzi wa kituo cha Afya cha Sungusungu kilichoko Nyamongo na umeendelea kuboresha kituo hicho kwa kufunga tenki za maji, kusafisha maeneo ya hospitali na kufanya matengenezo madogo madogo.

Aidha, mwaka jana, mgodini ulitoa mashine ya *Anaesthesia* (mashine ya usingizi) katika jitihada za kuboresha huduma za upasuaji katika hospitali ya Mkoa wa Mara, mwaka jana mgodini wa *North Mara* ulitoa mchango wa shilingi milioni mia sita kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ukarabati barabara ya Ochuna-Nyamongo (*Old German Road*).

Mgodini unatoa udhamini wa masomo ya wanafunzi kutoka vijiji vinavyozunguka mgodini huo katika vyuo vya juu mbalimbali. Ili kuondoa migogoro, udhamini huu unahakikiwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Tarime. Mgodini umelipia gharama za kuwanoa walimu wa sayansi, hesabati na kiingereza katika chuo cha walimu Tarime. Chuo cha Walimu Tarime pia kimefaidika kwa kujengewa nyumba za walimu.

Aidha, kwa kushirikiana na VETA kampuni ya *African Barrick Gold* huwachukua vijana kutoka vijiji vinavyozunguka migodi yake na kuwapa mafunzo ya ufundi huko Moshi na baadaye kuwapa ajira. Mgodi unatekeleza mradi wa maji kwa awamu tatu ya usambazaji wa maji katika vijiji hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Mto Mara-Nyamongo-Nyamwaga hadi Tarime ni ya TANROADS hivyo utengenezaji wake unafanywa na taasisi hiyo. Aidha, utengaji wa maeneo ya uchimbaji kwa wachimbaji wadogo ni jukumu la Wizara yangu na kazi hiyo imefanyika na itaendelea kufanyika katika Wilaya ya Tarime na Tanzania nzima kwa ujumla.

(c) Mheshimiwa Spika, yalikuwepo maridhiano kati ya vijiji vitano vyenye mikataba na mgodi kuwa, mgodi utumie fedha za vijiji zilizotegemewa kutokana na asilimia moja ya mrabaha ili kulipia karo za shule. Karo hizi zililipwa tangu mwaka 2004, wakati uchimbaji wa Nyabigena (Shimo lenye mrabaha) ulikuja kuanza 2007 na kusimama 2009. Mgodi unasema fedha zote za mrabaha zimetumika hivyo kusitisha mpango huo.

Hivi sasa jitihada zinafanywa ili kuhakiki kilichopatikana na jinsi kilivyotumika. Kuhusu ushuru unaolipwa na mgodi kwenye Halmashauri za Wilaya unaratibiwa na Sheria na Kanuni za mikataba na kiasi cha juu kwa sasa ni USD 200,000 kwa mwaka. Serikali itakaa na wadau ili kuangalia uwezekano wa kupandisha kiwango hiki.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo yametolewa ambayo mimi siridhiki nayo ambapo kiasi kikubwa ni ya uongo. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

SPIKA: Tunasema siyo ya sahihi, siyo sahihi. Naomba ubadilishe hilo neno.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, majibu siyo sahihi. Pamoja na hayo basi naomba niulize maswali ya nyongeza. Utakumbuka kabisa kwamba kupitia Bunge lako Tukufu, umetuma Kamati mbili, Kamati ya Mheshimiwa James Daudi Lembeli na Kamati ya Mheshimiwa Makamba kuangalia matatizo yaliyopo katika mgodi wa Nyangoo.

Mheshimiwa Spika, utaangalia kabisa kwamba, kuna ahadi nyingi ambazo zimetolewa; hata Waziri wa Mambo ya Ndani alienda akaahidiwa kabisa kwamba, huu Mgodi uliahidi kwamba, utajenga barabara ya lami kutoka Mto Mara, Nyamongo, Nyamwaga mpaka Tarime Mjini kwa kiwango cha lami. Lakini leo tumeambiwa kwamba, TANROAD ndio itakayohusika na ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, naomba Kauli ya Serikali kupitia Waziri wa Ujenzi, atuambie ni lini wananchi wa Nyamongo na wananchi wa Tarime watajengewa hiyo barabara ya lami?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mimi napata shida kwamba, wananchi wa Tarime, hasa Nyamongo, wanakalia dhahabu, wanalalia dhahabu, wanaamkia dhahabu, lakini wanaishi katika kiwango cha umasikini sana kwa kulipwa dola 200,000.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini, Serikali isifanye juhudi ikakaa na hao wanaoitwa wawekezaji waweze kulipwa kiwango cha hata angalau dola milioni 2 tu, zikaweza kuleta maendeleo? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Chacha Nyangwine, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nilichosema awali ni kwamba umiliki wa barabara ile uko TANROADS. Sasa kama kulikuwa na makubaliano baina ya TANROADS na Halmashauri na Mkoa na hasa kwa sababu ni barabara ya TANROADS, ya kupata ufadhili kwa ajili ya kujenga barabara hiyo ni ya lami; mimi ninachosema ni kwamba, barabara ile iko chini ya umiliki wa TANROADS na kwamba kama kuna mkataba wa kujenga barabara ile kwa njia ya lami, TANROADS watatuhakikishia.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida makubaliano kama yale hayafanywi kwa mdomo tu, kwa bla-bla! Yanafanywa kwa kuandikiana.

Kwa hiyo, mimi ninachomwambia Mheshimiwa Nyangwine, hana haja ya kuelekea kule kwenye ooh, majibu ya uongo, nk. Ushahidi wa makaratasi upo! Sasa kama wao wanasema kwamba, hawakufanya *commitment* ya kujenga kwa lami, lakini na Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wake anasema wamefanya *commitment* ya kujenga kwa lami, Serikali itakuja na maelezo na watu wa TANROADS wapo na kama makubaliano hayo yapo, yatakuwa ni makubaliano yaliyofikiwa kwa kuandikiana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutapata ufumbuzi wa suala hili kwa sababu yanatakiwa kuwa ni makubaliano yaliyohakikiwa kwa maandishi, tutapata makubaliano hayo. Sasa kama wewe unasema walikuwepo na wao wanasema hawakuwepo! Tutakuja kupata ufumbuzi huo na Mheshimiwa Waziri wa TANROADS atanisaidia nikimaliza swali langu.

Mheshimiwa Spika, hili la pili kuhusu maridhiano ya kimkatiba ya dola 200,000 kwa mwaka kwenye kila Halmashauri. Jana tu nimezungumza na Madiwani wa Geita, walikuja kuniona na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Geita kulalamikia masuala haya ya GGM kulipa dola 200,000!

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakati wa makubaliano ya kimkatiba mwanzoni mwa mwaka 2000, dhahabu bei yake ilikuwa ni kama dola 280 au 290, sasa hivi bei ile imefika mpaka 1,700! Sasa madiwani wa Geita walikuwa wananiuliza jana ni kwa nini jambo hili halibadiliki hali ya kwamba bei ya dhahabu imepanda sana! Wao wanang'ang'ania kwenye masuala ya mikatiba.

Mheshimiwa Spika, sisi tumeshakuja hapa mara kadhaa tumesema kwamba, tunaongozwa na mikatiba tuliyoandikiana wakati huo. Lakini nataka niseme, Mwezi Disemba kwenye Mkutano na Mawaziri wa Madini, Addis, kwenye *African Mining Vision*, jambo hili limekuja na tumelisemea! Mimi nilikuwa miongoni mwa waliolisemea; kwamba, *when the price of gold is changing* kwa nini vile vipengele vinavyohusiana na mapato ya dhahabu havibadiliki?

Mheshimiwa Spika, sasa kwa bahati nzuri wawekezaji walikuwepo, Serikali zao na Mabalizi wao walikuwepo na tulikubaliana kwa pamoja kwa nchi mbalimbali. Sisi tumelisemea, Ghana wamelisemea, Namibia wamelisemea kwamba, hii sio sawa! Kwa hiyo, sasa utaona hata *attitude* ya Makampuni ya dhahabu pale kwenye masuala ya *windfall gain* inabadilika. Kwa sababu kimsingi zamani ilikuwa inaonekana kwamba ukibadilisha mikatiba unakwenda kwenye kukiuka mikatiba ya *Good Governance!* Lakini sasa hivi kuna masuala ya haki ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Nyangwine, Waheshimiwa Wabunge wa Geita, Mheshimiwa Lembeli kwa upande wa Buzwagi na watu wake wa Kahama, ni kwamba hili suala ni jambo ambalo linaeleweka na limeshaanza kuzungumzwa hata kwenye *international forum* na sisi tukalikazania mpaka tupate mabadiliko kwenye masuala haya ya *commitment* za kwenye Halmashauri, *local community commitments*, lakini pia kwenye masuala ya *Corporate Social Responsibility*. (Makofi)

SPIKA: Jamani punguzeni urefu wa maswali! Tayari dakika 10 hili Swali limeshachukua, sitaweza kumpa mtu mwingine.

Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha.

Na. 110

Ahadi ya Kupeleka Umeme Mji Mdogo wa Laela

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Serikali inahimiza sana uanzishwa wa viwanda vidogo vidogo vya wajasiriamali waliopo vijijini kuongeza pato la wananchi na Taifa, sanjari na msisitizo huo, mji mdogo wa Laela ni miongoni mwa miji inayokua kwa kasi kubwa na wananchi wake wanajishughulisha na kilimo cha karanga na alizeti kwa wingi. Ili kupata mafuta yenye ubora wa kuuzwa ndani na nje zinahitajika mashine za kisasa zenye kutumia umeme, kutokana na hali hiyo Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni zake za uchaguzi mwaka 2010 aliahidi kupeleka umeme kwenye mji huo:-

(a) Je, ni lini dhadi ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa ili kurahisisha uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo kama Serikali inavyohimiza?

(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kupeleka umeme mji mdogo wa Laela ili kuwezesha ujenzi wa Ofisi za Utawala na uwakilishi wa ngazi ya Wilaya kujengwa haraka ili kusogeza huduma muhimu kwa wananchi?

SPIKA: Wastani wa kujibu swali ni dakika 5! Sasa unakuta limemaliza dakika 10 lenyewe peke yake!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mji mdogo wa Laela ulioko Wilayani Sumbawanga Vijijini, katika Mkoa wa Rukwa, ni miongoni mwa miji inayokua kwa kasi kubwa. Utekelezaji wa dhadi ya Mheshimiwa Rais umeshaanza, ambapo tathmini ya gharama za upelekaji umeme katika mji huo zilifanyika mwaka 2009 lakini zilihakikiwa mwanzoni mwa mwaka huu wa 2012.

Mheshimiwa Spika, mradi utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa KV 33 ukitokea Sumbawanga, yenye urefu wa km 137 na ufungaji wa *transfoma* ishirini na sita (26). Mradi huu utapitia katika vijiji 18 ambavyo ni Isesa, Ulinji, Malonje, Sandulula, Jangwani, Makuzani, Mpwapwa, Malolwa, Mkima, Mpui, Ikozi, Kalambanzite, Mshani, Lusaka, Ndelema, Kaengesa, Katumba-Azimio, Tamasenga pamoja na Mkunda. Gharama ya kupeleka umeme katika mji wa Laela zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 8.256.

Aidha, TANESCO imekwishapeleka kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, hivyo ujenzi wa njia za umeme utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza hapo juu, Laela ni miongoni mwa mji mdogo inayokuwa kwa kasi sana na hivyo kutimiza vigezo vyote vya kupatiwa umeme hivyo ni kweli sasa ni wakati muafaka kupeleka umeme katika mji huo ili kusogeza huduma muhimu kwa wananchi. Lakini kama nilivyoieleza kwenye kipengele (a) hapo juu, juhudi zinaendelea kufanywa ili kuupatia umeme mji huo kwa wakati kulingana na upatikanaji wa fedha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na yenye ufafanuzi mzuri. Lakini hata hivyo nina swali moja la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kufikisha umeme katika Wilaya zote nchini ambazo hazina umeme, hususan Makao Makuu ya Wilaya, ili kurahisisha shughuli za utawala?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ignas Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupeleka umeme kwenye Wilaya zote za Tanzania, uko katika utaratibu wa Kisera ambao umeanza kufanyiwa kazi na unanza kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya na baada ya hapo tunasambaza kwenye maeneo mengine kulingana na uwezo, lakini pia na vigezo mbalimbali vinavyohusu kupeleka umeme vijijini.

MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, namshukuru. Kwa kuwa, kazi ya kutoa umeme Mjini Sumbawanga kupeleka Namanyere, kupitia vijiji vya Nkundi, Kipande, Kantawa, Vilundikwa, Kasu, Kacheche na Chala, unaenda vizuri sana. Na kwa kuwa, wananchi wa maeneo hayo wana hamu kubwa ya kupata huduma hiyo. Je, Serikali inatuhidi lini wananchi hawa watakata umeme huu ambao wananchi hawa wana hamu kubwa sana nao?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwamba, ametambua kwamba mradi huu unakwenda vizuri; ni mradi mkubwa kidogo una kilometa 91, una vijiji 12 ambavyo vitapatiwa umeme. Hadi sasa *line* kubwa ujenzi wake umekamilika kwa 100% isipokuwa sasa hivi kazi inayoendelea ni kukamilisha kusimika kwa *line* ndogo zile ambazo sasa hivi zimefika 93%.

Mheshimiwa Spika, sisi tumejipanga Wizarani katika kwenda kuangalia utekelezaji wa kazi hii na kazi inayofanywa na Mkandarasi, mimi mwenyewe tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwamba, tutakapopata muda tutakwenda kuangalia utekelezaji wa kazi hii ambayo inatarajia kuwapatia umeme wateja kama 900 hivi kwa hivi sasa.

Na. 111

Fedha za ASDP – Mbozi

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Je, Serikali kupitia mpango wa kuendeleza Sekta ya Kilimo imepeleka kiasi gani cha fedha Wilayani Mbozi kwa ajili, ya uchimabji wa mabwawa pamoja na shughuli za kilimo cha umwagiliaji?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, kama ifuatavyo:-

Kati ya mwaka 2005/2006 na 2011/2012; Serikali, kupitia Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*DADPS*), Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*DIDF*) na Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Taifa (*NIDF*), imepeleka jumla ya shilingi bilioni 3,510,656,400 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Fedha hizo zilitolewa kwa awamu kama ifuatavyo:-

Mwaka 2005/2006	Shilingi milioni	26,670,881.00
Mwaka 2006/2007	Shilingi milioni	51,435,000.00
Mwaka 2007/2008	Shilingi milioni	27,200,000.00
Mwaka 2008/2009	Shilingi milioni	58,611,000.00
Mwaka 2009/2010	Shilingi milioni	896,117,600.00
Mwaka 2010/2011	Shilingi milioni	1,461,977,180.00
Mwaka 2011/2012	Shilingi milioni	<u>988,644,739.00</u>
		3,510,656,400.00

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, shilingi milioni 752,965,000 ni za ujenzi wa mabwawa na shilingi bilioni 2,757,691,400 ni za miundombinu ya umwagiliaji.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeorodhesha namna ilivyopeleka pesa za miradi hiyo kama Mheshimiwa Waziri alivyojibu. Lakini nasikitika kusema kwamba, kazi iliyofanywa hasa kwenye mabwawa ni mbaya sana! Kazi hiyo hailingani na thamani ya pesa ambazo zimekwenda.

Je, Waziri yuko tayari kwenda kuona kazi ya mabwawa iliyofanywa vibaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, ili aweze kuchukua hatua na kuwawajibisha wote waliohusika na upotevu wa fedha za Serikali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mipango yote hii ya umwagiliaji pamoja na mabwawa inalenga kuimarisha kilimo na hususan cha mazao ya chakula katika Wilaya ya Mbozi, lakini na nchini kote. Lakini

mwaka huu wakati tunalenga tuinue mazao ya kilimo hasa chakula, Serikali imepeleka mbolea kwa kuchelewa!

Lakini mbali ya kuipeleka kwa kuchelewa mbolea yenyewe imegawiwa kwa mafungu; wananchi wanalalamika kwamba, wanapewa mbolea ya palizi peke yake! Lakini DAP na mbegu ambayo ilikuwa pia haki yao, wananchi hawajapewa! Sasa wanalalamika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawaeleza nini wananchi ili waache malalamiko ambayo wanayatoa sasa hivi?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu! Hilo la pili, na mimi yamenipata huko.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali la Mheshimiwa Zambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Zambi kwamba, iko haja kabisa kufuatilia fedha zinazopelekwa Wilayani kwa ajili ya miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, na sio Mbozi tu, mimi nimepanga kuzungukia sehemu nyingi kwa sababu, ni kweli fedha zinazopitia hasa kwenye DADPS zinapeleka kwa mafungu kidogo kidogo milioni 20, milioni 20! Orodha niliyo nayo hata mimi inanionesha kwamba, miradi mingi iko katika hatua za awali tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Zambi kwamba, nimepanga tena mimi mwenyewe na ninaomba nimhakikishie, katika suala la umwagiliaji Mheshimiwa Zambi, mimi wala sidanganyi ni suala ambalo mimi mwenyewe nalifahamu vizuri, hata nikipata taarifa, sio kwamba nazichukulia tu kama zilivyo. Nitafuatilia mpaka tujue zimetumikaje na kama hazijatumika, tuweze kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea kuchelewa. Nadhani mbolea, hili ni suala pana kidogo, sio kwa ajili ya Mbozi tu! Mahali pengi, nafikiri najibu tena swali baada ya muda mfupi kuhusu mbolea, imetokea kuchelewa kutokana na vocha kuchelewa kuwafikia wakulima.

Lakini vocha pia ilikuwa sio tatizo, nafikiri nitatoa maelezo kidogo baadaye kidogo. Tatizo lililopo ni kwamba, sio mbolea kuchelewa, mbolea inafika kwa wakati! Isipokuwa changamoto zilizojitokeza ni zile vocha kuchelewa. Utaratibu tulioupeleka ni wale Mawakala nao ikawa wengi wao bado wanasita.

Lakini suala la mbolea kufika, ilifika! Isipokuwa utaratibu wa kuwagawia wakulima ambao mawakala walikuwa na wasiwasi kwamba huenda hawatalipwa, nao umechangia kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri majibu mengine zaidi nitayatoa nitakapokuwa ninajibu swali linalohusiana na mbolea, linalofuatia.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, swali halikujibiwa!

SPIKA: Swali la!

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, swali langu la pili halikujibiwa kabisa Mheshimiwa Spika!

SPIKA: Anasema kuna swali linalofuata, linalingana na hilo! Kwa hiyo, atajibu la mbolea specific.

Sasa nimwite Mheshimiwa Rajab Mbaruk.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, Mifuko hii ya DIDF na NIDF ina ukomo wake katika utoaji fedha. DIDF ukomo wake ni milioni 800!

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ilitumia vigezo gani kuweza kuwapatia fedha za ziada Wilaya hii ya Mbozi, zaidi ya hiki kiwango ambacho imejiwekea?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi yote ya maendeleo tunapoipanga na kuitekeleza, si kweli kwamba kila mradi ukishasema ni milioni 800 basi inaishia hapo hapo! Ziko factors mbalimbali ambazo zinaweza kusababisha mradi gharama zake zikaongezeka.

Sasa tunapoongeza fedha, kama ukomo ulikuwa ni shilingi milioni 800 kwa ajili ya *DIDF* na wakati mradi huo umeonekana kwamba gharama zake zinazidi hapo, tunachofanya tu ni kuhamisha kutoka sasa kwenye *DIDF* kuuweka katika lile kundi la *National Irrigation Decelopment Fund* ili tuongeze fedha kusudi mradi ule uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, hicho tu ndicho kigezo kinachotumika; *otherwise* itabidi tujikite kwenye kikomo halafu tufanye kazi ambayo haikamiliki.

Na. 112

Usambazaji wa Pembejeo Kufuatia Misimu Mbalimbali ya Mvua

MHE. CYNTHIA H. NGOYE aliuliza:-

Kalenda za kilimo nchini hutofautiana kulingana na msimu wa mvua kwa kila Mkoa au Kikanda.

Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kusimamia na kuhakikisha usambazaji wa pembejeo za kilimo hasa mbolea unafanyika kulingana na msimu wa mvua kwenye maeneo husika?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imegawanyika katika Kanda za Mazao na misimu ya mvua tofauti. Yapo maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua, yaani vuli na masika (*bimodal*) na maeneo mengine yanapata msimu mmoja mrefu wa mvua (*uni-model*). Kwa kawaida, mazao ya vuli huchangia 27% ya chakula chote katika maeneo yanayopata mvua hizo.

Serikali imeweka utaratibu unaolenga kuwafikishia pembejeo wakulima kabla ya msimu husika kuanza. Kabla ya msimu wa kilimo kwanza, Wizara yangu inawasiliana na Mikoa na Halmashauri zote nchini kupata taarifa ya mahitaji ya pembejeo za kilimo kwa aina na kiasi. Wizara inatumia taarifa hizo kuwashauri wazalishaji na waagizaji wa pembejeo zinazohitajika katika maeneo yanayohusika na kwa msimu husika.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine muhimu ni Wizara kuandaa vocha za pembejeo na taarifa muhimu zinazohusu mbolea yenye ruzuku ili ziwafikie wakulima kabla ya msimu kuanza.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mbolea yanakadiriwa kuwa tani 400,000. Hadi tarehe 3 Novemba, 2011 upatikanaji katika Mikoa mbali mbali ikiwemo yenye msimu wa vuli ulikuwa tani 246,454 sawa na 61.6% kiasi kilichobaki, tani 130,000 kilipatikana mwezi Disemba, 2011 na kupelekwa katika Mikoa inayoanza kilimo katika mwezi Januari na Februari, 2012.

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali madogo mawili kama ifuatavyo:-

(i) Katika msimu huu wa kilimo tunaouzungumzia hivi sasa wakulima wengi sana katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa na hasa katika Tarafa ninazotoka mimi huko Busokelo, Tarafa ya Kukwe huko

Mbozi, Ireje na Mbeya Vijijini, wamepanda bila kutumia mbolea, kwa sababu mbolea hii inayozungumzwa hapa haikufika kwa wakati. Je, kama ni kweli Serikali inafuata kalenda za kilimo na taarifa zinatoka Mikoani na Wilayani; kwa nini mbolea haikufikishwa kwa wakati kulingana na kalenda? (Makofi)

(ii) Kwa kuwa hivi sasa kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira; miti mingi imekatwa na kwa hiyo mvua siyo za kuaminika tena, lakini kwa mikoa michache hii ya Nyanda za Juu Kusini kama Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa ni Mikoa ambayo walau inapata mvua za kuaminika. Je, Serikali ipo tayari kuwa *serious* zaidi ili kuhakikisha kwamba Mikoa inapatiwa pembejeo zake kwa wakati tusipate tena tatizo la njaa hapa nchini? (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu kwa kifupi sana tuko nyuma ya wakati.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba tuelewane kwamba, Serikali yenyewe kama Serikali, haigawi mbolea wala haiagizi na kupeleka mbolea; tunachokifanya, mbolea hii inaagizwa kwa mfumo wa Soko Huria. Hata hiyo mbolea tunayoizungumzia ya ruzuku, hakuna mbolea iliyoandikwa ruzuku. Mbolea hiyo inaagizwa na wafanyabiashara na kuipelekea huko. Kazi ya Serikali ni kupata takwimu ambazo nimezieleza katika majibu yangu ya msingi na kuwapa hawa wafanyabiashara na kuwapa kalenda ya kilimo, ambayo ni hii hapa na nimempatia Mheshimiwa Ngoye leo asubuhi, inayoonesha mvua za vuli zinapatikana katika mikoa gani na wakati gani na mvua za masika zinapatikana katika mikoa gani na wakati gani.

Tunapotoa kalenda hii sasa wafanyabiashara ndiyo wanajiaandaa kupeleka mbolea hiyo kwa wakati huo na kulingana na msimu. Sasa kinachogomba mara nyingi hapa ni kwamba, wao nao kwa sababu wanapata fedha kutoka kwenye taasisi, wanawinda kupata uhakika na faida. Kwa hiyo, ukitazama vizuri ni kwamba, mbolea ile huwa ipo, tatizo ni hawa watu wanaoizua wanabaki wanajiuliza hivi nikiitoa sasa hivi nitalipwa malipo yangu kwa haraka au hapana. Kwa kipindi hiki ambacho kimetokea, kwa bahati mbaya vocha zimechelewa na kama nilivyosema wakati mwingine tunachelewa kupitisha bajeti hapa na sisi tunachelewa kutoa vocha, basi hilo linatokea.

Labda kwa ufupi niseme kwamba, sisi tutawasiliana na Hazina na wadau wengine, tuangalie mfumo mzuri utakaoiwezesha Wizara kupata fedha mapema ili vocha hizo ziwafikie wakulima kabla ya msimu na wale mawakala nao na wafanyabiashara wawe na uhakika kwamba watalipa fedha zao ili waweze kuuza mbolea yao kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, nadhani nimeyajibu maswali yote kwa pamoja; swali la kwanza na la pili la Mheshimiwa Ngoye.

SPIKA: Muda wenyewe unakwisha. Mheshimiwa Msabaha naomba uulize swali sijakusikia siku nyingi.

Na. 113

Wawekezaji Kuwaajiri Watanzania

MHE. MARIAM SALUM MSABAHA aliuliza:-

(a) Je, kwa nini wawekezaji wengi kutoka nje wanakuja na wafanyakazi wao?

(b) Je, kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuwalazimisha wawekezaji kutoa kipaumbele cha ajira kwa Watanzania kama ilivyo kwa nchi zingine kama Swaziland?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997, mwekezaji anaruhusiwa kuja na wafanyakazi wasiozidi watano na vilevile anaweza kuongeza kulingana na mahitaji jinsi ambavyo shughuli zake zinavyoendelea kupanuka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Sheria hii kutoa fursa kwa wawekezaji kuleta wafanyakazi, wageni hawa hufanya udanganyifu ikiwepo kufanya kazi kinyume na walizoombewa kwa kutumia vibali walivyoombea, kutumia vibali vya muda mfupi (*visitors pass*) na kutumia vibali vya kuishi kufanya kazi nchini; hivyo, kutoa taswira kwamba wanafanya kazi ambazo wazalendo wangeweza kuzifanya. Ili kupunguza tatizo hili, Wizara yangu kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji, hufanya kaguzi za mara kwa mara katika maeneo ya kazi. Vilevile katika kudhibiti ajira za wageni, Wizara inashirikiana na Asasi zingine kama Chama cha Waajiri Tanzania (*ATE*) na Chama cha Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*), ambapo kikao cha utatu hufanyika ili kupitia maombi yote ya vibali kwa ajira za wageni na kutoa vibali kwa wageni wanaostahili kupewa vibali hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika kipengele (a) hapo juu ni kwamba, kwa kutumia Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997, Serikali imekuwa ikidhibiti ajira za wageni kwa kuruhusu mwekezaji kuja na wafanyakazi watano tu na iwapo atahitaji kuongeza, ataruhusiwa tu iwapo atatoa sababu za msingi ambazo zitaonesha kama kuna umuhimu wa kupewa kibali. Aidha, Sera ya Ajira ya Mwaka 2008 imetoa kipaumbele katika kulinda na kukuza ajira kwa Watanzania kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- (i) Kuchambua kwa umakini maombi ya vibali vya wageni yanayoletwa kwa kushirikiana na wadau chini ya Kamati ya Utatu, yaani Serikali, Wafanyakazi na Waajiri ili kutoa vibali kwa wale tu wanaostahili;
- (ii) Kusimamia utaratibu wa kuhakikisha makampuni yaliyoajiri wageni yanatekeleza Programu ya Kurithisha Utaalam wa Wageni kwa Tanzania, yaani *Localization Plan*;
- (iii) Kufanya ukaguzi mara kwa mara katika maeneo ya kazi ili kubaini kama wageni wanaofanya kazi ni wale wanaostahili; na
- (iv) Kuimarisha, kukuza na kutunza taarifa za soko la ajira ili kusaidia kutoa maamuzi sahihi ya utoaji wa vibali vya ajira.

MHE. MARIAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru pia kwa majibu mazuri, yenye matumaini kwa vijana wetu. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Wananchi wamekuwa wakilalamikia wamiliki wa hoteli nyingi za kitalii na migodi iliyotuzunguka kuchukua wafanyakazi kutoka mbali lakini wale majirani hawapati ajira. Je, Waziri atanihakikishiaje na Wananchi hawa waliozungukwa na migodi na hoteli kubwa za kitalii nao watanufaika na ajira? (*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa tuna vijana wengi hapa Tanzania ambao ni wasomi wa Vyuo Vikuu na wamehitimu vizuri masomo yao; na kwa kuwa tumeona nafasi muhimu zinachukuliwa na wageni na vijana wengi wanabaki katika kazi ambazo hazina tija. Je, Waziri atanihakikishiaje na Vijana wa Tanzania wananufaika na nafasi muhimu katika sekta hiyo? (*Makofi*)

SPIKA: Kwa kifupi siyo kwa kirefu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, kama ifuatavyo:

Kuhusu hoteli na migodi kutochukua wafanyakazi kutoka maeneo ya jirani, hili suala limekuwa likizungumzwa. Kaguzi zetu na tafiti ambazo tumefanya kwenye maeneo hayo na mimi juzi juzi nilikuwa kwenye Hoteli katika Kanda ya Kaskazini, zimeonesha kwamba, kazi nyingi hasa za chini wanachukua wafanyakazi walioko jirani. Suala la ajira kwa ujumla ni uwezo na watu kushinda katika *interview* na kama kazi ni za kitaalam, huwezi kulazimisha wachukue kutoka sehemu za jirani. Kwa maeneo ambapo kazi ni za

kawaida, za chini, wanachukua katika maeneo ya jirani. Tutaendelea kusisitiza hilo ili wale wanaozunguka maeneo haya hasa vijana wapate ajira.

Kuhusu wageni kuchukua kazi ambazo Watanzania wanaweza kufanya, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi; tulikuwa tukifanya kaguzi kuangalia wanaofanya kazi zile ni wale tu ambao kazi zile ama ni kwa kutokana na Sheria ya TIC ama ni kazi ambazo Watanzania hawawezi kufanya. Hii ndiyo maana juzi nilipofika kule Manyara, nilipokuta mgeni amejiriwa kupaka rangi (*vanish*), nilipiga kelele na juzi nilisikia ameshaondoka nchini. Hii yote ni kwa sababu kazi ya kupaka rangi inaweza kufanywa na Mtanzania na kazi zingine zote zinazoweza kufanywa na Mtanzania siyo vizuri zikafanywa na wageni. Tutaendelea kufanya kaguzi ili lisiwe tatizo kwa Watanzania.

Na. 114

Vyombo vya Habari Kutafsiri Lugha za Ishara

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR aliuliza:-

Watu wenye ulemavu wa kusikia ni wengi na kwamba na wao wana haki ya kupata taarifa mbalimbali za nchi yao kupitia katika Vyombo vya Habari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuagiza Vyombo vya Habari vya Televisheni kuanza kutafsiri Lugha ya Ishara ili watu wenye ulemavu wa kusikia waweze kujua mambo yanayotokea nchini mwao?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nakiri kwamba upo umuhimu wa kuwepo Wakalimani wa Lugha ya Ishara kwa ajili ya jamii yenye ulemavu wa kusikia.

Mheshimiwa Spika, Seriakli inakamilisha Marekebisha ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya *Electronic* na Posta ya 2010 (*Electronic and Postal Communication Act (EPOCA)*), ambazo zitavitaka Vyombo vya Habari vyote kuwa na Wakalimani wa Lugha ya Ishara. Kukamilika kwa Kanuni hizi kutafanya uwepo wa Wakalimani hao Kisheria; hivyo, kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa wito kwa Wamiliki wa Vyombo vya Habari nchini kufanya jitihada za makusudi ili kuwawezesha Wananchi wote kupata habari kwa mujibu wa Ibara ya 18(d) na Ibara ya 30(1)(2)(a)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa Katiba, watu wenye ulemavu wana haki sawasawa na Mwananchi mwingine yeyote wa Tanzania; na kwa kuwa hivi sasa Nchi yetu ya Tanzania ipo kwenye mchakato wa kupatikana kwa Katiba mpya na watu wengi Katiba ya zamani hawajui; na kwa kuwa Vyombo vya Habari vinatoa mijadala kwa watu mbalimbali katika kuelimisha kuhusiana na mchakato wa Katiba hii; lakini hao watu wenye ulemavu wa kusikia sijui kama wanasikia maana inatoka kwenye *television* sasa wanaona tu labda lakini hawasikii na wao wana haki:-

Je, Serikali itawasaidia vipi watu hawa wenye ulemavu wa kusikia na wenye ulemavu wengine ili waweze na wao kuwa huru katika kujadili mchakato huu wa Katiba Mpya ya Tanzania?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu kwa kifupi sana, nina maswali sita na muda ni mchache.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, labda nianze kwa kusema kwamba, jibu langu la msingi la kwanza nimeelezea kabisa kwamba, tunashughulikia kanuni itakayothibitisha na kusimamia Vyombo vya Habari na kuhakikisha wanaweka watu ambao wanaweza

kutafsiri lugha mbalimbali au michakato mbalimbali inayoendelea katika Vyombo vya Habari ili watu ambao wana matatizo ya ulemavu ya kusikia na kadhalika, waweze kupata habari kama Wananchi wengine wanavyoweza kupata.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nichukue nafasi hii pia nielezee kwamba, pamoja na hiyo kanuni kuwa bado haijashughulikiwa rasmi, vipo Vyombo vya Habari mbalimbali ambavyo tayari vimeshaanza kushughulikia mchakato. Kwa mfano, TBC na ITV ambavyo vinarusha Vipindi Maalum vyenye Wakalimani wa Lugha ya Ishara kama vile vipindi vya wape nafasi na kipindi cha wape nafasi kinatayarishwa na mtu ambaye ana ulemavu, anakishughulikia kile kipindi na anawaelekeza wenzake na watu wengine wanaweza kuelewa kinachoendelea.

ITV pia ina kipindi cha matukio ya wiki kinachorushwa kila wiki na pale kuna mtu anayetafsiri Lugha za Ishara. Ahsante.

Na. 115

Uhaba wa Walimu Wenye Taaluma ya Elimu Maalum

MHE. MARGARET AGNES MKANGA aliuliza:-

Kukua kwa uelewa wa wazazi juu ya umuhimu wa kusomesha watoto wenye ulemavu kumechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la uandikishaji wa watoto hao pamoja na changamoto zilizopo za uhaba wa walimu wenye taaluma ya elimu maalum katika ngazi zote za elimu:-

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza udahili wa wanachuo katika Chuo cha Ualimu Patandi pekee cha Serikali kinachoandaa walimu wenye taaluma maalum?

(b) Je, Serikali inakubaliana nami juu ya kufundisha elimu maalum kwa walimu watarajiwa wote ili kuondokana na changamoto hiyo ya uhaba wa walimu hao?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nitoe ufafanuzi kuhusu kozi za elimu maalum ambazo hutolewa katika Chuo Ualimu Patandi. Kozi hizi hutolewa katika ngazi ya cheti mwaka mmoja na stashahada ya miaka miwili. Walengwa wa kozi hizi ni walimu ambao wako kazini na wana uzoefu katika ya ualimu. Kozi zitolewazo zimegawanyika katika makundi matatu kama ifuatavyo; wasiona, viziwi na ulemavu.

SPIKA: Naomba utulivu ndani ya nyumba, naona kila mtu anasambaratika na kitu gani sijui.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Sifa za kujiunga na mafunzo ya elimu maalum ngazi ya cheti ni ufaulu wa masomo ya sayansi katika kiwango cha kidato cha nne. Aidha, sifa maalum za kujiunga na mafunzo ya kujiunga na mafunzo maalum ngazi ya stashahada ni ufaulu wa masomo ya sayansi katika kiwango cha kidato cha sifa, hususan masomo anayofundishwa katika shule za sekondari, yaani O - Level na kuwa na uzoefu kazini usiopungua miaka mitatu.

Pamoja na sifa zilizotajwa, walimu wanaochaguliwa kujiunga na mafunzo haya wanatakiwa wawe na upenzi, nia na uwezo wa kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu.

Mheshimiwa Spika, udahili wa wanachuo katika vyuo vya ualimu unategemea uwezo wa chuo husika. Chuo cha Ualimu Patandi kina uwezo wa kudahili jumla wanafunzi watano kwa mwaka. Katika kipindi cha miaka miwili, hali ya udahili wa wanachuo mwaka 2010/2011 walimu 289 waliochaguliwa kujiunga na mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti na kati ya hao walimu 248 waliripoti na kuendelea na masomo. Kwa ngazi za stashahada waliochaguliwa ni walimu 104 na waliripoti kuendelea na masomo ni

walimu 67. Mwaka huu wa fedha walimu ngazi ya cheti, waliochaguliwa ni walimu 450 na walioripoti ni 257. Kwa ngazi za stahhada walimu 150 walichaguliwa na walioripoti walikuwa 55 tu. Aidha, kuna chuo kisicho cha kiserikali kilichoko Lushoto, Mkoani Tanga, kinachoitwa *Sebastian Kolowa University College (SEKUCO)*, kinachotoa Shahada ya Ualimu wa Elimu Maalum.

Mheshimiwa Spika, udahili huu umeshindwa kufikia uwezo wa chuo kutokana na sababu mbalimbali; baadhi ya sababu hizo ni pamoja na upungufu wa walimu uliopo shuleni unosababisha baadhi ya waajiri, yaani wakurugenzi kushindwa kuwaruhusu walimu hao kwenda masomoni na baadhi ya walimu kushindwa kuchangia gharama za mafunzo kutokana na sababu za uchumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea wazo hili lililotolewa na Mheshimiwa Mbunge kuhusu kuongeza udahili kujumuisha na wanachuo tarajali. Hata hivyo, kwa wakati huu kuna changamoto ambazo zinakabili ufundishaji wa masomo ya elimu maalum. Utekelezaji wa wazo la Mheshimiwa Mbunge, linahitaji kufanyiwa utafiti wa kitaalamu kuona namna ya kuanzisha mafunzo ya ualimu wa elimu maalum kwa wanachuo tarajali.

MHE. MARGARET AGNES MKANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ambayo ni marefu kabisa; nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(i) Tunafahamu elimu ni msingi wa maisha na ni haki ya kila mtoto hapa nchini kutokana na sera zetu. Je, Serikali inafahamu kwamba hata hao wachache wanaojitolea kwenda kusoma; maana hapa wamesema kujitua na nini; wanaojitolea na kwenda kusoma pamoja na uhaba wa fedha na nini wakimaliza kozi zao wakirudi kwenye maeneo kuna baadhi ya maafisa wanawapanga walimu hawa kwenye shule zingine ambazo hazina vitengo vya watu wenye ulemavu; kwa hiyo kuendeleza ule upungufu na kukosesha watoto hawa haki yao ya elimu?

(ii) Nashukuru Serikali imekiri upungufu huu na kwamba itajitahidi kufanya utafiti. Je, utafiti huu ambao Serikali imekiri hapa kwamba kuna umuhimu wa kuufanya; utanza lini ili uingize hata *programme* ya kuwa na shule za kiwango cha *degree* badala ya kuiachia tu *SEKUCO* peke yake?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu kwa kifupi kwa sababu majibu yenu yalikuwa marefu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Margaret Mkanga, kwa namna anavyofuatilia shughuli za watu wenye ulemavu. Napenda vilevile nimpe faraja kwamba, baada ya Serikali kuhudumia masuala ya elimu katika ngazi za Halmshauri kuendeshwa na TAMISEMI na Wizara ya Elimu kubaki na Sera na mambo mengine na Vyujo vya Ualimu, lakini tayari kuna Kamati inayoitwa Kamati ya Ugatuuji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, inayoshirikiana na Wizara ya Elimu, wanapanga mambo haya ikiwa ni pamoja na changamoto hizi. Ilikuwa kwamba, walimu wakienda kusoma Patandi au Chuo cha *SEKUCO*, wanarudi kwenye Kurugenzi zao kuendelea kufundisha kwa sababu Wakurugenzi walikuwa wanawahitaji.

Kwa mwaka huu wa fedha, hilo tumeliona, ilikuwa ni changamoto tayari Walimu wote waliokuwa wamemaliza mwaka 2009/2010 na mwaka 2010/2011, tumeshawapangia kwenye Shule Maalum ili kuweza kutoka kule na kufundisha kitu ambacho wamekisomea. Pia ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kabla ya mwisho wa mwezi huu, tayari atanza kuona walimu wanamiminika na tumeshaanza kuwapanga kwenda kufundisha kwenye shule za Elimu Maalum.

Swali la pili kuhusu utafiti utanza lini; hili nadhani linakwenda na masuala ya bajeti, mwaka huu wa fedha tutaliweka kwenye bajeti ili baada tu ya Bunge la Bajeti tuanze utafiti.

Na. 116

Uandishi wa Katiba

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA aliuliza:-

- (a) Je, ni kikundi gani tofauti na Bunge ambacho kinaweza kuandika Katiba ya Nchi?
- (b) Je, kikundi hicho kitakuwa na uhalali gani?
- (c) Je, kitatoka katika jamii gani kati ya Wasomi, Wanasiasa, Wakulima, Wafanyabiashara na Wafanyakazi wa kawaida?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Nchi ni Kanuni za Msingi zinazotungwa kwa ridhaa ya Wananchi kwa madhumuni ya kuweka Mamlaka ya Nchi, mgawanyo wa Mamlaka kati ya Mihimili mitatu ya Dola, kuweka majukumu ya vyombo vingine vya umma na pia kuweka dira ya nchi. Katiba inatungwa kwa kuzingatia mchakato maalum na kwa kuzingatia mazingira halisi ya nchi yaliyopo wakati Katiba inatungwa.

Katiba inaweza kutungwa kwa madhumuni ya kuleta maridhiano kati ya vikundi ambavyo vimetoka katika mapambano ya vita kama ilivyo kwa Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Congo. Aidha, Katiba ya Nchi inaweza kutungwa kwa nia ya kuleta maridhiano baina ya makundi ambayo yanapingana katika nchi kutoka na tofauti ya itikadi zao kwa madhumuni ya kupata mwafaka wa kisiasa. Katiba inaweza pia kutungwa kwa madhumuni ya kutaka kuwa na Katiba Mpya baada ya Katiba iliyotangulia kuwa imetumika kwa muda mrefu na kutokana na mahitaji mapya ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, kutahitaji Katiba itakayozingatia hali halisi ya wakati husika. Katiba inayotungwa kwa madhumuni ya kuingiza matarajio mapya, huwashirikisha wadau wote katika nchi.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa uandishi/utungaji wa Katiba ya Nchi ni mchakato, Bunge pekee haliwezi kutunga Katiba ya Nchi. Katiba ya Nchi itatungwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali likiwemo Bunge kwa kuzingatia mazingira halisi ya nchi. Misingi ya uandishi wa Katiba huanzia katika kukusanya maoni ya wadau mbalimbali. Maoni hayo hutafsiriwa katika Rasimu ya Katiba ambayo huandaliwa na Wataalamu hatimaye Bunge la Katiba kujadili kifungu kwa kifungu cha Rasimu ya Katiba na hatimaye kuipitisha. Katika mifumo mingine, uandishi wa Katiba, wananchi/wadau hupata fursa ya kupiga kura ya maoni (*referendum*), ambayo matokeo yake ndiyo yanahalalisha Katiba Mpya.

(b) Kwa kuwa siyo mtu au kikundi cha watu pekee kitakuwa na Mamlaka ya kutunga Katiba, uhalali wa kutungwa Katiba unatokana na mchakato mzima na wala siyo kikundi kimoja katika jamii.

(c) Kwa kuwa Tanzania tupo katika mchakato wa maandalizi ya kutunga Katiba Mpya, ambao nchi yetu tunatarajia kufanya hivi karibuni; makundi yote ya kijamii yatashirikishwa katika hatua mbalimbali za mchakato huo yakiwemo makundi aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri katika swali hili lakini hata hivyo, napenda kuuliza maswali mawili madogo.

(i) kwa kuwa Serikali imekiri kwamba Katiba hutungwa kwa kujumuisha makundi mbalimbali wakiwemo Wananchi; na kwa kuwa Wananchi wengi hawaelewi Katiba ya sasa; na kwa kuwa nchi inajiandaa kuandika Katiba mpya; je, Serikali itayasaidiaje makundi na asasi za kiraia kutoa elimu hii kwa Wananchi ili waweze kutoa maoni yao kwa usahihi?

(ii) Je, Serikali itanza lini kusambaza nakala za Katiba za kutosha ili Wananchi watumie wakati wa kutoa maoni kwenye Tume ya Maoni? Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mbunge wa Dole, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Wananchi hawaifahamu vizuri Katiba ya sasa na ili waweze kutoa mchango mzuri zaidi kuelekea Katiba Mpya ni lazima waipate hiyo Katiba na waisome na kisha waelimishwe. Kwa hiyo, kama nilivyowahi kujibu swali hili katika kikao hiki hiki nilisema kwamba, Wizara ya Katiba na Sheria hivi sasa inaandaa nakala za Katiba ambazo zitasambazwa nchi nzima ili kuwawezesha Wananchi kupata uelewa wa Katiba ya sasa na kuandaa kwa ajili ya kutoa maoni ya Katiba Mpya. Nakala hizo zitaanza kusambazwa muda si mrefu na hata baada ya kuundwa kwa Tume ya Kukusanya Maoni, moja ya kazi hiyo itakuwa ni kutoa elimu; kwa hiyo, kutakuwa na vipeperushi ambavyo vitasambazwa kwa ajili ya kuwawezesha Wananchi kushiriki katika mjadala wa Katiba Mpya.

Na. 117

Kuimarisha Usafiri wa Reli Mpanda

MHE. SAID AMOUR ARFI aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiahidi kila mara kuimarisha usafiri wa reli ambapo hali ya reli Kaliua/Mpanda ni mbaya sana kiasi cha kuhatarisha maisha ya watu na mali zao:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hizo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Serikali inafanya juhudi za kuimarisha huduma za usafiri wa reli hasa kwenye Reli ya Kati inayojumuisha Tawi la Kaliua - Mpanda. Serikali tayari inatekeleza ahadi yake ya kuimarisha usafiri wa reli ya Kaliua/Mpanda, yenye urefu wa kilomita 210, ambayo imejengwa kwa reli za uzito mdogo wa pauni 45 kwa yadi. Serikali inabadilisha uzito huo kuwa zaidi ya pauni 56 kwa yadi. Hadi kufikia mwaka 2011, jumla ya maeneo yenye urefu wa kilomita 33.9 yamebadilishwa. Maeneo hayo ni Kaliua - Lumbe km. 5, Lumbe - Ugalla River km. 8.5, Ugalla River - Katumba km. 13.4 na Katumba - Mpanda km. 7.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ina Kambi za Magenge Kaliua, Lumbe, Ugalla River na Katumba ili kuimarisha utendaji kazi na ina vitendea kazi vyote zikiwemo *Motor Trolleys* tatu ambazo imekodi kutoka *TRL* kwa ajili ya kusafirisha wafanyakazi kwenda maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kuweka reli za uzito wa pauni 80/yd badala ya zile za pauni 56 kwa yadi, umbali wa kilometa 80 kati ya Kitaraka hadi Malongwe, utawezesha kupatikana reli na mataruma ya pauni 56 yatakatayotumika kubadilisha urefu uliobakia wa Reli ya Kaliua/Mpanda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi pia amekuwapo Mkandarasi kwa muda mrefu sasa toka tarehe 16 Oktoba 2008, ambaye anafanya kazi za kusafisha njia ya reli, kupigilia reli, kuimarisha tuta la reli, kusafisha mifereji ya maji ya mvua na kuondoa mchanga relini kabla na baada ya mvua kuonyesha, kubadilisha reli zinazochakaa, kuondoa vifungio vilivyolegea na kufunga vilivyo imara. Kazi nyingine anazozifanya ni kusafisha na kuzibua makalvati na madaraja, kukagua njia ya reli kila baada ya mvua kunyesha ili kuhakikisha usalama wa njia, kubadilisha mataruma ya mbao zilizoza na kufanya kazi nyingine za dharura kwa maagizo au maelekezo ya Mhandisi wa Reli Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri; Kampuni ya Reli (*TRL*), imo katika jitihada za kuongeza safari za garimoshi katika Reli ya Kati, sambamba na zile za Kaliua - Mpanda ambapo safari za sasa ni tatu kwa juma na kila safari ina mabehewa sita na mabehewa ya mizigo 13.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, Watanzania na hususan Wananchi wa Mpanda wameshachoshwa kabisa na hizi ngonjera zinazotolewa kama majibu ya Serikali.

(i) Kwa kipindi cha miaka sita ambayo nimekuwa Bungeni na kila mwaka nikiulizia suala la reli wametengeneza kilomita 33.9 katika umbali wa kilomita 210 kutoka Kaliua mpaka Mpanda kwa wastani wa kilomita tano kwa mwaka. Kwa maana hiyo, kilomita 210 ni miaka 40. Sasa ni lini kama swali lilivyoulizwa ambalo halijajibiwa; watakamilisha kazi hiyo?

(ii) Katika majibu aliyoyotoa Mheshimiwa Waziri ambayo hayamo katika maelezo aliyokuwa amenipa, ameeleza juu ya mabehewa na usafiri wa reli, lakini anasema kwamba tutahitaji sana upatikanaji wa fedha. Je, Watanzania wanaposikia kwamba mnajenga daraja la shilingi bilioni 300 na mkaacha kuiimarisha reli kweli mna utashi wa kuondoa matatizo katika nchi hii? *(Makofi)*

SPIKA: Hilo daraja la shilingi bilioni tatu ni wapi?

MHE. SAID AMOUR ARFI: Ni Daraja la Kigamboni, bilioni 300 kwa ajili ya matajiri watakojenga Mji wa Kigamboni.

SPIKA: Haya unagonganisha watu! Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana kwani tupo nje ya wakati.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Amour Arfi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa muda mrefu tumejitahidi kuweka mipango ya kuiimarisha reli na ndiyo maana tukaingia hata mkataba na mwekezaji. Sasa haya yamekwisha, tupo katika mpangilio wa kuiboresha reli yetu wenyewe. Haya niliyomweleza Mheshimiwa Arfi ni mambo ya muda mfupi sana; ni mambo ambayo tutayatekeleza kwa muda mfupi iwezekanavyo.

Nimewaambia kuwa, kuna mataruma ambayo tunayatoa kutoka sehemu za Singida na sehemu za Tabora kuyapeleka kule kuimarisha ili Reli ya Kaliua - Mpanda ifikie uzito wa reli wa pauni 56 kwa yadi, lakini haya ni ya muda mfupi. Kama tulivyoeleza wakati wa kuwasilisha wakati wa bajeti yetu, kikubwa tunachotaka kukifanya sasa ni kubadilisha mfumo mzima wa reli zetu. Naomba watuamini hivyo; kwani tuna miaka minne bado ya kufanya kazi hiyo, tumeshapita kila mahali kukutana na wawekezaji ambao watatusaidia kufanya kazi hiyo, tupo katika mikakati ya mwisho ya kutafuta ni yupi ambaye tufanye naye kazi hiyo.

Naomba muwe wavumilivu mwone tutafanya nini baada ya miaka mine. Reli hii tunataka tuiboreshe itoke kwenye reli nyembamba tuliyonayo sasa hivi iende kwenye *standard gauge* ya mita 1.435, ambayo itaweza kwenda kuruhusu treni za *speed* kilomita 120 kwa saa zipite hapo na kuweza kuchukua mizigo mikubwa ambayo ipo Rwanda, Burundi na hapa Tanzania. Tunaelewa sisi Serikali kwamba, uchumi wa nchi hii unategemea sana ubora wa reli hii sambamba na bandari na hiyo, ndiyo kazi ambayo tunaifanya.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 118

Ajali Mbalimbali Nchini

MHE. MASOUD ABDALLA SALUM aliuliza:-

(a) Je, ni ajali ngapi zimetokea Barabarani kuanzia Januari 2011 – Oktoba 2011?

(b) Je, ni ajali ngapi zimetokea Baharini kuanzia Januari 2011 – Oktoba 2011?

(c) Je, ni ajali ngapi zimetokea kwenye Maziwa kuanzia Januari 2011 – Oktoba 2011?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Jumla ya ajali ambazo zimetokea katika kipindi cha Januari hadi Oktoba 2011 kwenye usafiri wa barabara zimesababisha vifo 2,831 pamoja na majeruhi 10,196.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, samahani, hivi viboksi usivisome tutamgawia, maana yake ni kila mwezi kwa miaka mitatu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kama ulikuwa kichwani kwangu, sitavisoma.

Hizi ni wastani wa ajali 2,066 vifo 283 na majeruhi 1,016 kwa mwezi. Hata hivyo, mtiririko wa ajali unaonesha kupungua kwani katika kipindi chote hicho ajali chache zilitokea mwezi Oktoba mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ajali za majini na vyombo vya usafiri ambavyo *SUMATRA* imepata taarifa zake katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari – Oktoba 2011; jumla ya ajali 13 zilitokea Baharini ambapo watu 230 walipoteza maisha na 1,125 waliokolewa.

Miezi iliyokuwa na ajali ni Januari ajali tano, Mei ajali tatu, Julai ajali mbili, Agosti ajali moja na Septemba ajali mbili.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, ajali tatu zilitokea kwenye Maziwa ambapo watu wanane walipoteza maisha na 19 waliokolewa na ajali hizi zilitokea moja kila mwezi katika mwezi Januari, Mei na Julai. Mwelekeo wa kupunguza ajali unaonesha ufanisi wa hatua za *SUMATRA* na vyombo vingine vya dola katika kudhibiti tatizo hili. Hata hivyo, hatua za ziada zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikisha Taasisi na Asasi zake, imechukua hatua mbalimbali za kupunguza ajali ikiwa ni pamoja na:-

- (a) Kutengeneza Kanuni na taratibu za usimamizi zinazolenga kuweka vigezo vya usalama na kupunguza ajali;
- (b) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya usafiri wa majini na nchi kavu;
- (c) Kutoa elimu kwa wamiliki, wasafiri na watoa huduma za uchukuzi kuhusu mambo ya kuzingatia katika kutoa huduma na haki za watumiaji wa huduma hizo; na
- (d) Kuchukua hatua mbalimbali kwa wanaokiuka taratibu na masharti ya uendeshaji wa vyombo ikiwa ni pamoja na kuttoa leseni kwa vyombo ambavyo havikidhi vigezo na adhabu kwa wanaokiuka taratibu hasa za ujazaji abiria katika vyombo vya uchukuzi.

Nawaomba na kuwasisitizia watoa huduma na watumiaji wa vyombo hivi kwamba, waheshimu na kuzingatia Sheria na Kanuni ili ajali zizidi kupungua.

SPIKA: Mheshimiwa Masoud, swali la nyongeza, lakini hapo muda angalieni wenyewe!

MHE. MASOUD ABDALLA SALUM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa vilio vimekuwa vikisikika kila wakati kutokana na ajali za baharini, barabarani na kwenye maziwa; na kwa kuwa miezi mitatu ya mwisho wa mwaka 2011 kuanzia mwezi wa Oktoba hadi Desemba jumla ya Watanzania 1,086 walikufa, watu 5,005 walijeruhiwa kutokana na ajali za barabarani; na kwa kuwa vyanzo vya ajali hizo vinaeleweka ni pamoja na ulevi wa madereva, mwendo kasi na leseni feki. Je, Serikali ina mpango gani wa ziada wa makusudi wa kuhakikisha kwamba wanadhhibiti vyanzo vya ajali hiyo?

(ii) Kwa kuwa kulikuwa na Msiba wa Kitaifa uliotokana Mv. *Spice Islander* tarehe 10 Septemba uliopelekea nchi yetu kupeperusha bendera nusu mlingoti, Watanzania 2,760 walikufa na 920 waliokolewa; lakini Mheshimiwa Waziri anasema watu waliokufa kutoka kwenye taarifa ya *SUMATRA* ni 230. Mheshimiwa Waziri; je, Watanzania hawa 2,760 hawako katika takwimu yako ya Watanzania na huoni kwamba hukuwatendea haki Watanzania wa Zanzibar kutotaja marehemu hawa?

SPIKA: Hebu uliza swali moja kwa moja! Haya majibu, tena kwa kifupi maana tunakula muda mwingine.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumejizatiti kukabili tatizo hili kwa juhudi zote; sasa hivi *SUMATRA* imeongeza mfumo wa kutoa adhabu za ziada siyo tu pale ajali zinapotokea lakini hata pale tunapoonza kuwa mwelekeo unakwenda kwenye ajali kwa kuhakikisha kuwa kila anayesafirisha, ambaye anarudiarudia mambo ambayo yanatufanya tuamini sisi yeye anaanza ku-*practice accident*, tumzuie kabla *accidents* hizo hazijatokea.

Juzi nilieleza hapa ni leseni ngapi za magari ambazo zimefutwa na ni kampuni ngapi ambazo zinahusika, hatuishii huko tunakwenda pia kwa madereva wenyewe na leseni za sasa za madereva zinatusaidia katika hilo.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo hapa ni Januari hadi Oktoba 2011 lakini lile la *MV Spice Islander* halikuwekwa hapa kwa sababu wakati inatayarishwa hii taarifa ilikuwa haijathibitika bado.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 119

Kero Ulipaji wa Vivuko

MHE. DAVID E. SILINDE aliuliza:-

Huduma ya kuvuka madaraja na mito hapa nchini ni bure katika maeneo mengi lakini katika Jimbo la Mbozi Magharibi kuvuka katika Mto Momba uliopo kati ya Kata ya Kamsamba na Kijiji cha Kijamatundu Wananchi hulipishwa shilingi 500, pikipiki shilingi 2,000 na mizigo pia huchajiwa kulingana na ukubwa wake:-

- (a) Je, Serikali itawasaidiaje Wananchi wa maeneo hayo kuondokana na kero hiyo?
- (b) Je, ni lini Serikali itajenga daraja la kudumu na la uhakika kwa kuwa daraja la kamba lililopo siyo zuri kwa usalama wa Wananchi?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zetu zinaonesha daraja la watembea kwa miguu (*cable supported pedestrian bridge*), linalounganisha Vijiji vya Kamsamba na Kilyamatundu, linamilikiwa na kusimamiwa na Uongozi wa Kanisa Katoliki lililopo Kamsamba. Hivyo, Wizara yangu haina taarifa kuhusu malipo wanayotowza Wananchi kwa kuvushwa katika Daraja hilo. Aidha, Serikali imeanza maandalizi ya kujenga daraja la kudumu katika Mto Momba kwa kukamilisha kazi ya usanifu wa kina wa daraja hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, usanifu wa Daraja la Mto Momba, lenye urefu wa mita 75 litakalounganisha Barabara za Mkoa wa Sitalike – Kilyamatundu Mkoani Rukwa na Mlowo - Kamsamba Mkoani Mbeya, umekamilika mwaka 2011 kwa gharama ya shilingi milioni 164.7. Kazi za usanifu wa Daraja la Mto Momba imegharamiwa na Serikali ya Denmark kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimatifa

(DANIDA). Baada ya kukamilika kazi ya usanifu wa Daraja hilo, Serikali inatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuwezesha kuanza kwa ujenzi wa Daraja hilo ambalo litakuwa la kudumu na la uhakika.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa katika majibu ya Waziri kipengele cha (a) ni kwamba, hawana uhakika, lakini taarifa zilizo sahihi niweke tu vizuri ni kwamba; Wananchi wanalalamika na wanaendelea kutozwa mpaka sasa. Kwa hiyo hii ni kuweka taarifa sahihi.

(i) Mwaka 2009, Awamu ya Kwanza ya Rais Jakaya Kikwete, alizuru eneo hilo na kuahidi ujenzi wa daraja hilo mara moja. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezeka kwa asilimia mia moja?

(ii) Kwa kuwa ahadi nyingi sana zimekuwa zikitolewa na Mheshimiwa Rais na hazikamiliki kwa wakati mwafaka; je, Serikali sasa haioni ni wakati mwafaka wa kuziandikia kitabu ahadi zote alizozitoa na kuainisha gharama halisi na muda utakaotumika kuzitekeleza?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa kwamba, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi na ndiyo maana katika jibu langu la msingi, sehemu (b) nimesema, *feasibility study* na *detailed design study* ya daraja hilo linalounganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Rukwa zimekamili na jumla ya fedha ambazo zimetumika ni shilingi 164.7. Lengo ni kuhakikisha kwamba, daraja pale linatengenezwa. Katika ujenzi wa daraja, unaanza na *feasibility study*, unakuja na *detailed design*, halafu unakuja na *construction*. *Feasibility study* na *detailed design* ndiyo zimefanya kujua urefu wa eneo hili ni mita 75. Serikali itaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali kuhakikisha daraja lile linatengenezwa kwa sababu ni muhimu kwa Wananchi kule.

Kuhusu ahadi nyingi ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Rais kwamba zinatakiwa ziandikiwe kitabu; ahadi zote za Mheshimiwa Rais zimeandikiwa kwenye Kitabu cha Ilani ya Uchaguzi, ukurasa wa 85 hadi wa 93, zinazohusu barabara na madaraja na kwa bahati nzuri hadi sasa hivi utekelezaji wake ni mzuri sana. Mpaka sasa hivi zaidi ya kilomita 11,174 zinajengwa kwa kiwango cha lami na katika Miradi hiyo ambayo kwa sasa hivi inatakiwa kufunguliwa au kuwekewa mawe ya msingi ni miradi 54 katika nchi nzima, yenye *cost* ya zaidi ya shilingi trilioni 3.880. Kwa hiyo, ahadi za Mheshimiwa Rais zinatekelezeka na zinatekelezwa kulingana na utekelezaji wa kweli. Nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kutoa ahadi ambazo zinatekelezeka. (Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumekula muda wa kazi nyingine, sababu kubwa ni majibu marefu na maswali ya nyongeza yanayokuwa hotuba; kwa hiyo, naomba siku zijazo mtuangualie kwa sababu wastani wa kila swali kujibiwa ni dakika tano. Nikiangalia orodha yangu hapa inafika 10, 15, hamuwezi kumaliza kwa wakati. Kwa hiyo, tunazingatia wale waliouliza swali la msingi angalau swali lao liulizwe kuliko ninyi mnaodandia maswali ya wenzenu basi pumzikeni.

Ninao wageni kama ifuatavyo:-

Wageni waliopo Ukumbi wa Spika ni Mheshimiwa Didas John Massaburi, Mbunge wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Meyi wa Jiji la Dar es Salaam. Yuko wapi? Ahsante. (Makofi)

Ninaye Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Katibu wa Umoja wa Nchi za Maziwa Makuu aliyemaliza muda wake. Ahsante, tunakupongeza kwa kazi nzuri uliyofanya kipindi hicho chote na tunakutakia kheri katika kipindi kingine.

Mwingine aliyeko kwenye *Speaker's Gallery* ni Dkt. Edmund Mndolwa, Kamishna wa Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Bodi ya *Kenya Commercial Bank*. Ahsante sana, tunashukuru ni swali ambalo huwa linafika sana hapa Bungeni.

Mwingine tuliyenaye pale ni Mheshimiwa Muttamwega Bhatt Mgaywa, Mbunge wa zamani kupitia Chama cha *TLP* na aliyekuwa Mgombea Urais kipindi hicho. Ahsante sana. Tulikuwa naye hapa Bungeni, alikuwa anatupa changamoto za kutosha. (Makofi/Kicheko)

Tunao wageni kumi wa Mheshimiwa Edward Lowassa, wanatoka *Tanzania Association of Managers and Owners of Non Governmental Schools and Colleges*, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Mahmoud Mringo. Hawa wako wapi sijui? Ahsante sana, tunashukuru. (Makofi)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Dustan Mkapa, ambaye ni Chifu Mkonona kutoka Lupaso, Masasi, ambaye ameambatana na mkewe Ndugu Ahano. Sasa Mheshimiwa Chifu uko wapi na ametoka rasmi na mavazi ya Kichifu hivyo! Ahsante sana. (Makofi/Kicheko)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan, ambao ni Wachezaji na Viongozi wa Timu ya *Villa Squad Sports Club* ya Kinondoni Dar es Salaam. Timu hiyo itacheza na Timu ya Polisi ya Dodoma kesho tarehe 11 Februari 2012. Nyote mnakaribishwa. Timu hiyo iko wapi? Nafikiri wamekosa nafasi, kwa hiyo, Wabunge itabidi muahirishe safari mkaone huo mchezo. (Makofi)

Kuna wageni wa Mheshimiwa John Cheyo, ambao ni Bwana na Bibi Buitter kutoka *Botech Project Management*. Hawa wako wapi? Okay, nadhani wamekosa nafasi humu ndani. Kuna mgeni wa Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, ambaye ni Prof. Joseph Mbwiliza kutoka Chuo Kikuu Huria Tanzania. Huyu pia alikuwa Mbunge kipindi fulani na sisi hapa. Karibu sana. (Makofi)

Nina mgeni wa Mheshimiwa Amina Makilagi, ambaye ni Ndugu Hellen Bogoye - Mjumbe wa Baraza Kuu ya U.W.T. Sijui yuko wapi? Ahsante karibuni sana. (Makofi)

Wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 75 na walimu kutoka Shule ya Sekondari ya Hijra Dodoma. Wanafunzi wa Hijra na walimu naomba wasimame. Okay. Ahsante sana, tunawatajia masomo mema na mmependeza sana. (Makofi)

Tunao wanafunzi 65 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; naomba walipo wasimame wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ahsante sana, tunawashukuru sana na tunawaomba mkazane kusoma, mwisho wa siku kila mtu na maisha yake. Yale ya ujumla ujumla huwepo mwishoni mwa safari, someni watoto wetu ili nchi iweze kufaidika na elimu yenu. Ahsanteni sana. (Makofi)

Tuna Wakufunzi wawili kutoka *Algonquin College of Hospitality and Tourism* cha Canada, ambao ni Prof. Sandy Oullete na Prof. Rebecca Volk, wakiwa na wenyeji wao Betram, Eriyo na Cyril Mjindo kutoka VETA Dodoma. Hawa wageni wetu wako wapi? *We are pleased to have you*; naamini mtakuwa na maisha mazuri wakati mkiwa na sisi hapa, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho wa matangazo ya wageni.

Tuna matangazo ya kazi: Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa, kutakuwa na kikao leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa "B".

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Momose Cheyo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma na Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara wataochaguliwa na Wenyeviti wao kuwa, leo saa saba mchana, kutakuwa na kikao cha pamoja kitakachofanyika katika Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, hapa kuna Kamati tatu nadhani wanaohusika wanajifahamu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba watakuwa na mkutano katika Chumba Namba 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa, watakuwa na kikao kitakachofanyika saa nane mchana katika Ukumbi Namba 227. Anaomba mhudhurie.

Waheshimiwa Wajumbe, hapo ndiyo mwisho wa matangazo.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOSES J. MACHALI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa kufanya nini wakati hatujafanya kitu. Ehe! Mheshimiwa nani; maana unajua kuna mwongozo tumefanya nini mbona tumeuliza maswali tu? Mheshimiwa Machali, tusiwe na muda wa kupoteza sasa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, hapana siyo muda wa kupoteza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Natumia Kanuni ya 68(7), juu ya jambo ambalo limejitokeza asubuhi ambalo limekuwa linaonekana kuweza kujirudia rudia wakati baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri wetu wanapokuwa wanatujibu maswali hapa kuna majibu ambayo unakuta kabisa kwamba hayajakidhi matakwa na mahitaji ya hali halisi.

Kwa mfano, wakati swali namba 111 na 112 yakijibiwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, alieleza kuhusiana na masuala ya vocha za pembejeo za kilimo imekuwa ni kawaida ya kutupatia majibu kwamba, watachukua hatua, lakini wakulima wetu wanaendelea kupata shida. Sasa nilikuwa ninaomba Bunge lako liridhie wakati mwingine Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa niaba ya Serikali watueleze watachukua hatua gani ili kuweza kukomesha tatizo hili la vocha kuchelewa kila wakati wakulima wetu wanatusumbua sisi Waheshimiwa Wabunge tatizo liko kwao Wizarani. Nilikuwa naomba Serikali ije itupatie majibu vinginevyo tutakuwa tunataniana na kudanganyana mahali hapa. Ahsante.

SPIKA: Haya sasa siyo hoja; sijui ombi; sijui ni kitu gani Serikali imesikia.

MHE. YUSUPH A. NASSIR: Mheshimiwa Spika, ni kwa mujibu wa Kanuni hiyo hiyo ya 68(7), naomba kunukuu: "Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge yeyote anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa hapo hapo."

Mheshimiwa Spika, mbele yetu kuna hoja inayohusiana na Zao la Mkonge.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, naomba nikukatishe, hatujafika huko; Kanuni inasema usiwahishe kazi ya Spika.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Ahaa! Tafadhali, tusifanye mchezo jamani.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, niliomba mapema.

SPIKA: Uliomba nini?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Niliomba mwongozo wako mapema sana.

SPIKA: Kwanza, sijakuona haya sasa endelea.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, leo tunamaliza Bunge, kwa hiyo, nimekuwa nafuatilia yanayotokea ndani ya Bunge na hususan majibu ya Serikali hasa Wabunge tunaposimama kuuliza maswali yanayohusiana na maeneo mapya ambayo Serikali inatarajia kuyaanzisha hususan mikoa. Sasa wapo Mawaziri wanapojibu maswali wanasema mathalani Mkoa wa Katavi, Geita, Simiyu au Njombe.

Mheshimiwa Spika, sasa kinachosumbua haya mambo yanakwenda kwenye *Hansard*; ninaomba Serikali au Mheshimiwa Spika utupe mwongozo wako kama mikoa hii ipo au namna gani; maana haya yanarekodiwa na yanabaki historia kwa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

SPIKA: Hiyo mikoa ilitangazwa, nafikiri Serikali itatangaza Viongozi wa Mikoa hiyo rasmi. Kwa hiyo, watu wana hamasa kutaka kuona kama wako katika sehemu ya mikoa yao, lakini nadhani Serikali inakamilisha mambo yake hayo.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 (The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2011)

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Jana tulipokuwa tumeahirisha kipengele kilichokuwa hakikukamilika katika Kamati ya Bunge Zima, niliomba Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala, waweze kukaa pamoja na wengine waweze kufikia mahali ambapo tunafikiri tunamaliza Muswada wetu bila ya matatizo.

Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati au Makamu wake, aweze kutoa matokeo ya kikao kile; Mheshimiwa Angellah Kairuki.

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kutoa taarifa kwamba kazi uliyotupangia jana jioni tumeimaliza na tumeweza kufikia mwafaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulikutana jana usiku baada tu ya kuahirisha Bunge mpaka saa 6.00 usiku ili kuweza kujadili hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge, iliyokuwa inahusu Jedwali la Marekebisho ambalo aliliwasilisha Bungeni kupendekeza kufanyia mabadiliko kifungu kidogo cha (c) kilichopo katika sehemu (b) ya Jedwali la Marekebisho ya Serikali linalopendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 17(5) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya majadiliano ya kina baina ya Wajumbe wa Kamati, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge na Wabunge wengine waliohudhuria katika kikao cha Kamati kama vile Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Shellukindo, pamoja na Mheshimiwa Stella Manyanya, hatimaye mwafaka ulifikiwa kwa Kamati kumshauri Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kukubaliana na mapendekezo ya Serikali; hivyo, Kamati ikaishauri Serikali kukifuta kifungu cha aya ya "C" sehemu ya "B" na kukiandika upya kifungu hicho kama inavyosomeka kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilimshauri Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa katika kifungu kidogo cha 9 kinachopendekezwa aya ya (a) kuongeza maneno Mkuu wa Wilaya mara baada ya maneno kwa niaba yake na popote yanapoonekana katika kifungu hicho kidogo cha 9.

Mheshimiwa Spika, kwa mabadiliko hayo, yatakfanya kifungu cha 17(5) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 kisomeke kama ifuatavyo:-

(a) Kwa upande wa Tanzania Bara, kumtaka Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Afisa Mtendaji Kata au Mtaa au Afisa Mtendaji wa Kijiji, kuitisha mkutano wa wakazi wa Mji, Kata, Mtaa au Kijiji, kwa vyovyote itakavyokuwa. Mwafaka huo pia uliridhiwa na upande wa Upinzani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana. Naishukuru Kamati kwa kazi nzuri na wale wote waliohiriki pale. Kwa hiyo, tunaendelea.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko

ya Katiba wa Mwaka 2011 [The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2011]

Ibara ya 3, Sehemu C, Section 17

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala alivyosema jana jioni, na nusu ya usiku wa jana Kamati ilikutana na tulikubaliana kufanya marekebisho katika kifungu hicho kama ifuatavyo:-

Kwenye kifungu (c) kwenye Jedwali la Marekebisho, ile section 17 sasa kisomeke kama ifuatavyo:-

"A bill entitled the "Constitution Review Amendment Act, 2011" is further amended in subparagraph (c) which appear under item B of the "schedule of amendments" by:-

- (a) *deleting paragraphs (a) and (b) and substituting for them the following paragraphs"*
 - (a) *inserting after the designation "District Commissioner" which appear in paragraph (a) of subsection (5), the designation "a Director of Local Government Authority; and*
 - (b) *inserting after the designation "District Commissioner" which appear in paragraph (b) of subsection (5), the designations "Municipal Director, Clerk to the Town or District Council."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Tunachosema ni kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Katiba unafanyiwa Marekebisho ya nyongeza kwenye aya ndogo ya (c) ambayo inajitokeza kwenye aya ya (b) ya Jedwali kwa:-

- (a) kufuta aya za (a) na (b) na kuweka badala yake aya zituatazo:- Wale walio na Sheria.
- (a) kuingiza baada ya maneno Mkuu wa Wilaya ambaye anajitokeza kwenye aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (5) maneno "Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa", na
- (b) kuingiza maneno "Mkuu wa Wilaya: yanayojitokeza kwenye aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (5), maneno "Mkurugenzi wa Manispaa, Katibu wa Halmashauri ya Mji na au Wilaya."

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho pia yanakwenda kwenye aya ya (c) kuingiza baada ya maneno "kwa niaba yake" au kwa Kiingereza yanasomeka: *"in that behalf"* yanayojitokeza kwenye kifungu kidogo cha (9) kiko kwenye mabadiliko yaliyoletwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, maneno "Mkuu wa Wilaya" popote yanapojitokeza kwenye kifungu hicho kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nizungumze athari ya mapendekezo haya ya Serikali. Athari ya kinachopendekezwa ni hiki kifuatacho:-

Katika Wilaya moja yenye Mkuu wa Wilaya na yenye Mkurugenzi, hiki kifungu cha (1) kitaitaka Tume inapotaka kuitishiwa mikutano aidha iende kwa Mkuu wa Wilaya au iende kwa Mkurugenzi. Wilaya moja inatoa *option* ya watu wawili wa Serikali ile ile, una-*create confusion*. Hiyo ni ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili ni kwamba kwenye hiki kifungu kinachohusu taarifa kwa wanaotaka kwenda kutoa elimu kwa umma. Mtu anayetaka kutoa taarifa ya elimu kwa umma, aidha aende kwa Mkuu wa Wilaya au aende kwa Mkurugenzi kwenye Wilaya hiyo hiyo. Kwa hiyo, wapo watakaokwenda kutoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya, kuna wengine watakaokwenda kwa Mkurugenzi. Ni Wilaya moja, halafu hawa watu wawili wa Serikali moja inabidi sasa wapeleke hizo taarifa kwenye Tume ya Katiba kwamba Mheshimiwa Mbowe ameniletea taarifa mimi Mkurugenzi, Mheshimiwa Nagu ameniletea mimi DC, *is a confusion*. Tunatengeneza na tunaona aibu tu ya kushindwa kutunga Sheria nzuri ili kulinda

watu isionekane kwamba tumeshindwa, tumekubaliana kila kitu! Tunatengeneza Sheria mbaya itakayoleta mgogoro *in practise! It is simply bad legislation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipendekeza kwamba tuangalie Wabunge, Sheria mliyoipitisha mwaka jana, kifungu cha 17(2)(d) kinailazimisha Tume kuitisha mikutano. Hilo ndilo jambo la msingi la Tume. Ina jukumu la kuitisha mikutano. Ina *mandatory duty to convene meetings*. Sasa kwanini tusiachie Tume iamue kuitisha mikutano yake? Ina Sekretarieti, ina watumishi, ina magari ina *loud speaker*, inaweza ikatengeneza mabango ya mikutano ikapeleka matangazo ya *radio*, ikafanya kazi badala ya kuleta hii *confusion* ili watu fulani fulani wasionekane wameshindwa kwa kumbeba huyu kada wa CCM Mkuu wa Wilaya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu. Nadhani mnakuwa *emotion too much* katika kitu ambacho mmekaa, mmeongea, taarifa imetolewa na ilikuwa kusudio letu hili. Sio kurudi tena kwenye *debate* ya ajabu. Mheshimiwa Lukuvi, *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri *spirit* ya kuongeza orodha ya watu watakaopewa taarifa au ambao wanaweza wakatumika, maana wanaweza wakatumika na Tume kuitisha mikutano, ni kwa sababu tu kwamba wananchi watakaopenda. Tume inaweza ikamtumia mtu yeyote kulingana na mazingira yaliyopo. Nataka nimfahamishe aliyetoa hoja kwamba kuna Wilaya ambazo zina Mkuu wa Wilaya mmoja, lakini Halmashauri tatu. Sasa kama wako kwenye eneo la Halmashauri ambako Mkuu wa Wilaya hayupo, wasilazimike kwenda Makao Makuu huko mbali kumfuata Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi yupo. Sasa wanaweza wakatoa taarifa kwa Mkurugenzi badala ya kumfuata Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Wakuu wa Wilaya ni wachache sana ukilinganisha na Halmashauri zilizopo, kwa hiyo, hii ni *option*. Anayetoa taarifa Tume ataamua yupo katika eneo gani na katika hao waliotajwa kwenye Sheria, yupi yupo jirani naye. Sana sana huyu Mkuu wa Wilaya ni *protocol* tu kwa tabia, tumeona hata ninyi viongozi wa vyama mkienda Wilayani bila kujali vyama huwa mna-*pay courtesy call*. Kiitifaki huwa mnakwenda kumsalimia Mkuu wa Wilaya, tuncendelea. Kwa hiyo, mimi nafikiri, kwa sababu Wilaya hizi madaraka haya makubwa wamegawana hawa wawili, lakini hawa Wakurugenzi wapo wengi.

Ni busara tu kwamba wote wawepo na hawa kwa sababu wanafanya kazi kwa kuhusiana, watawasiliana. Lakini Wakurugenzi ni lazima wawepo kwa sababu Wakurugenzi wapo wengi zaidi na wapo kila mahali ukilinganisha na Wakuu wa Wilaya ambao wapo wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naafiki wote wawili wawepo ili kurahisisha hilo.

MWENYEKITI: Nadhani hatuelewani. Kwa tatizo hili, labda mambo haya mengine yameandikwa Kiingereza na mengine yameandikwa Kiswahili. Anayewatumia hawa tunaosema, siyo Tume ndiyo inawatumia hawa? Tume inaweza ikawaacha, ikawatumia, ama ikafanya nini. Waheshimiwa msifanye kazi mliyofanya usiku ambayo haina kazi. Tume ndiyo ina hiari ya kuwatumia hawa watu ama kutokuwatumia. Ndivyo lilivyotumika hapa, *unless* mmebadili. Mwanasheria Mkuu, hebu tueleze tena, maana tunafanya wananchi waelewe kama kuna kitu hapa. Hakuna hata kitu!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi inanihuzunisha kwa sababu Mheshimiwa Tundu Lissu jana tulikuwa naye. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Halima Mdee alikuwepo. Mimi nilifundishwa kunyamaza wakati mtu mwingine anazungumza. Hii hoja ni rahisi mno na mimi nasema kama nilivyosema jana kwamba nia yetu hapa ni kuwa na mchakato ambao hauleti giza kwa watu. Nimesoma Sheria na nimeahidi kutumia elimu yangu niliyosoma bila kupotosha watu. Kifungu kinachohusika hapa kinatoa ridhaa ya kutumika au kutotumika. Neno "yaweza" ni la Kiswahili. Jana ulitumia neno moja siji "*succours*", katika Kiingereza, hakuna neno kama hilo. Halipo!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, tuwe na heshima ya Bunge. Wote mnyamaze, wote mtulie, tuncendelea na kazi. Tumsikilize mmoja mmoja tutapata mantiki. *(Kicheko)*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria...

Waheshimiwa Wabunge tuheshimu kiti. Katika Mamlaka za binadamu hawa ndio wakubwa wetu. Tuheshimu. Sheria inasema 'Tume yaweza.' *Actually* inaweza isiwatumie hao watu. Sasa hiki sio kitu cha kusimama hapa na kuzungumza mpaka mishipa inapanda wakati wewe mwenyewe jana usiku ulikuwepo na hukupinga. Basi kama ulipinga, mawazo yako hayakusikika.

Mimi nasema hivi, namshukuru sana Mheshimiwa Mbowe, ninaomba niseme ukweli. Mheshimiwa Mbowe jana alikuja hapa wakati ambapo kulikuwa na moto. Akaniambia kitu ambacho na mimi nilikwenda kumwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu na nawashukuru sana hawa. Ni lazima tuwe na moyo wa ku-*compromise* na kutukana haisaidii kitu. Mimi nakuheshimu sana Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini kama ukiwa na nidhamu utakuwa Mbunge mzuri sana. Kwa sababu kwanza kumwonyesha mtu kidole ni kinyume cha kanuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niliseme hili wazi, yeye ni ndugu yangu, lakini hapa kama unavyojua, hakuna cha undugu. Hapa ni Kanuni pamoja na Sheria. Kwa hiyo, bila kwenda kwenye itikadi za vyama, mimi sina chama chochote cha siasa. Bila kwenda kwenye hiyo, lakini ni Wakili wa Serikali ya CCM, hiyo lazima ieleweke wazi na mkipata ninyi mtaniteua tena mimi nitakuwa *neutral*. Kwa hiyo, maneno yale mimi nashangaa na nawashukuru sana Waandishi wa Habari niliowaona leo kwenye Jambo Tanzania asubuhi. Wanasema haya mambo tunayogombea ni madogo mno. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba tukubaliane na makubaliano yaliyofanyika kwenye Kamati kwa sababu Mheshimiwa Tundu Lissu hakuwa peke yake. Kulikuwa na watu wengine kutoka CHADEMA na walikubali.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote, kwanza niseme tu kwamba ni bahati mbaya sana kwamba tumefika hapa.

MWENYEKITI: Bahati mbaya nini?

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Nasema ni bahati mbaya tumefikisha malumbano haya katika *level* hii. Ni mambo ambayo yangestahili tuwe tumeyamaliza mapema zaidi. Lakini napenda kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhitimisha kama ifuatavyo, kwa sababu lazima tufikie muafaka. Lakini lazima tufikie muafaka, wakati huo huo tukiweka *on record* ni nini hofu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho tumekizungumza tangu mwanzo ni kujaribu ku-*avoid politicization* ya hii *process* ya Katiba. Hiyo ndiyo imekuwa hoja yetu. Tunatambua nafasi ya Mkuu wa Wilaya kama kiongozi wa Serikali katika Wilaya. Lakini vilevile tunatambua kwa uchungu sana utendaji wa Wakuu wetu wa Wilaya katika Wilaya. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunapokuwa tunatoa hofu zetu, tafadhari, tunategemea na tunaamini busara za upande wa pili zitakuwa zinatuelewa. Mkurugenzi wa Wilaya ni Mtendaji wa Serikali na Serikali iliyopo madarakani leo ni Serikali hiyo hiyo ya Chama cha Mapinduzi. Ni watendaji wa Serikali kwa misingi kwamba hawa wanasimamia shughuli za maendeleo za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokuwa kwenye Bunge leo na Serikali, ama Wabunge wanaotokana na Serikali wakaonyesha kutokuwaamini Wakurugenzi wao, ni bahati mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, tunakubali yaishe. Lakini, tuelewane kwa sababu uungwana lazima tufikie mahali. Hatuwezi kulumbana hapa mwaka mzima. Tunakubali kwa misingi ya ndani ya Bunge, yaishe. Kwa misingi ya kwisha maana yake nini? Katika hatua ya sasa tunalazimika, na narudia hili neno na mlielewe vizuri (*copy me*), tunalazimika kukubaliana na mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lakini, tunapenda kuweka *on record* kwamba huu utaratibu wa "kufunika kombe mwanaharamu apite", utatu-cost sisi kama Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki tu kuonekana tuko *naughty*, kwamba yaani tuko tu wapinzani, tunabisha, tunakataa kila jambo, lakini tunapenda kuiweka *on record* na Waheshimiwa Wabunge naomba mnielewe kwenye hili. Tutakubaliana kwa misingi kwamba tunataka ugomvi huu ama mabishano haya, kwa *spirit* ambayo tumeianza jana, tuyamalize. Lakini, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, Wabunge wenzangu wa CHADEMA, Chama cha CUF, TLP, UDP na NCCR –Mageuzi, utamaduni huu

tunaoujenga wa kufunika kwa sababu tunaogopa ku-address the primary contradiction, na primary contradiction hapa ni the fact kwamba tuna-politicize the process ya kubadilisha katiba yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua ya sasa, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani, tukubali yaishe. Twendeni tukatengeneze katiba ya nchi, twendeni tukatambue kwamba katiba ya nchi ni important kuliko vyama vyetu, twendeni tukatengeneze katiba ya nchi tukijua kwamba tunakwenda kutengeneza instrument ya kuliongoza Taifa hili for the next hundred years, beyond the life span of CCM, possible behind the life span of CHADEMA or any other political establishment. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru! (Makofi)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi niseme mambo machache tu. Nimefurahishwa kwa kiwango kikubwa na kauli ya Kiongozi wa Upinzani kwamba lazima tu-compromise, kwa sababu kutunga sheria ni ku-compromise, ni give and take. Kwa hiyo, tunapofika mahali tuka-compromise, maana yake kuna wengine wametoa, wengine wamepokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilitaka kusahihisha jambo moja tu la kwamba upande wa Serikali hauna imani na Wakurugenzi wa Wilaya. Nasema sio kweli. Wakurugenzi wa Wilaya ni sehemu ya Watendaji wa Serikali, na upande wa Serikali hatuna sababu hata kidogo ya kutokuwa na imani na Watendaji wa Serikali katika ngazi ile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba tunachofanya hapa, tunaulizana, tunamweka Mkurugenzi au DC, nani ana mamlaka gani na nani anafanya kazi namna gani? Hiyo ndiyo hoja. Lakini, kwamba tuna kundi maalum, hatuna imani nalo, nasema hiyo siyo sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hiyo, nakubaliana na Leader of Opposition kwamba tu-compromise, tufikie hapo, twende mbele. Ahsante sana. (Makofi)

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana mahali tulipofikia. Naomba niseme kwamba naunga mkono hoja ya marekebisha ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nia yangu ieleweke kwamba nilipokuwa nasema Mkuu wa Wilaya, ilikuwa ni kupanua wigo na pia kuheshimu mtiririko wa utawala wa Serikali yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na Wabunge wote mniunge mkono, tuunge mkono mapendekezo ya Serikali yaliyoletwa asubuhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Kuna mapendekezo yaliyowekwa na Serikali. Kwa maana hiyo, alishaondoa yeye ya kwake, amekubaliana na haya ya Serikali. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuweke record sahihi. Seriously mkiacha hicho mnachokiweka vichwani mwenu ninyi wote, sisemei nani au nani, hicho mnachokiweka katika vichwa vyenu hakiko kwenye sheria, kabisa. Tume “inaweza”, neno hilo inaweza kufanya ama inaweza isifanye.

Waheshimiwa Wabunge, lakini mmelifanya jambo likaonekana ni kubwa kabisa, wananchi wote wanashangaa tunafanya nini. Kweli, hamuitendei haki nchi hii. Wote kwa pamoja hamuitendei haki nchi hii!

Madaraka makubwa tunayotoa ni kwa Tume yenyewe. Haya hii “inaweza”, si neno ambalo linatufanya sisi tugawanyike au mkaenda kufanya siasa, unajua hawa walifanya hivi, hawa walifanya hivi. Jamani haina maana. Tutunge katiba hii bila kuingiza vikwazo vyovyote na hakuna cha “funika kombe mwanaharamu apite.” Halipo! “Funika kombe...” Kwanza mimi Kiswahili chenyewe sikijui, lakini haina maana yoyote. (Makofi)

Jana usiku AG alifanya marekebisho kuhusiana na kile kifungu kilichosema “Katiba ya sasa”, akasema “katiba inayokuja”. Hatukuwa tumehoji. Kwa hiyo, ninapohoji hii, ninahoji na ile pia.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)
(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011
*(The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2011)***

(Kusomwa Mara ya Tatu)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa hoja, naomba kwa ruhusa yako kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa haya waliyoamua. Lakini pia nawaomba wengi hasa vijana wafanye tafiti za kutosha juu ya namna ya utendaji wa Bunge lenye vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna alivyosaidia kutufikisha hapa tulipofikia. Lakini pia niwashukuru Wanadhimu wa vyama ambao niliongea nao wote pamoja na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Mbowe, nakushukuru sana kwa maneno yako uliyosema jana na uliyosema leo asubuhi. Mwenyezi Mungu akuzidishie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 *(The Constitutional Review Amendment Act, 2011)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na mabadiliko yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011 *(The Constitutional Review Amendment Act, 2011)* kama ulivyorekebishwa, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)
(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika safari tuliyokuwa tumenuia kufika. Kama ninavyosema ndugu zangu, hili ni swali kubwa sana, midomo yetu wanasiasa, hasa wanasiasa wenyewe Wabunge, inaweza kubomoa ama kujenga. Maana tuna midomo mizuri kabisa, tukianza kusema, kusema huko watu wanatuamini kwa kila kitu.

Sasa naomba jamani kwa maslahi ya nchi, tuseme kilichopo kwa lengo la kwenda mbele na siyo kurudi nyuma. Kwa hiyo, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ninyi wote kwa moyo mlioonyesha katika hatua tuliyofikia. Kwa namna ya pekee, naomba niishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kufanya kazi bila kuchoka katika kipindi chote na wengine wamekesha sana.

Nashukuru Kambi zote kwa kufanya kazi nzuri. Kazi hii nzuri tuipeleke hivyo kwa wananchi kusudi wawe na uhuru wa akili yao kutoa maoni yao kuhusiana na mchakato huu. Wawe na uhuru, maana tukiweka sisi pilipili, uhuru wao utakuwa mgumu sana kuufanyia kazi. Tuwaache wawe huru. Atakayeelewa

vyovyote vile, aelewe hivyo kwa sababu kutakuwa na wengine ambao wataweza kumwelimisha zaidi kuliko sisi kutia chumvi mahali mbapo chumvi imetosha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mimi nawashukuruni sana. Huu umoja tunaotakiwa kufanya, tuufanye mpaka mwisho wa safari hii. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

HOJA BINAFSI ZA WABUNGE

Hoja Binafsi ya Mhe. Kabwe Zuberi Zitto Kuhusu Hali ya Zao la Mkonge Nchini

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kufuatia kusudio langu ambalo nilileta kwako kuwasilisha Hoja Binafsi kuhusiana na hali ya zao la Mkonge nchini na kwamba Bunge liazimie kwamba mwaka 2012 uwe ni mwaka wa kupanda Mkonge, naomba kutoa maelezo ya awali.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeshuhudia kuporomoka kwa kasi ya sarafu yake kutokana hasa na kuongezeka kwa kasi ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje tofauti na kasi ndogo ya uuzaji wa bidhaa nje.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Benki Kuu ya Tanzania, mpaka mwezi Septemba Mwaka huu, 2012 uagizaji wa bidhaa kutoka nje ulifikia Dola za Marekani bilioni 10.8 wakati mauzo ya bidhaa nje ya Tanzania ilifikia Dola za Kimarekani bilioni 6.7 tu. Hali hii inahitaji mkakati maalumu siyo tu kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje, bali pia kuongeza kasi ya mauzo ya bidhaa nje.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza mauzo nje ni muhimu Taifa liwe na mikakati ya bidhaa mojamoja na hasa bidhaa za kilimo ambazo pia zitasaidia kupunguza tatizo la ajira nchini na kupunguza umasikini Vijijini.

Hivi sasa Taifa linategemea kwa kiasi kikubwa mauzo nje yanayotokana na dhahabu na madini mengine ambapo mchango wake ni takriban nusu ya mauzo nje wakati mchango wa kilimo katika kukuza mauzo nje umekuwa ukiporomoka mwaka hadi mwaka. Ni dhahiri kwamba Tanzania inahitaji kuongeza mchango wa mazao ya kilimo katika mauzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kilio kikubwa kwa vijana wa Tanzania hivi sasa ni ajira. Takwimu zinaonyesha kwamba katika jumla ya Watanzania milioni 42 waliopo katika taasisi mbalimbali za elimu kuanzia shule za msingi mpaka vyuo vikuu, wanafikia Watanzania milioni 12. Hawa wote wanapaswa kuandaliwa shughuli za kufanya ili waweze kupata ajira au kujijiri na kuendesha maisha yao na Taifa letu pia.

Mwaka 2010 takribani asilimia 50 ya vijana waliomaliza Kidato cha Nne hawakufaulu na wengi wao wapo vijijini bila ajira. Ajira na hasa ajira kwa vijana ni changamoto kubwa inalolikabili Taifa letu kwa sasa. Mikakati yote ya kiuchumi ambayo Taifa linafanya ni lazima ijibu swali la ajira kwa vijana. Sekta ya Kilimo ndiyo ambayo inaweza kuajiri vijana wengi zaidi na kupunguza tatizo la ajira nchini kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, masuala haya mawili (kuongeza mauzo nje na kuongeza ajira kwa vijana) ndio yamenisukuma kuleta hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Zao la mkonge ni zao ambalo linaonyesha dalili zote za kujibu changamoto hizi mbili kwa kiasi kikubwa sana. Mkakati maalumu kwa ajili ya zao la mkonge na baadaye mazao mengine kama Pamba, Chai, Korosho, Kahawa na kadhalika, utalisaidia Taifa la Tanzania kukabili changamoto za kuondoa umaskini kwa kuongeza uuzaji wake nje na kupanua nafasi za ajira kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa kipindi kirefu ilikuwa ikiongoza kwa uzalishaji wa Mkonge Duniani. Shamba la kwanza la mkonge nchini lilianzishwa mwaka 1900 kwenye kitongoji cha Bushiri Wilayani Pangani. Kuanzia hapo, zao hili likaenea kwa kasi na kulimwa kibiashara katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Kilimanjaro, Pwani, Lindi, Mtwara, Arusha, Mara, Mwanza na Shinyanga. Zao la Mkonge lilikuwa kwa haraka hadi kufikia kuwa zao kuu na muhimu katika uchumi wa Tanganyika chini ya ukoloni wa Kijerumani na Kiingereza na baadaye Tanganyika huru.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1964 Tanzania ilizalisha tani 230,000 za mkonge na hivyo zao hili lilifanya Tanzania kuongoza ulimwenguni katika uzalishaji na mauzo nje. Mwaka huo wa 1964 mkonge ulichangia asilimia 65 ya mauzo ya nje, hivyo kuiletea nchi fedha nyingi za kigeni.

Hivyo, Mkonge ulikuwa ni zaidi ya dhahabu kwa sasa katika mauzo nje na hata ajira. Zao hili liliweza kutoa ajira kwa watu zaidi ya milioni moja kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini na nchi nyingine za Afrika.

Kwa watu wa Kigoma wanakumbuka kwamba kwa kuwa Wakoloni waligeuza Kigoma kuwa eneo la kutoa ajira kwa mashamba ya mkonge (*labor reserve*), koo za watu wa Kigoma zimezagaa katika Mikoa ya Tanga, Morogoro na Kilimanjaro. Leo huwezi kuandika historia ya Mkoa wa Kigoma bila kutaja Mkonge na *Sisal Labor Bureau (SILABU)*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mkonge umekuwa ukipanda na kushuka kwa nyakati tofauti kabla na baada ya Uhuru kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, mdororo wa uchumi duniani wa mwaka 1930 na 2009, mageuzi ya kiuchumi duniani pamoja na matumizi ya singa bandia (*synthetic fibres*). Uzalishaji wa juu ulifikia tani 230,000 mwaka 1964 na kushuka hadi kufikia tani 20,489 mwaka 2000.

Baada ya kukamilika kwa zoezi la ubinafsishaji wa mashamba yaliyokuwa chini ya Mamlaka ya Mkonge Tanzania mwaka 2005, uzalishaji ulianza kupanda na kufika tani 33, 327 mwaka 2007. Athari za mdororo wa uchumi duniani za mwaka 2008/2009 zilisababisha kushuka tena kwa uzalishaji hadi kufikia tani 24,676 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, wakati mwaka 1964 Mkonge ulichangia asilimia 65 ya mauzo ya Tanzania nje, mwaka 2010 Mkonge umechangia asilimia 0.1 ya mauzo nje ambapo ni takribani dola za Kimarekani 11,000,000 pekee zilizoingizwa na zao hili. Hali hii inapaswa kubadilishwa kwani Mkonge una faida nyingi sana na bei yake katika soko la dunia inazidi kupanda siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, faida za zao la mkonge, zao la mkonge ni zao linalostawi vizuri katika mazingira yoyote isipokuwa maeneo yanayotuamisha maji. Kwa hali hii, mkonge unaweza kukua hata sehemu ambazo ni kame kiasi cha kutoweza kustawisha mazao mengine. Ingawa zao la Mkonge linahitaji wafanyakazi wengi ila halihitaji mtaji mkubwa isipokuwa katika hatua za mwanzo. Kwa ujumla zao hili lina sifa kuu zifuatazo:-

(i) Mkonge ni zao la asili na rafiki wa mazingira, ambalo linaweza kumsaidia mwanadamu vizuri zaidi kuliko bidhaa bandia ambazo zinaharibu mazingira.

(ii) Ni zao ambalo halina msimu maalum wa kupanda, hivyo kupelekea kuweza kupandwa wakati wowote na linapokuwa tayari kwa kuvunwa pia linaweza kuvunwa wakati wowote bila kuathirika. Hivyo, ni zao ambalo linaweza kumpatia mkulima kipato cha uhakika katika kipindi chote cha mwaka.

(iii) Mkonge ni zao linalostahimili magonjwa na halidhuriwi kirahisi na magugu na majanga mengine kama moto. Pembejeo kama mbolea, viugugu na viuatilifu katika mazingira ya kawaida sio lazima kutumika ingawa matumizi yake yanaongeza uzalishaji na mavuno ya mapema. Ni zao rahisi kulilima na kulitunza na halina upotevu wa mazao baada ya kuvuna (*no post-harvest losses*).

(iv) Zao la Mkonge linaweza kuchanganywa na mazao mengine ya msimu kama kunde, mahindi, maharage, alizeti, njegere, karanga, na kadhalika. Hii inamwezesha mkulima kupata mazao ya chakula na biashara kwa kipindi ambacho mkonge unakuwa bado haujakomaa. Hivyo, kumpatia mkulima kipato cha ziada kwa eneo moja. Kutokana na uchanganyaji wa mazao mkulima anapunguza kiasi cha wafanyakazi watakaohitajika kulima mazao ya chakula na biashara. Kwa lugha nyingine, mkulima anaongeza tija kwa eneo.

(v) Kama nchi, tuna uzoefu na utaalum katika kutunza, kusindika na kuuza mkonge wa zaidi ya karne moja. Aidha, tafiti na huduma za ugani zipo nchini kwa kupitia Chuo cha Utafiti wa Kilimo cha Mlingano ambacho ndicho Kituo pekee cha Utafiti wa Zao la Mkonge Duniani siyo Tanzania peke yake ni dunia nzima Tanzania peke yake ndiyo ina kituo cha utafiti wa zao la mkonge. Hivi karibuni, Kituo cha

Utafiti cha Mlingano kimepata vifaa vya kisasa ambavyo vinakiwezesha kituo hicho kuzalisha mbegu bora za mkonge kwa njia ya maabara (*Meristematic Tissue Culture*).

(vi) Ni zao ambalo halina uhaba wa vipando. Mara baada ya kuvunwa, miundombinu ya usindikaji wa zao hili inakuwa hapa hapa shambani.

(vii) Bidhaa zitokanazo na Mkonge zinaweza kuhifadhiwa katika mazingira ya kawaida kwa zaidi ya miaka kumi bila kupoteza ubora wake.

(viii) Zao hili linaweza kuchakatwa hapahapa nchini na kuweza kutoa bidhaa zenye matumizi mbalimbali na kwa sasa kuna soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

(ix) Mkonge una matumizi mengi, unaweza kutumika katika tasnia ya kilimo, nishati, ujenzi, machimbo, ufamasia, magari, meli, majumbani, ofisini na mazingira.

(x) Mmea wa Mkonge unaweza kuishi kwa kipindi cha miaka 10 mpaka 25, hivyo kumhakikishia mkulima kipato cha uhakika na kwa muda mrefu.

(xi) Mkonge ni zao pekee ambalo Tanzania iliweza kuongoza kwa uzalishaji na ubora ulimwenguni, rekodi ambayo hadi sasa haijavunjwa na zao lolote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuzalisha tani 200,000 za Singa ifikapo 2016. Naliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuitaka Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Bodi ya Mkonge nchini kuweka lengo la kuzalisha Singa tani 200,000 ifikapo mwaka 2016. Lengo hili litaturejeshwa kuwa nchi ya Kwanza Duniani kwa kuzalisha singa, kuingiza mapato ya fedha za Kigeni kwa kiwango cha Dola za Marekani milioni 300 na kutengeneza ajira 500,000 za moja kwa moja katika tasnia nzima ya mkonge. Kwa nini tuzalishe kiasi hiki cha singa kwa mwaka ifikapo 2016?

Mheshimiwa Spika, kuna sababu zifuatazo za kuweka lengo hili:-

(i) Upatikanaji wa Soko la Uhakika. Kwa sasa mahitaji ya singa za Mkonge yamefikia tani 20,000,000 kwa mwaka. Kama nchi, Tanzania tuna uwezo mkubwa wa kuzalisha (*comparative and competitive advantage in sisal globally*) mkonge na bidhaa zitokanazo na mkonge. Bidhaa zifuatazo zinaweza kuzalishwa hapa nchini; Rojo ya karatasi (*Pulp and Paper*), Composites inayoweza kutumika katika tasnia ya magari, fanicha na bidhaa nyinginezo. Vile vile tunaweza kuzalisha kamba za aina mbalimbali, bidhaa za kufuma (*Woven Products*) kama kapeti, kitambaa msasa na mabegi. Bidhaa za Mkonge zinaweza kutumika katika ujenzi wa barabara, kuzuia mmomonyoko wa udongo katika barabara za reli kwa kutumia *Geo-textiles*.

Aidha, tunaweza kuzalisha umeme mkonge kwa kutumia mabaki ya mkonge teknolojia ambayo yanaweza kutumiwa na wazalishaji wote wa mkonge kuanzia mkulima mdogo hadi mkulima mkubwa. Kwa kutokana na kutumia mabaki kuzalisha umeme tunaweza kuzalisha mbolea yenye virutubisho muhimu vinavyohitajiwa na mmea. Pia tafiti zimeshaonesha kuwa mabaki ya mkonge yanaweza kutumika kama chakula cha mifugo na zaidi mkonge unaweza kutoa kemikali za viwandani.

(ii) Upatikanaji wa ardhi inayofaa kwa kilimo cha mkonge. Ardhi inayofaa kwa kilimo hapa nchini inakadiriwa kufikia jumla ya hekta 44,000,000. Kwa sasa ardhi iliyo chini ya mashamba ya mkonge ni jumla ya hekta 174,552 ambayo ni takriban asilimia 0.4 ya ardhi yote inayofaa kwa kilimo. Ili kufikia lengo hili jumla ya hekta 200,000 zitahitajika. Kwa utekelezaji wa azma hii maeneo ambayo ni makame yanaweza kutumika kuzalisha mkonge ambao hauhitaji umwagiliaji au maeneo ambayo hakuna zao kuu la biashara linaloweza kuwaingizia wananchi kipato cha uhakika. Vilevile hata maeneo yenye rutuba ya kutosha bado zao la mkonge linaweza kulimwa kwa kuchanganywa na mazao mengine.

(iii) Rasilimali watu inayohitajika. Tanzania kwa sasa ina jumla ya watu wanaokadiriwa kufikia milioni 42. Ili kuweza kufikia lengo hili, tunahitaji takriban watu 500,000 walioko maeneo ya vijijini na mijini watakaoshiriki katika hatua mbalimbali za uzalishaji wa mkonge.

(iv) Mheshimiwa Spika, matokeo ya tafiti zilizokwishafanywa. Zaidi ya dola za Marekani 9,000,000 zimekwishatumika katika kufanya tafiti mbalimbali za kufanya tasnia hii ya mkonge iweze kutufikisha huko ambako tunataka kufika.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya uzalishaji wa tani 200,000 za Singa. Tangu zao la Mkonge liletwe hapa nchini, limekuwa likizalishwa na wakulima wakubwa wanaomiliki mashamba makubwa ya mkonge yaliyoko katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Kilimanjaro, Arusha, Pwani na Lindi. Ili kuongeza wigo wa umiliki wa zao la mkonge, ni vema sasa kuwashirikisha wakulima wadogo katika uzalishaji wa mkonge kazi ambayo kimsingi ilishaanzwa na sasa tunahitaji kuitekeleza kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama nchi tunaweza sasa kugeuza uzalishaji wa mkonge uwe wa wakulima wadogo kama ilivyo nchi za Brazili na Uchina. Tunahitaji kaya 18,334 tu nchi nzima zenye uwezo wa kumiliki hekta sita za mkonge au jumla ya kaya 36, 667 tu zitakazokuwa na uwezo wa kumiliki jumla ya hekta tatu kwa kila kaya. Kwa kuongeza jumla ya hekta 110,000 tu zitakazomilikiwa na wakulima wadogo katika ngazi ya kaya, tutaweza kuzalisha jumla ya tani 110,000 za singa mara baada ya miaka mitatu tangu kuanza kwa utekelezaji. Kiasi kingine cha singa kinategemewa kuzalishwa na wenye mashamba makubwa na hivyo kurudia uongozi wetu katika uzalishaji kwa kufikia tani 150,000; kwani kwa sasa nchi inayoongoza kwa kuzalisha mkonge ni Brazil inayozalisha jumla ya tani 110,000 kupitia mfumo wa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na mkonge. Kwa uzalishaji huu wa tani laki mbili (200,000) za singa, jumla ya tani 100,000 za singa zinaweza kutumika kuzalisha kamba za aina mbalimbali, tani 70,000 zinaweza kutumika kuzalisha bidhaa za kufuma na jumla ya tani 30,000 zinaweza kutumika kuzalisha bidhaa nyinginezo zitakazotumika katika shughuli za ujenzi na bidhaa za mikono.

Mheshimiwa Spika, mabaki ya mkonge kuzalisha umeme 1000 MW. Sambamba na uzalishaji wa mkonge, mabaki yatumika kuzalisha umeme, mkonge kwa ajili ya matumizi ya viwanda vya mkonge na majumbani, pia mbolea itakayotumika kurutubishia udongo, chakula cha mifugo na kemikali za viwandani. Tafiti zinaonesha kwamba shamba la mkonge la hekta 3500 linaweza kuzalisha umeme wa 100 MW. Wakulima wadogo 100 wenye hekta 3.5 kila mmoja wanaweza kuzalisha umeme 10 MW kwa mwaka, kwa bei za sasa kujipatia pato la shilingi 100,000,000 kila mmoja kwa kuuza umeme huo katika gridi ya Taifa. Taifa likiamua kuwekeza hekta 35,000 kati ya hekta 200,000 zitakazolengwa kwa ajili ya uzalishaji umeme peke yake, jumla 1000 MW zitazalishwa. Sehemu yake itatumika katika Viwanda vya Mkonge na sehemu kubwa kuingizwa katika gridi ya Taifa na hivyo kuongeza mapato kwa wakulima wa mkonge na kusaidia kuondoa tatizo la umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya ajira 500,000 zinategemewa kutengenezwa Vijijini na Mijini kwa kipindi hicho ambacho nchi itakuwa inazalisha tani 200,000 za singa kila mwaka na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa sana juhudi za kuondoa umaskini nchini. Ajira nyingi zaidi zitategenezwa katika viwanda vya bidhaa za mkonge na pia watoa huduma katika tasnia ya mkonge. Sekta ya Nishati itapanuka na kuzalisha ajira nyingine na vile vile sekta ya huduma itakua kwani sasa watu watakuwa na fedha za kutumia. Ajira zitakuza uchumi na kupunguza umaskini kwa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, tasnia ya mkonge kuingiza dola 300,000,000 kwa mwaka. Tani ya Mkonge katika soko la dunia imefikia dola 1500 na kutokana na mahitaji zaidi ya bidhaa za mkonge, bei inazidi kupanda. Kwa bei ilivyo sasa uzalishaji huu utaliingizia Taifa fedha za kigeni zitakazotoka na mauzo ya mkonge nje ya nchi jumla ya dola za Marekani 300,000,000 (*Export earnings*). Hii itasaidia nchi kupunguza uhasi (*negativity*) katika urari wa mauzo nje na kusaidia katika kudhibiti kuporomoka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine kwa Taifa. Uzalishaji huu utachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza viwanda katika tasnia ya mkonge, kipato endelevu na kupunguza umaskini kwa Watanzania walio wengi, kuongeza wakulima wakibiashara na wajasiriamali maeneo ya vijijini, vilevile uzalishaji huu utaongeza pato la Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007:-

KWA KUWA Tanzania imekuwa katika mipango mbalimbali ya kuongeza mauzo ya bidhaa nje na kuongeza ajira kwa raia wake na kwamba mazao ya kilimo yana mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi na hivyo kuondoa umaskini kwa Watanzania;

NA KWA KUWA zao la mkonge limeonekana ni zao linaloweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza mauzo nje ya nchi, kuongeza ajira na kuondoa umaskini; ukizingatia kwamba Tanzania imewahi kuwa mzalishaji mkubwa wa mkonge duniani na kwamba Tanzania imedhamiria kurejea katika hali hiyo;

NA KWA KUWA faida za zao la mkonge ni nyingi na zitakazosaidia kukuza uchumi wa nchi yetu na kwamba Tanzania imedhamiria kuboresha maisha ya wananchi wake;

NA KWA KUWA Serikali ya Tanzania imetangaza Kilimo kuwa ni kipaumbele kwa kupitia kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, naliomba Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Sita wa Bunge la Kumi liazimie yafuatayo:-

(1) Kwamba Mwaka 2012 utakuwa mwaka wa kupanda mkonge na hivyo Serikali kupitia Taasisi zake ijiandae inavyopaswa kutekeleza azma hii kwa kuhamasisha wakulima wadogo kupata ardhi ya kulima mkonge. Kampeni ya kupanda mkonge ihusishe wadau mbalimbali;

(2) Kwamba Serikali itaweka miundombinu ya kifedha kuwezesha kufikiwa kwa lengo la kupanda hekta 200,000 za Mkonge na hivyo kusaidia wakulima wadogo na wakubwa kupata mikopo nafuu kutoka katika Taasisi za Kifedha;

(3) Kwamba Sheria ya Mkonge ya mwaka 1997 ipitiwe upya kwa lengo la kuipa nguvu Bodi ya Mkonge katika kusimamia tasnia nzima ya zao la mkonge (*upstream, midstream and downstream*). Vile vile kuweka masharti ya matumizi ya bidhaa za mkonge hapa nchini;

(4) Kwamba Serikali ichukue hatua madhubuti kulinda bidhaa za mkonge dhidi ya ushindani usio halali;

(5) Serikali ichukue hatua ya kuwanyang'anya wawekezaji wote walioshindwa kuendeleza mashamba na kuyapangia matumizi mengine ikiwemo kuyagawa kwa wananchi ambao watayaendeleza;

(6) Kwamba Serikali ipige marufuku kuuza nje ya nchi bidhaa ghafi zinazozalishwa hapa nchini; na

(7) Kwamba ufanyike utafiti na mpangilio utakaobainisha ni ardhi ipi ya mashamba ya mkonge yaendeleo kutumika kwa zao la mkonge na ipi itumike kwa mazao mengine na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono.

MWONGOZO WA SPIKA

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge naomba ukae chini kwanza. Kwa mujibu wa Kanuni ya 58(1) ambayo inasema kwamba: "Endapo Mbunge anapenda kupendekeza mabadiliko yafanywe katika hoja kwa kufuata masharti ya Kanuni hizi, anaweza kutoa hoja yake ya kufanya mabadiliko wakati wowote baada ya hoja anayotaka kuibadili kutolewa, lakini kabla ya Bunge halijahojiwa lifanye uamuzi. Sasa hapa nimepata hoja ya mabadiliko kutoka kwa Mheshimiwa Nassir.

MHE. YUSUPH A. NASSIR: Mheshimiwa Spika nakushukuru. Naleta hoja kwa mujibu wa Kanuni kama ambavyo umetuelekeza, sisi ndiyo wadau wa mkonge.

Kwa kuwa, zao la Mkonge ni moja ya mazao makubwa kama ilivyothibitika, hoja ya mtoa hoja imejikita katika maeneo makubwa mawili. Moja ni kuantangaza mwaka 2012 kuwa mwaka wa mkonge na hoja nyingine imejikita katika kuipa mamlaka makubwa Bodi ya Mkongе. Kwa sababu amekiri katika hoja yake kwamba mkongе unahitaji maandalizi makubwa, kwa hiyo, kuwеka mwaka 2012 kuwa ni mwaka wa mkongе.

SPIKA: Hoja yako unaweza kuisoma, unaruhusiwa siyo unajadili.

MHE. YUSUPH A. NASSIR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniongoza. Kwa mujibu wa Kanuni ya 58(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kutoa hoja ya kubadilisha hoja binafsi kuhusu hali ya zao la mkongе nchini na Bunge kuazimia kwamba mwaka 2012 uwe mwaka wa kupanda mkongе iliyotolewa na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Zitto inalenga katika masuala makuu mawili, mwaka wa Mkongе na kutoa mamlaka makubwa kwa Bodi ya kusimamia Zao la Mkongе. Kutangaza mwaka wa Mkongе kunahitaji maandalizi na si suala la kukurupuka leo na kesho.

Melezo ya mtoa hoja yamelenga bayana kuwa, kabla ya kupanda Mkongе ni lazima pawepo na uwekezaji mkubwa mwanzoni. Hata hivyo uwekezaji huo hauwezi kutekelezwa kwa kuwa sekta hii ina matatizo mengi. Suala la ardhi kwa wakulima wadogo wadogo bado halijapatiwa ufumbuzi kwa kuwa kuna mfumo mbaya wa Nyarubanja unaoendelea hivi sasa, Wawekezaji waliopo wamedhihirisha kushindwa kuendeleza zao hilo na Mheshimiwa Zitto amelithibitishia Bunge. Sehemu kubwa ya mashamba ya Mkongе hasa pale maeneo ya Korogwe yamekuwa ni mapori na hayajaendelezwa kwa kipindi kirefu sasa.

Mheshimiwa Spika, ni katika Bunge lako Tukufu katika kikao hiki kinachoendelea mnamo tarehe 3 Februari, Serikali ilitoa tamko hapa kupitia Waziri wa Kilimo kwamba wanaunda Tume mahsusi itakayoshughulikia suala hili la mkongе. Sasa kujadili hoja ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto sijui mamlaka ya Kauli ya Serikali tunayaweka wapi hasa katika uundwaji wa Tume.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali ilitokana na swali Na. 44 lililoulizwa na Mbunge wa Korogwe Vijijini, Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani akitaka kujua mustakabali wa mashamba ya mkongе na tukijikita katika suala zima la maslahi ya wafanyakazi na wananchi waliopo maeneo ya katikati na maeneo ya pembezoni, ambapo sasa miji ile imekua.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la kutoa uwezo mkubwa kwa Bodi ya Mkongе yenye matatizo mengi. Bodi imeshindwa kupigania mafao ya waliokuwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Mkongе kwa takriban kipindi cha miongo miwili sasa. Bodi imeshindwa kusimamia mgao sawia wa ardhi kwa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali ya mwaka jana ilijibu swali langu la tarehe 28/7, iko kwenye *Hansard* ilisema wakulima wadogo wadogo wanaweza kupewa kati ya hekta tano mpaka 200, mgao ule haukufuata malipo yale. Kuipa nguvu Bodi ni kuendeleza upungufu uliojitokeza hasa pale hati za mashamba ya Serikali zilipotolewa kwa kampuni binafsi na kwenda kukopa fedha za wafanyakazi kwenye mifuko. (Makofi)

Nasimama kidete kusema kwamba Bodi isipewa nguvu iliyoombwa na Mtoa Hoja. Kadhalika kukua kwa vijiji na vitongoji kumeanza kutokea mgogoro wa mipaka kati ya vijiji vinavyohusika pamoja na mamlaka na wawekezaji waliopewa baadhi ya mashamba. Sasa basi kutokana na sababu hizo, naomba kuwasilisha hoja yangu ya kubadili hoja binafsi ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto kuhusu hali ya zao la mkongе nchini na Bunge kusema au kuazimia kwamba mwaka 2012 uwe mwaka wa kupanda mkongе kama ifuatavyo:-

KWA KUWA zao la mkongе ni moja ya mazao makubwa ya biashara nchini ambapo awali uzalishaji huo ulikuwa unafanywa na Serikali.

NA KWA KUWA uzalishaji wa zao hili ulitolewa chini ya Serikali na kuhamishiwa sekta binafsi.

NA KWA KUWA baada ya sekta binafsi kuanza kuzalisha zao hili kumetokea matatizo na changamoto mbalimbali kama vile mfumo wa umiliki, kwa wakulima wadogo mpaka leo hatujawapa hati za mashamba ili waweze kukopa na kujiongeza tija na kadhalika haujapatiwa ufumbuzi. Wawekezaji wa zao la mkonge wamedhihirisha kushindwa na kuendeleza zao hilo ambapo sehemu kubwa ya mashamba hayo bado yanaendelea kuwa mapori,

NA KWA KUWA Bodi ya Mkonge ambayo imepewa jukumu la kusimamia na kuendeleza zao la mkonge imeonesha kuwa na uwezo mdogo wa kutekeleza majukumu yake na kushindwa kama nilivyosema hapo awali kusimamia mafao ya waliokuwa wafanyakazi wa mamlaka ya mkonge pamoja na changamoto nyingine.

NA KWA KUWA Serikali kupitia swali namba 44 liliulizwa kwenye Bunge lako hili Tukufu na kauli ile ya Waziri wa Kilimo ya kwamba wataunda Tume. Basi ni vema niliombe Bunge lako Tukufu lifanye mabadiliko katika kipengele kile cha hoja ya mtoa hoja kutoka namba moja mpaka saba na hatimaye basi tusiikubali hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Kabwe Zitto mpaka wakati muafaka utakapofika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. HAMISI A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Kunakuwa na Mwongozo wakati mtu anafanya kazi yake, tumalize moja halafu tunaingia Mwongozo. Ukisoma ile kanuni ya Mwongozo inasema watu wakikaa kimya siyo wengine wamesimama, wewe unaomba Mwongozo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu linaongozwa na Kanuni. Kwanza, nasikitika sana kuona Mbunge kutoka Tanga anapinga hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe.

SPIKA: Hebu uliza unachotaka kuuliza kusikitika hakupo hapa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ukija moja kwa moja kwenye kanuni ya 57 inaelezea utaratibu mzima wa kubadilisha hoja, kitu ambacho Mheshimiwa Nassir alikuwa anakiwasilisha hapa. Sasa naomba ninukuu vifungu vya Kanuni ya 57 vinasema: "(1) Hoja ikishatolewa ili iamuliwe inaweza kubadilishwa kwa, kuna vigezo hapa:-

- (a) Kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine;
- (b) Kuondoa maneno fulani bila kuongeza maneno mengine; au
- (c) Kuingiza au kuongeza maneno mapya.

Kwa hiyo, badiliko lolote halitaruhusiwa kama kwa maoni ya Spika, linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja anayoitoa Mheshimiwa Nassir inapingana kwa asilimia mia moja na hoja aliyotoa Mheshimiwa Kabwe Zitto. Kwa hiyo, kama hoja yake ni kwamba mwaka 2012 ni mapema anachoweza ni kuomba mabadiliko yafanywe itoke mwaka 2012 iende 2013 ili Serikali ijiandae. Kwa hiyo, kwa kuleta hoja yake mpya amekinzana kabisa na matakwa ya Kanuni. Kwa hiyo, naomba tusimamie kanuni zetu ili hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe itendewe haki kwa matakwa ya kanuni. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Hii kanuni ya 57 kama ulivyosema inakusudia kufanya mabadiliko, huyu anakusudia kwamba hii hoja ya mwenzake iondolewe. Kwa hiyo, kuna mambo mawili hapa na sababu za kusema iondolewe amezitaja hapa kwamba kulikuwa na ahadi ya Serikali kwamba, itaunda Tume kuchunguza

industry hii yenyewe. Sasa nitawaita Serikali ili waseme ile haja iko wapi. Serikali mtoe maelezo kwamba hilo liko wapi. (Makofi)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maelezo ya Serikali kuhusu hoja ambayo imewasilishwa na hatua iliyochukuliwa na Mheshimiwa Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini katika kuirekebisha hoja hiyo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Februari, 2012 katika Kikao hiki cha Bunge, Mheshimiwa Ngonyani, Mbunge wa Korogwe, alileta swali ambalo lilitaka Serikali itatue changamoto nyingi ambazo zinakabili tasnia ya mkongwe katika Wilaya ya Korogwe na Tanzania kwa ujumla. Aidha, swali hilo lilitaka Serikali itatue matatizo ya mashamba mengi ambayo yameachwa, hayatumiki na kueleza ni hatua gani ambayo imefikiwa katika kufufua na kuendeleza viwanda ambavyo vilibinafsishwa.

Serikali katika kujibu swali lile ilikubali kuunda kikosi kazi ambacho kitakwenda kutembelea mashamba yote ya Mkongwe ambayo yalibinafsishwa, yale ambayo yanaendelezwa na yale ambayo hayajaendelezwa. Katika yale yanayoendelezwa iweze kuleta ni hatua gani imefikiwa katika kuendeleza mashamba katika kufufua viwanda vilivyopo na ni hatua gani imechukuliwa katika kuwahusisha wakulima wadogo. Aidha, Tume hiyo italeta taarifa kuhusu mashamba yale ambayo yameachwa na kuleta mapendekezo ya namna na hatua gani zichukuliwe ili kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nimepokea na kusoma kwa makini hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe na wale ambao mmesoma hii mtaona kwamba hoja hii imetokana na Mpango Mkakati wa Miaka Kumi wa Maendeleo ya Zao la Mkongwe ambayo imepitishwa na wadau wa Mkongwe tarehe 6 Aprili, 2011. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la hoja hii ni kuupa nguvu ya Bunge mpango mkakati uliopo na kwa kuwa Serikali imekubali na imeshaanza mchakato wa kuunda kikosi kazi hiki, kiende kufanya kazi na kuleta majibu ambayo yatatuzesha kutekeleza mpango mkakati huu kwa urahisi zaidi, naliomba Bunge lako Tukufu litupe muda ili kikosi kazi hiki kifanye kazi halafu tutaleta majibu na mipango ambayo Serikali inadhani inatekelezeka ili kufufua vizuri zao la mkongwe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

SPIKA: Sasa nina hoja nyingi, sasa niachieni nianze kufanya kazi yangu, wote mkae chini. Hoja aliyotoa Mheshimiwa Halima ni ya kufanya mabadiliko ndani ya Hoja, Hoja aliyotoa Mheshimiwa Nassir ni ya kuondoa hoja. Maelezo aliyotoa Waziri ni kwamba, huu mpango ukiletwa leo tarehe 12 utekeleze mazingira yale siyo sahihi. Kwa hiyo, Kamati aliyounda kuifanyia hiyo kazi, iacheni ifanye kazi kusudi hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe iweze kupata mazingira mazuri.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliafiki Kuondolewa kwa Hoja Binafsi Kuhusu Hali ya Zao la Mkongwe Nchini na kuazimia kwamba mwaka 2012 uwe mwaka wa kupanda Mkongwe)

SPIKA: Hoja ya Kabwe Zitto ni nzuri lakini kwa mazingira haya yaliyo na matatizo tunafikiri ije baadaye. Tunaendelea.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Tutaongozana mpaka mwisho, naomba nimalize kazi yangu kwanza.

HOJA BINAFSI

Hoja Binafsi ya Mhe. January Makamba Kuhusu Sheria ya Udhibiti wa Shughuli za Upangaji

Nyumba za Makazi

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na heshima ya kuwasilisha hoja hii katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ina madhumuni ya kuliomba Bunge lako Tukufu liazimie, kwa kauli moja, kuitaka Serikali, kwa haraka inavyowezekana kuleta Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Upangaji wa Nyumba za Makazi (*Rental Housing Act*); Sheria:-

- (1) Itakayoweka utaratibu na udhibiti wa sekta ya upangaji wa nyumba nchini kwa ujumla;
- (2) Itakayowezesha kuanzishwa kwa Wakala wa Udhibiti kwa Mamlaka ya udhibiti wa Sekta ya Nyumba – *Real Estate Regulatory Authority (RERA)*;
- (3) Itakayoinisha wazi haki na wajibu wa wapangaji na wenye nyumba;
- (4) Itakayoweka utaratibu wa haraka na rahisi zaidi kwa wapangaji na wenye nyumba kupata haki zao;
- (5) Itakayodhibiti na kuweka adhabu kwa vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wapangaji;
- (6) Itakayoweka utaratibu wa ukaguzi wa viwango na hali za makazi ya kupanga;
- (7) Itakayozuia na kuweka adhabu kwa utaratibu wa kutoza kodi ya nyumba kwa miezi sita au mwaka mzima; (*Makofi*)
- (8) Itakayodhibiti wenye nyumba kuwalazimisha wapangaji kulipa kodi ya nyumba kwa fedha za kigeni, hasa dola za Kimarekani; (*Makofi*)
- (9) Itakayodhibiti upandishaji holela wa kodi za nyumba; (*Makofi*)
- (10) Itakayowezesha mikataba ya upangaji wa nyumba kusajiliwa; (*Makofi*)
- (11) Itakayoweka utaratibu wa kuwatambua na kuwasajili madalali wa nyumba ili kudhibiti vitendo vyao; (*Makofi*)
- (12) Itakayoiwezesha Serikali kupata mapato kutokana na biashara ya upangaji nyumba kwa kuwalazimisha wenye nyumba kujisajili kwenye Mamlaka husika na kutoa risiti kwa wapangaji; na
- (13) Itakayoweka taratibu nyingine mbalimbali zitakazolinda haki za wapangaji na wenye nyumba na zitakazowezesha sekta ya makazi kukua na kushamiri na kupunguza tatizo la makazi nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, msingi wa hoja hii ni malalamiko mengi ambayo mimi na naamini ninyi viongozi wenzangu mmekuwa mkiyapata kutoka kwa wananchi wengi hasa waishio mijini kutokana na adha wanazopata katika kutafuta nyumba za kupanga na kuishi kwenye nyumba za kupanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nitoe mifano kadhaa ya baadhi ya watu niliokutana nao na walionielezea masaibu yao. (*Makofi*)

Nilikutana na binti mmoja anaitwa Dora, ni mwandishi wa habari ana miaka 30, anafanyia kazi Gazeti moja la Serikali pale Dar es Salaam. Alimaliza Chuo Kikuu hivi karibuni akabahatika kupata kazi ya Uandishi wa Habari na kwa kuwa wazazi wake hawaishi Dar es Salaam, hana ndugu aliamua sasa atafute chumba aanze maisha mwenyewe. Kwa hiyo, alihangaika miezi nane bila kupata pa kukaa kwa sababu kila alipokwenda, aliambiwa leta kodi ya miezi sita na sehemu nyingine anaambiwa leta kodi ya mwaka mzima. Sasa huyu mtu amepata tu barua ya kazi, *offer* hajaanza kupata mshahara, halafu akitafuta makazi ili aanze maisha anaombwa kodi ya pango ambayo hana na hana kipato na hana namna ya kuweza kuipata.

Sasa akaamua kutafuta wenzake ili aweze kuishi nao ili waweze wachange fedha waweze kupunguza yale makali. Kila sehemu walipokuwa wanakwenda sehemu nyingi, wenye nyumba walikuwa wanawaambia sisi hatupangishi mtu ambaye hajaoa wala hajaolewa. Kwa hiyo, akawa anahangaika na kimsingi kilichotokea siyo haki. Huku nyuma hakuwa na mahali pa kwenda kutafuta haki yake.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ukiwasilisha hoja unasoma kama ulivyoandika siyo habari zingine tena.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, huko nyuma, ilikuwepo Sheria ya Udhhibiti wa Pango ya Mwaka 1984 (*Rental Restriction Act of 1984*), ambayo ingeweza kumlinda Dora asitozwe kodi ya mwaka. Hata hivyo, Sheria hiyo ilifutwa mwaka 2005 na baadhi ya vipengele kuingizwa kwenye marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Mahakama ya Ardhi ya Mwaka 2005. Hata hivyo, vipengele madhubuti vya kumlinda mpangaji vilitupwa kabisa katika mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, pia yupo Bwana Saidi Bakari Shemweta, mzaliwa wa Jimbo langu la Bumbuli ambaye anakaa Mbagala Dar es Salaam. Ana familia ya watu sita; mke na watoto watatu na ndugu wengine wawili. Anafanya biashara ndogondogo pale Dar es Salaam na kipato chake ni cha siku kwa siku. Alikuwa na mkataba wa pango wa mwaka mzima.

Lakini mkataba wenyewe ulikuwa wa kuandikishiana kwenye kipande cha karatasi. Mkataba huo ulitengenezwa na mwenye nyumba na ulisheheni zaidi maslahi ya mwenye nyumba kuliko yeye. Alikuwa analipa kodi bila kupewa risiti na wapangaji wenzake nao wanalipa kodi bila kupewa risiti. Lakini yeye kwenye biashara zake, ambazo zina kipato kidogo kuliko kipato cha mwenye nyumba, analipa kodi. Vile vile hali ya makazi anayoishi, kwa maana ya idadi ya watu kwenye hiyo kulinganisha na vyoo vilivyopo na kulinganisha na hali ya upatikanaji maji, ilikuwa hailingani na kiwango cha kodi anayolipa. Hata pale ambapo mwenye nyumba alipaswa kufanya matengenezo, hakuwa anafanya hivyo.

Pamoja na yote hayo, ghafla mwenye nyumba aliamua kupandisha kodi katikati ya mkataba kwa kuwa tu alipata mpangaji aliyekuwa tayari kulipa pango kubwa kuliko Bwana Shemweta. Bwana Shemweta alitafutiwa kosa tu kama mnavyojua mtu anakutafutia kosa labda umepika wali unaonukia zaidi, akapewa notisi ya ghafla.

Kwa kuwa hakuweza kupata nyumba ndani ya kipindi kifupi, kwa tatizo lilelile la kukosa kodi ya mwaka mzima, akalazimika kuondolewa kwa nguvu kwenye nyumba na vitu vyake kutolewa nje pamoja na watoto na ndugu zake, shemeji zake. Hapakuwa pa kwenda kudai haki yake. Hakujuu analindwa na Sheria gani na hakujuu pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, naamini masaibu kama haya ya Dora na Shemweta yapo mengi na ukisikia yanasikitisha zaidi. Sisi Wabunge tumekuja hapa Bungeni kama wawakilishi wa watu ili tutunge Sheria kwa manufaa ya walio wengi. Lakini tupo hapa tukitambua kwamba jamii yetu vile vile ina matabaka. Ina wanyonge na ina wenye mabavu. Ina watu wanaokunywa mvinyo wa dola 2,000 kwa chupa na ina watu ambao hawajui mchana watakula nini, lakini wote hawa wanahitaji makazi. Lakini kuna waliojaliwa kujenga nyumba zao, ambao makazi sio jambo linalowasumbua. Lakini kuna wengi zaidi ambao hawakujaliwa kujenga nyumba zao na makazi ndio shaka yao kubwa. Katika kutunga Sheria hapa Bungeni, lazima tuendeshwe na msingi wa kusaidia wanyonge, pamoja na kwamba tunalinda haki za raia wote bila kujali hali yao ya kipato.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005, Bunge lilifuta Sheria ya Udhhibiti wa Pango ya Mwaka 1984 (*Rental Restriction Act of 1984*) ambayo ilikuwa inatoa ulinzi kwa wanyonge ambao wengi ni wapangaji. Moja ya sababu ya kuifuta Sheria hii ilikuwa ni kwamba eti Sheria ya Kudhibiti bei ni sheria ya enzi za kijamaa na kwamba pango liachwe liwe kazi ya soko huria. Huu sio ukweli. Sheria hii ilitungwa mwaka 1962 ambapo nchi yetu ilikuwa bado haijaingia kwenye siasa ya ujamaa. Lakini zipo nchi nyingi za kibepari ambazo zina Sheria ya Kudhibiti Pango, (*Rental Restriction Act*) ikiwemo Kenya, ambapo chini ya Sheria yao namba 296, ni kosa kudai pango la zaidi ya miezi miwili na Uganda na wenyewe wana Sheria kama hiyo, Sheria namba 231.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika mageuzi ya uchumi wa nchi yetu ambayo tumekuwa tukiyafanya katika miaka ya 1990, tumeunda taasisi nyingi na tumetunga Sheria kadhaa zinazodhibiti bei za bidhaa mbalimbali, bei na utaratibu wa bidhaa na huduma. Mfano, *SUMATRA* inadhhibiti bei za usafiri; *EWURA*, bei ya nishati; *TCRA*, bei za kupiga simu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama tumeona ni sahihi kuweka udhibiti kwamba makampuni ya simu yasipandishe bei za kupiga simu holela, kwa nini tusiweke udhibiti kwenye hitaji muhimu la maisha ya mwanadamu, yaani makazi, kwamba mwenye nyumba asipandishe kodi holela, kwa kiwango chochote kwa wakati wowote anaotaka.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kukawa na wasiwasi kwamba tukiweka udhibiti wa shughuli za pango, biashara za upangishaji itaharibika na uwekezaji utazorota. Hiyo inawezekana tu kama hakuna udhibiti wa Serikali. Ndio maana napendekeza kwamba katika Sheria ambayo Serikali itaileta hapa Bungeni basi kuanzishwe Mamlaka ya Udhibiti wa Biashara ya Nyumba (*Real Estate Regulatory Authority – RERA*) ambayo itadhhibiti mienendo ya wadau wote katika sekta ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi ambazo zimefanya vizuri katika sekta ya makazi zina mamlaka hizi. Vilevile, tumeona kwamba, hata baada ya kuifuta Sheria ya *Rental Restriction Act* ya 1984, bado mahitaji ya nyumba yameongezeka na uwekezaji haujakidhi mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ninayopendekeza itungwe sio ya kudhibiti bei ya pango pekee yake, ni sheria ya kudhibiti mwenendo mzima wa biashara ya upangaji ili wadau wote na washiriki wote kwenye biashara hii, yaani wenye nyumba, wapangaji, madalali na Serikali, wapate haki zao za msingi na mashauri na migogoro ya nyumba ipate kushughulikiwa kwa haraka, kwa ukamilifu na kwa haki.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ni muhimu nikaweka wazi kwamba Sheria ninayopendekeza kutunzwa sio Sheria ya kuwakandamiza wenye nyumba. Ni Sheria itakayolinda maslahi ya wote, kwani ni dhahiri kabisa kwamba wapo wapangaji ambao nao hawatimizi wajibu wao na ambao ni wasumbufu katika kulipa pango na wazembe katika kutunza mali za wenye nyumba.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba liko tatizo la nyumba na makazi nchini. Takwimu zinaonesha kwamba kuna upungufu wa nyumba takriban milioni tatu na kwamba kila mwaka kunahitajika nyumba mpya 200,000. Kasi ya ujenzi wa nyumba haiendani na mahitaji haya licha ya uamuzi wetu wa kuweka uhuru mkubwa wa soko katika biashara hii. Lakini hatuwezi kukaa, kama viongozi, na kukubali kwamba kwa kuwa kuna upungufu wa nyumba na kwa kuwa soko la nyumba linawapa nguvu zaidi wenye nyumba, basi haki za wanyonge, ambao ni wapangaji, zisilindwe.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa ikaja hoja kwamba Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Mahakama ya Ardhi ya mwaka 2005, zinatoa kinga kwa wapangaji. Baada ya utafiti wangu na kwa msaada wa wataalam wa Sheria zinazohusiana na makazi, ukweli ni kwamba Sheria hizo hazitoshelezi. Kwa mfano, kwa Sheria za sasa, mwenye nyumba hana haja ya kwenda Mahakamani kupata haki yake ya kimkatiba. Anaweza kuuza kitu chochote cha mpangaji hata kama kina thamani kubwa kuliko pango analodai lakini mpangaji, ili kupata haki yake ya kimkatiba, lazima aende mahakamani ambapo kuna mlolongo mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hatuna haja kufanya utafiti wa kina kubaini tatizo kwenye shughuli za upangaji, matatizo kwenye sekta ya upangaji tunayoona kila siku na tunayajua na tunasimuliwa kwa msingi huo inahitajika Sheria mpya, Sheria mama mahsusi kabisa kwa masuala ya makazi ili Sheria hizi mbili Sheria ya Ardhi na Sheria ya Mahakama ya Ardhi zibaki katika masuala ya ardhi pekee ambayo nayo yana mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, naamini katika azma ya Serikali kuboresha makazi hapa nchini, naamini katika uongozi wa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Profesa Anna Tibajuka, ambaye anafanya kazi nzuri. Naamini kabisa tukitunga Sheria hii na ikasimamiwa vizuri tutakuwa tumewasaidia Watanzania zaidi ya milioni 14 wanaoathirika na udhibiti mdogo katika shughuli za upangaji. Naamini pia kwamba, katika mchakato wa kutunga sheria hii, wadau wote watashirikishwa kutoa mawazo na maoni yao ikiwa ni pamoja na Bunge kwa maana ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa hoja yenyewe napenda kuwashukuru viongozi wa Chama cha Wapangaji Tanzania walionisaidia na kunihimiza kuleta hoja hii. Nawashukuru pia waandishi wa habari walioandika habari na makala kuunga mkono kusudio la hoja hii. Nawashukuru marafiki zangu wote kwenye mitandao ya kijamii ya *twitter* na *facebook* kwa kunipa maoni na ushauri na kuunga mkono hoja hii. Nawashukuru wote, ikiwemo Waheshimiwa Wabunge ambao wamenipa moyo katika kuleta hoja hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa niwasilishe hoja yenyewe. Hoja hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 54(1):-

KWA KUWA, asilimia kubwa ya Watanzania, hasa waishio mijini, wanaishi kwenye nyumba za kupanga na karibu asilimia 40 ya kipato chao wanakitumia kwa ajili ya kulipia pango;

NA KWA KUWA, kumekuwa na udhibiti mdogo wa biashara ya upangaji na kupelekea kuongezeka kwa vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wapangaji, ikiwemo kudaiwa pango la miezi sita hadi mwaka mzima, tena kwa fedha za kigeni;

NA KWA KUWA, kumekuwa na tatizo la makazi mijini na hivyo kuwalazimisha wapangaji kukubali masharti ya upangaji yanayokwenda kinyume na haki na kwa kuwa vitendo hivi vimekuwa vinaendelea kwa muda mrefu bila udhibiti;

NA KWA KUWA, hakuna sheria mama inayodhibiti upangaji na inayolinda haki za mpangaji na kwa kuwa Sheria ya Ardhi ya 1999 na Sheria ya Mahakama ya Ardhi ya 2005 hazitoa udhibiti kamilifu wa sekta ya upangaji nyumba;

HIVYO BASI, Bunge liazimie kuitaka Serikali, kwa haraka inavyowezekana, ilete Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Shughuli za Upangaji wa Nyumba (*Rental Housing Act*) ambayo, pamoja na mambo mengine, itakayoweka utaratibu na udhibiti wa sekta ya upangaji wa nyumba ikiwemo kuweka haki na wajibu wa wapangaji na wenye nyumba, kuweka mazingira ya ukuaji wa sekta ya makazi na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Sekta ya Nyumba (*Real Estate Regulatory Authority*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliitolewa iamuliwe)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Waheshimiwa Wabunge kwanza kabisa naomba nimpongeze mtoa hoja Mheshimiwa January Makamba kwa sababu suala analolizungumzia ni suala la msingi na mambo ambayo ni kero ambazo si geni kwa Serikali tunazifahamu na katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM ambayo ni Chama Tawala chenye Serikali na ambayo kama Waziri wa Ardhi nachukua ile kama *terms of reference* za kazi yangu, sekta ya nyumba imeandikwa kabisa kwamba ni sekta maalum. Katika Ibara ya 60 ya Ilani hiyo ni sekta maalum na katika Kifungu cha (6) Serikali iko katika mchakato wa kutengeneza *Housing Policy*, kwa hiyo, ni jambo lililopingika kwamba sekta hii inapotoka kwenye utawala au *regime* ya *Rent Restriction Act* na kuingia katika mfumo wa sasa wa soko huria, ni sekta ambayo iko katika transition.

Kwa hiyo, ni wazi kabisa kwamba utungaji wa Sheria ambayo itasimamia mambo ya msingi ambayo Mheshimiwa Makamba ameyasema lazima na sharti kusudi iwe na tija ni lazima itanguliwe na sera.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nasema mambo yaliyosemwa ni ya msingi, Serikali inayafahamu na mimi mwenyewe nayatambua ila sasa sio suala ambalo unaweza ukakurupuka na Sheria kabla hujatafuta maoni ya wadau. Kwa mfano, ni kweli kwamba nyumba hazitoshi na ni kweli kwamba *Rent Restriction Act* ilikuwepo tuseme takriban miaka 45 kabla hajijafutwa, lakini hali halisi hasa kwa mtazamo wa uchumi, ile sheria ilipofutwa ilikuwa yenyewe haifanyi kazi. Kwa hiyo, huu utamaduni wa kulipa mwaka mmoja, miezi sita ambacho sio kitu kinachokidhi viwango vya Kimataifa ambayo na mimi natambua kwamba sio haki, lakini suala linakuja, unaliondoa jambo lile kwa Sheria au kwa kuwa na nyumba za kutosha.

Kwa hiyo, ndugu zangu, hapa kitu muhimu na ndiyo maana Serikali inajitayarisha na sera kusudi tupate mawazo ya wadau yaliyo mengi, maovu, kero ambazo zimeainishwa na Mheshimiwa January Makamba zifanyiwe kazi, lakini pia tupate hali halisi. Sekta ya nyumba ni sekta muhimu sana, nadhani ni *nursery rhyme* unasema *food, clothing and shelter*, vitu hivi ni vitu muhimu, ni *basic*. Lakini ukitaka sasa hivi kuwa na chombo cha kudhibiti bei za vyakula utafika wapi?

Sasa unapokuwa na chombo cha kudhibiti kwa mfano, bei ya pango lakini huna nyumba za kutosha kama nchi nyingi ambazo zina Sheria hizi, pia zinakuwa na mfumo wa *council housing* kwamba unazalisha nyumba. Kwa upande wa Serikali sasa hivi chombo chetu tulichonacho ni Shirika la Nyumba la Taifa. Nadhani Bunge hili Tukufu linafahamu yaliyolisibu Shirika la Nyumba la Taifa lilipoacha kufanya kazi kwa sababu mfumo uliokuwepo ulikuwa hauruhusu lile Shirika kwenda mbele.

Sasa hivi, Shirika lile halipewi hata shilingi moja ya ruzuku ya Serikali mbali na ule mtaji waliopewa kufanya shughuli zao, sasa ukiweka chombo cha kudhibiti pango katika soko huria, katika *private sector* tunajua kitakachotokea, tunaita ni *black market* kwa sababu kwa Kiswahili sijui wanasemaje, lakini kutakuwa na soko la chini chini, chini ya meza. Sasa hii tabia ya kuchangishana miezi sita, mwaka mmoja mimi mwenyewe nailaani, ila nataka kusema kwamba unaiondoaje? Uelewa wangu wa mambo ni kwamba Sheria inaweza ikashindwa kuiondoa kwa sababu Sheria itakuwa hapo kwenye *shelf* kama ilivyokuwepo kabla haijafutwa, lakini huku soko litakuwa linatawala vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa mantiki hiyo basi, naomba kwamba hoja hii ni ya msingi lakini Serikali inahitaji muda na kuwatendea wananchi haki, kumaliza sera ya nyumba, kusudi sasa tuangalie ni vyombo gani, ni Sheria gani, ni uhakiki gani tutauweka badala ya kusema kwamba tufanye jambo hili kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kutoa hoja kwamba jambo hili tupewe nafasi ya kulifanyia kazi kwa mujibu wa taratibu. *(Makofi)*

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliitolewa iamuliwe)

SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nimesikia hoja ya Serikali na ningependa Waheshimiwa Wabunge wachangie na watoe mawazo yao kama inawezekana. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hata kama nitawapeni nafasi nitawapa nafasi labda watu wawili tu. Mheshimiwa Mbowe na Mheshimiwa Ole- Sendeka basi.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hoja hii. Kwanza, nimshukuru mtoa hoja kwamba hoja ni ya msingi kwa kweli, ni hoja ya msingi ambayo inapigania haki kwa Watanzania wa kawaida hasa wale wa kipato cha chini. Lakini nisikitike kwamba Serikali inakiri leo ndani ya Bunge kwamba haina sera ya makazi *fifty year of independence*, Serikali inakiri mpaka leo inakusanya maoni yaani ina maana miaka hamsini hatuna sera ya makazi.

Mheshimiwa Spika, sasa hilo tuliache, ambalo ningetaka kushauri kwa kifupi sana na juzi kwenye semina ya uchumi nililizungumza hili *though* kwa kifupi, inaonekana bado Serikali haijaona makazi kama chanzo muhimu sana cha mapato na nilitoa mfano wa wenzetu wa Dubai. Dubai ni mojawapo ya maeneo ambayo yanajengeka kwa kasi sana duniani na Dubai pamoja na kwamba wana mafuta, lakini mafuta ya Dubai yanachangia asilimia sita ya GDP ya Dubai, lakini *housing*, makazi yanachangia GDP ya Dubai kwa zaidi ya asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, nchini sasa hivi kuna ujenzi mkubwa sana unaoendelea, lakini ujenzi hauko *regulated*, yaani ni ujenzi holela kwamba kuna makazi makubwa yanajengwa, kuna miradi mingi inafanywa kati ya Shirika la *National Housing* ambao nawapongeza sana kwa kazi kubwa ambayo

wanaifanya. Pia Mheshimiwa Waziri nakupongeza, lakini ni kwamba, wanajenga wao na wanajenga watu wengine binafsi makazi ambayo hayako *regulated* yaani hakuna utaratibu wowote. Sasa huwezi kujua ni watu wa mipango miji ama watu gani ambao wanadhibiti ujenzi ambao unaendelea katika Taifa kwa sasa na nina hakika Serikali inakosa mapato makubwa sana kwenye upande wa makazi haya.

Mheshimiwa Spika, wako watu wana majumba makubwa Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na maeneo mengine mbalimbali ambako unakuta wanaweza wakapangisha nyumba kwa dola elfu kumi kwa mwezi na unakuta mtu ana nyumba tano, ana nyumba kumi maana yake nini? Kama mtu ana nyumba kumi ana *income* ya *a hundred thousand dollars* kwa mwezi na halipi kodi. Kwa hiyo, Serikali inapoteza mapato makubwa sana kwa sababu hatuna *mechanism* ya ku-control hii, ambapo naomba kwa Serikali wafuate mpango wa Dubai, wajifunze, tuna sababu zote za kuanzisha *Real Estate Regulatory Authority* ambayo hiyo sera anayozungumza Mheshimiwa Waziri basi inakuwa ni sera ambayo inaweza ikatekelezeka *through a certain authority* katika Mamlaka ya Serikali na kwa kufanya hivyo tunaweza tukajikuta tunabuni vyanzo vikubwa sana vya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wote tuna ushahidi sasa hivi kwamba, tukiangalia majengo makubwa yanayojengwa, mengi yanajengwa na hii Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii, lakini ukiacha hiyo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii angalau ni Mashirika ya Umma, bado kuna watu binafsi wengi na wengine wakiwa ni wageni wanaokuja kujenga hapa. Wanapojenga hapa wanaingiza mitaji kutoka nchi za nje na wanauza hizi nyumba mapema kabisa kabla hata majengo haya hayajajengwa, lakini hakuna udhibiti wowote unaofanyika, hakuna Mamlaka yoyote inayodhibiti hali hii zaidi ya kusema labda ni watu wa Manispaa ambao wanatoa vibali vya ujenzi, lakini zaidi ya hapo hawana Mamlaka mengine yoyote yale ya kisheria ya kudhibiti ujenzi huu na Serikali haina mkakati wowote wa kawaida wa kisheria wa kupata mapato kutoka kwenye majengo haya.

Mheshimiwa Spika, leo ninapozungumza ni kwamba, *construction industry* inachangia over 8% ya GDP kwa Tanzania na vile vile *growth* yake kwa mwaka ni over 14%. Ni sekta muhimu mno, lakini ni sekta muhimu ambayo haina *control* wala haina mamlaka inayodhibiti. Kwa hiyo, niombe kwamba, Serikali au Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwamba, angalau basi Serikali imeona ilifanyie kazi suala la sera, naomba mli-speed up. Lakini katika kuli-speed up vilevile hebu fikiria Mheshimiwa Waziri umuhimu wa kuanzisha *Real Estate Regulatory Authority*, haya mambo yetu lazima tuya-control, tusiwe tunakurupuka yaani lazima tuweze kuona *trend* yetu ya uchumi, sasa hivi *Real Estate* ina msukumo mkubwa sana na kwa sababu *Real Estate* ina msukumo mkubwa, basi tuweke Mamlaka ya kudhibiti na katika kudhibiti, tuweze ku-tape revenue ya Serikali. Kuna mapato makubwa mno, sisemi kwamba hiyo *authority* ianze kudhibiti nyumba ya mtu binafsi, mtu ana nyumba yake moja au mbili *basically* unaweza kuzidhibiti, hapana, sizungumzii hilo.

Mheshimiwa Spika, natambua vilevile kwamba kuna *property tax* ya Serikali, lakini Mheshimiwa Waziri naweza ku-share leo *property tax* ya nchi hii hailipwi, kama kuna *property tax* inayolipwa nchi hii leo inalipwa *less than 5%*. Mimi natoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ambayo tumekuwa tuna *argue* sana, Halmashauri yetu inafanya nini katika ku-collect *property tax*. Nashangaa sana, nalizungumza hili hapa ili Mheshimiwa Waziri unisaidie kwamba leo Dar es Salaam hata *street names* hamna, maeneo kama mikocheni hata basi kuita barabara, basi iiteni barabara ya Freeman Mbowe, itasaidia.

Mheshimiwa Spika, tunajenga makazi makubwa, tunashindwa hata kutoa *street names*, *street names*! Leo Dar es Salaam, *fifty years after independence*, no, hii haiwezi kukubalika. Lakini vilevile unakuta watu wana majengo makubwa, tumejenga majengo, watu wanaishi kwenye majengo mazuri angalau Tanzania tukiweza ku-collect *property tax* tu na Serikali ikawa makini katika ku-collect *property tax* nina hakika Serikali itapata mapato makubwa sana ya kuweza kutoa *services* nyingine kama maji, barabara na *system* za sewerage katika maeneo ya wananchi ambayo wanaishi watu wenye uwezo wa kati na uwezo wa juu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ambacho nataka kukishauri, ili niwaachie wenzangu wachache pengine wapate fursa ya kuchangia, Mheshimiwa Waziri hebu angalia wenzetu wanafanya nini? Hiyo *policy* iende sambamba na kuanzisha hiyo *Authority*, kuna mapato makubwa sana kwenye *industry* hii, tusiyapoteze na uwekwe mkakati maalum *through* hii *Authority* ninayoi-propose wa ku-collect *Property Tax*. Nina hakika kuna *revenue* ya ajabu ambayo inatokana na majengo lakini *I can assure you*, nenda Mikocheni yote ile, nenda Mbezi Beach yote ile, nenda Dar es Salaam yote, angalia *properties*

zinazojengwa pale, Serikali haipati *revenue*, watu hawalipi *Property Tax* na Serikali inashindwa kujenga miundombinu katika maeneo haya kwa sababu hai-*collect Property Tax*. Sasa Serikali isiyocollect *Property Tax*, ni Serikali ya namna gani? Mwalimu Nyerere alisema Serikali isiyoweza ku-*collect tax*, ni Serikali ya hovyoy. Sasa mimi sijasema Serikali hii ni ya hovyoy lakini naiomba Serikali ikifikirie mapato yanayopotea kupitia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, nikushukuru sana kwa nafasi hii. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu!

SPIKA: Jamani mimi utaratibu usiyo kuwa utaratibu sipendi kweli, Mheshimiwa Ole-Sendeka anajadili sasa. Utaratibu umetokea wapi? Unampiga utaratibu Mbowe kwa sababu amezungumza, maana ndiye aliyekuwa anaongea. Mheshimiwa Ole-Sendeka!

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu ya Mheshimiwa January Makamba, Mbunge wa Bumbuli, ambayo kimsingi na mimi naungana na rafiki yangu Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kwamba ni ya msingi na nataka nimpongeze kwa kweli kwa hoja hii muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Profesa Anna Tibaijuka, kwa majibu yake ya wazi. Yeye ni muwazi, ni mkweli na pale ambapo pana upungufu, huwa ni mfano wa kukiri upungufu. Mimi namwomba aendelee kwa sababu mwongozo wa CCM wa mwaka 1981 unasema kujikosoa na kukosolewa ni silaha ya mapinduzi. Ukienda mbele inasema kukiri upungufu si dalili ya kushindwa bali ni ishara ya kujiimarisha. Nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba suala la makazi ni jambo muhimu sana na kama tunavyojua kwamba kwa mujibu wa Katiba, lengo la Serikali yetu ni ustawi wa watu wake, ustawi wa watu ni pamoja na suala zima la kuwa na makazi mazuri na ya uhakika. Kwa hiyo, nataka kusema Mheshimiwa Januari Makamba ametusaidia sana kuleta hoja hii ya msingi ambayo kwa kweli mimi naiunga mkono, ukizingatia kwamba tunataka tuwapatie watu wetu maeneo mazuri, makazi mazuri lakini zaidi tukilenga wanyonge ambao hawana uwezo wa kujenga nyumba na ambao pengine wangehitaji kupangisha nyumba kwa gharama inayolingana na uwezo wa kipato chao.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana pia na Mheshimiwa Waziri kwamba huwezi kuja na Sheria tu kabla hujawa na Sera. Sasa kwa kukiri kwamba tuna umri huo tulio nao leo bila kuwa na Sera lakini kujua kwamba lipo tatizo, ni hatua mojawapo ya kuelekea kwenye ufumbuzi wa tatizo. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kwa kasi ileile ya Mheshimiwa Anna Tibaijuka tunayojua na kwa uzoefu wake na mchango wake mkubwa katika suala zima la makazi siyo Tanzania tu bali duniani, atusaidie kulikusuma jambo hili la Sera na alieleze Bunge hili Tukufu kwamba ni lini Serikali itahakikisha kwamba Sera hiyo ya makazi inapatikana ili Sheria hizi ambazo ni pamoja na Sheria ambayo inapendekezwa na Mheshimiwa Januari Makamba iweze kupata nafasi kwa sababu huwezi kuwa na Sheria bila kuwa na Sera.

Mheshimiwa Spika, ukosefu huo wa Sera pengine kimsingi ndiyo uliotufanya tukajikanganya huko nyuma. Tumejichanganya kiasi kwamba tumefika mahali tukagawana nyumba za Serikali kama chakula cha njaa. Waliokuwa na nafasi wakagawiwa nyumba zile, pamoja na masharti ambayo walipewa ya kutokubadilisha nyumba hizo kwa kiwango ambacho sasa wamefanya na kutokuuza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa natoka *Sea Cliff*, nilikuwa nazijua nyumba za Serikali zilizokuwa pale, nyingine ni maghorofa makubwa sasa. Ukiangalia unaambiwa hii ilikuwa ya Waziri fulani, hii ilikuwa ya Katibu Mkuu Fulani, hii ilikuwa ya nani lakini tumeuza nyumba za Serikali tukasahau kwamba hatujafuta Utumishi wa Umma kitendo kilichosababisha kuwapeleka Watumishi wa Umma na viongozi wetu nje ya maeneo muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo *Oysterbay* itabaki kuwa ya wageni kwa sababu waliopewa wanauza. Huko mbele tunakokwenda, nakusudia kuja na hoja itakayotaka Bunge liazimie nyumba za Serikali zilizouzwa zinrudishwa na hatua zichukuliwe kwa wale waliovunja mkataba wenyewe. Huu ulikuwa ni uamuzi

ambao mimi ningeshirikishwa, ningesema tu kama kuna mahali Serikali ya Chama changu ilikosea, ni pamoja na kuuza nyumba za Serikali na kuwagawia watu kama chakula cha njaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi natofautiana sana na Mheshimiwa Magufuli alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Mbunge mmoja aliposema kwamba zile nyumba zilizogawanywa kwa watu ambao hawakustahili zimerudishwa. Nina ushahidi wa kutosha, hata zile zilizogawanywa kwa ndugu na marafiki wa viongozi, nyingine hazijrudishwa hadi leo na wakati nitakapoleta hoja, nitathibitisha maneno hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niondoke huko, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Msechu, *Chief* wa *National Housing*. Mheshimiwa Waziri kupitia kwako, nataka niungane na Wabunge wenzangu waliowahi kupata nafasi ya kuchangia na kulipongeza sana Shirika la Nyumba la Taifa kwa mpango ambao sasa hivi siyo wa maneno ni wa vitendo unaofanywa na Bwana Msechu wa Shirika la Nyumba la Taifa kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata makazi bora. Kipekee pia nataka nimpongezee pia Ndugu Ramadhani Dau wa NSSF kwa mpango mzuri sasa hivi ambapo wanahakikisha kwamba Watanzania wanapata nyumba na makazi mazuri na kwa bei ambayo ni afadhali kuliko iliyokuwepo kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, watu hao wawili ni mfano na napenda sana na taasisi zingine ziige mfano huo ili utaratibu huu wa kuwapatia Watanzania maeneo mazuri ya kuishi uweze kuwa katika uhalisia wake. Ni kwa maana hiyo, suala la *Property Tax* katika nyumba zilizokuwa zimejengwa na watu wenye uwezo katika maeneo muhimu, naungana na Mheshimiwa Freeman Mbowe kwamba kuna umuhimu sana wa kuhakikisha kwamba Serikali inakusanya mapato. Nimsaidie tu kumkukumbusha pia kwamba Mwalimu alisema Serikali *corrupt* haiwezi kukusanya kodi na kwamba Serikali *corrupt* inatumwa na watu wenye fedha. Imani yangu ni kwamba Serikali ya Chama changu haitumwi na watu wenye fedha, ni Serikali ambayo siyo *corrupt*, kwa hiyo itafanya hili kwa vitendo. Ni suala ambalo nina hakika wenzangu wamelisikia na kodi ya Serikali itakusanywa kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda niongezee kidogo kwa kuungana sana na Mheshimiwa Makamba lakini akubali kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwamba tumpe nafasi ya kuleta Sera kwanza halafu baadaye ndipo tujielekeze kwenye Sheria. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba katika kuleta Sera hii ni vizuri mambo ya msingi ambayo yameainishwa kama alivyokiri mwenyewe kwamba hii inaweza kuwa *Terms of Reference* kama sehemu ya kuchangia kuboresha sera hiyo, basi mapendekezo haya ambayo yametolewa na Mheshimiwa Mbunge yazingatiwe na wadau wengi zaidi waweze kushirikishwa na kwa kuwa ni matakwa ya Ilani ya CCM ya 1960 na wewe unatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imani yangu ni kwamba haya Waziri atayafanya haraka zaidi ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia sasa kuhitimisha mchango wangu mfupi kwa kuipongeza Serikali kwa jitihada walizofanya katika kutatua mgogoro wa Madaktari na kuwapongeza Madaktari kwa kurudi kazini kama ambavyo tumesikia leo. Kipekee sana, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano na Mheshimiwa Spika, kwa ku-*manage* zoezi hili ndani ya Nyumba hii ambapo ulikuwa unazingatia maslahi mapana ya nchi na hadhi ya Bunge letu na kuheshimu mgawanyo wa makazi ya Mhimili wa dola na mimi nasema nakushukuru sana kwa jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, zaidi nawapongeza Madaktari kwa uamuzi wao wa busara walioufanya wa kurudi kazini lakini bado wanaishauri Serikali ihakikishe kwamba isikomee kuwaondoa wale wawili, isonge mbele kuwaondoa watu wote ambao walihusika na kusababisha vifo vya Watanzania kutokea na hii ndiyo itaweza kurudisha imani ya wananchi kwa Serikali ya Chama chetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kusudio letu ni kwamba shughuli ziishe asubuhi hii ili jioni tufanye kazi ya kufunga mijadala yote tuliyoifanya hapa. Kwa hiyo, nitatumia Kanuni ya 28(2) kuongeza dakika 30 baada ya saa ya kuahirisha, saa saba, ili tuweze kutoa nafasi ya mchangiaji mmoja. Sasa nampa *gender*, nitamwita Mheshimiwa Bulaya halafu mtoa hoja tumalize. Mheshimiwa Bulaya!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia hoja hii binafsi ya kijana mwenzangu Mheshimiwa Januari Makamba.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Januari Makamba kwa kuzingatia na kutambua tatizo kubwa ambalo linawakabili Watanzania wa kipato cha chini na hasa vijana ambao wengi ndiyo wanakutana na changamoto za kodi wakati wa kuanza maisha.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa unapozungumza changamoto katika maisha mbali na mambo mengine yote au matatizo ya ajira, matatizo ya uchumi wa mtu mmoja lakini tatizo la kukosa sehemu ya kulala ni tatizo kubwa. Watu ambao wanapata tabu sana na wanaokabiliana na changamoto ya gharama ya kodi ni vijana, ambao wengi ndiyo wanaoanza maisha. Hata wale ambao wamemaliza elimu ya juu, wanaamua kwenda kutafuta, kupanga vyumba, mbali na kwamba wamekosa ajira, labda wameweza kupata sehemu ya kujishikiza, bado wanakutana na changamoto ya kodi kubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tatizo hili la kodi kubwa kwa wapangaji pia limeleta matabaka kwa sisi wenyewe Watanzania. Leo hii ukitaka kufikiria watu wenye kipato cha chini na kwa asilia kabisa unazungumzia wananchi wa Mbagala lakini wengi wameenda kuishi siyo kwa sababu wengine wanataka kukaa Mbagala kwa sababu ndiyo kuna unafuu wa kodi lakini wapo watu ambao wanaishi Mbagala, wanatamani kwenda kuishi *Oysterbay*, wanatamani kwenda kuishi Mbezi lakini kwa sababu tumetengeneza matabaka kwamba maeneo hayo wanakaa watu wenye hadhi fulani kutokana na bei ya kodi kuwa kubwa. Ndiyo maana watu wengine wanaamua kwenda kuishi huko na hili tusipoliangalia litaendelea kuwa tatizo kwa Watanzania wetu, wapo Watanzania ambao wanataka kukaa maeneo ya hadhi. Wapo Watanzania ambao na wenyewe wanataka kuishi katika nyumba bora. Ukienda Kigogo, ukienda Manzese siyo kwamba wengi wanataka kuishi huko, ukweli ni kwamba hawana uwezo wa kulipa kodi ambayo itawawezesha na wenyewe kwenda kuishi Masaki, *Oysterbay*, kwenda kuishi Mikocheni, kwenda kuishi *Mbezi Beach*.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuzungumzia suala la wenye nyumba kutoza kodi kwa dola na hili limekuwa ni tatizo kubwa. Naungana kabisa na mpango wa *National Housing*, hilo wala sina tatizo lakini pia na wenyewe wangeliangalia tatizo hili. *National Housing* wana mkakati nzuri wa kujenga nyumba nyingi lakini na wenyewe kuna maeneo wanatoza kwa dola kuanzia dola 700, dola 500 mpaka dola 1,000 na hii inaondoa dhana ya kuwasaidia Watanzania kuwa na makazi bora. Unapomjengea Mtanzania makazi bora pia inapendeza ukampunguzia mzigo wa kodi. Namwomba Mheshimiwa Waziri alichukulie kwa umuhimu mkubwa suala hili, sanasana maeneo ya Kariakoo, Posta, *National Housing* inatoza kodi kwa dola kitu ambacho unakuta Watanzania wengi wanashindwa kumudu na matokeo yake ambao wako mjini ni Wahindi, hilo wala siyo siri Waheshimiwa Wabunge. Sasa hili linaondoa dhana nzima na dhamira ya dhati ambayo walikuwa nayo ya kuhakikisha Watanzania wanapata makazi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aharakishe Sera ya Ardhi, haya mambo yanaenda pamoja. Ukiwa na mipango ya kuongeza nyumba kwa maana ya watu wawe na makazi bora na hapo hapo ukiwa na Sera, ukituletea Sera haraka itakayotusaidia kupata Sheria, naamini kabisa tunaweza tukafikia uamuzi wa kuondokana kabisa na tatizo hili ambalo linawakabili sana Watanzania na hasahasa vijana wenzangu ambao wanaanza maisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa January Makamba na nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kupongeza Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, kwa hoja yake nzuri inayohusu udhibiti wa shughuli za upangaji nyumba za makazi nchini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli isiofichika kuwa wapangaji wengi wanapata shida kwa wenye nyumba kwani wenye nyumba wanazo Sheria ngumu mfano kulipa kodi miezi sita au kodi ya mwaka mzima bila kujali shida au vipato vya wapangaji, ukizingatia watumishi wengine huwa wameanza kazi kipindi cha muda mfupi sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile ni ukweli usiofichika kuwa Serikali inakosa mapato mengi kutoka kwa madalali ambao hujipatia fedha bila jasho pamoja na wenye nyumba kutolipa kodi wala ushuru, hivyo Sheria itungwe kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalizie kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Tibaijuka (Mb), kwa kukiri upungufu na kukubali kutunga Sheria. Vilevile ninaishauri Serikali kutunga Sera ndipo walete Muswada wa Sheria hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa January Yusuf Makamba (Mb) mia kwa mia.

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita mtoa hoja, yuko wapi?

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuhitimisha hoja yangu. Kwanza, naomba nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuunga mkono hoja pale nilipoitoa. Nawashukuru sana kwa sababu jambo hili ni muhimu kwa ustawi wa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua na kuwashukuru wote waliochangia, nikianza na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Diana Chilolo, ambaye amechangia kwa maandishi, Mheshimiwa Aeshi Hilaly ambaye naye amechangia kwa maandishi na Mheshimiwa Ester Bulaya ambaye amemaliza kuongea sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kwamba Serikali haina kipingamizi na inayatambua matatizo ambayo niliyacainisha kwenye hoja yangu na kwamba tatizo hili tunaliona wote kwa pamoja. Hilo ndilo jambo la msingi kwamba Serikali na yenyewe inaliona tatizo.

Mheshimiwa Spika, napata matatizo kidogo kwa sababu nilikuwa naamini kwamba tunayo Sera ya Maendeleo ya Makazi. Nimesoma taarifa ya mafanikio ya Serikali katika miaka 50 ya uhuru katika Sekta ya Ardhi na ninaomba ninukuu sehemu moja, inasema:-

"Katika uendelezaji wa Sekta ya Nyumba, Wizara imefanya utafiti wa hali ya nyumba nchini, utafiti huu ulisaidia katika kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000".

Mheshimiwa Spika, sasa sina hakika sababu tunaongelea mambo ya makazi, sina hakika Mheshimiwa Waziri Sera anayosema kwamba lazima tuanze nayo kabla ya hii Sheria, ni Sera ipi na labda tu turidhishane hapa kwamba Sera hii haitoshelezi kutengeneza Sheria ya kudhibiti vitendo vinavyoendelea sasa hivi kwenye upangaji. Kama haitoshi basi nitaelewa lakini ni imani yangu na ningeshangaa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi hadi leo ingekuwa haina Sera ya Makazi lakini Sera hiyo ipo na tumesoma ipo hata kwenye website ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba jambo hili linahitaji muda kwa sababu ni jambo kubwa, linaathiri sehemu kubwa ya mfumo wa kijamii na uchumi wa nchi yetu. Napenda kusisitiza kwamba basi usiwe muda mrefu labda tu atuambie kwamba muda gani, mwaka mmoja, miaka miwili ili tuweze kujua na mimi imani yangu ni kwamba jambo hili halihitaji muda mrefu kwa sababu mashauriano na wadau, na wadau kwenye jambo hili wako tayari, hata ukiwaita wiki ijayo tulizungumze jambo hili wako tayari, kwa sababu matatizo ni mengi na yanajulikana.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa kwamba huwezi kuwa na Sheria bila Sera lakini wananchi kule, ambao wanahangaika, ukiwaambia tupe muda tutengeneze Sera, kwanza ni jambo gumu kidogo kulielewa kwa sababu Sheria ndiyo inaweka meno, ndiyo inaweka adhabu kwa vitendo vya hovyo vinavyoendelea, Sera nafahamu inaweka mwongozo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, rai yangu ni kwamba tuharakishe hiyo Sera, kama hii Sera ya Maendeleo ya Makazi haitoshelezi basi tuharakishe kutengeneza hiyo Sera mpya kama inahitaji marekebisha ili iwezeshe Sheria hii ambayo inapendekezwa kwa sababu tunaposema tuchukue muda mrefu, muda huohuo mrefu ndipo ambapo manyanyaso na mateso yanaendelea. Muda huohuo ambao tunasema tunahitaji ndiyo Serikali inazidi kupoteza mapato. Kama walivyosema Mheshimiwa Mbowe na wengine waliochangia, mapato yanayopotea ni makubwa. Kwa hiyo, ni kwa manufaa yetu sisi sote, jambo hili liishe haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu nikubali lakini kwa kuomba ufafanuzi zaidi kuhusu Sera hii ya Makazi, je, haitoshelezi kuunda Sheria mpya? Pili, je, huo muda ambao Serikali inaomba basi ni muda gani ili sisi sote tujue tuwe tayari kushiriki kwa pamoja kwenye kuchangia Sheria hiyo mpya na kuanzisha mamlaka mpya ya uhibitaji wa shughuli za upangaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru, naomba kutoa hoja. (Makofi)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja Binafsi ya Mheshimiwa January Y. Makamba ilipitishwa na Bunge kwa Serikali kuifanyia kazi kwa mujibu wa taratibu)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, ufafanuzi kidogo. Nimefanya hilo kwa sababu hoja yake ilikuwepo, yeye ndiye mwenye hoja amefunga. Kwa hiyo, nisingeweza tena kumwita Waziri, tumemaliza, sasa Waziri aseme ili tuondoke bila mashaka.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nawashukuru wachangiaji wote kama nilivyosema, hapa kuna *Human Settlements Development Policy* ambayo kwa Kiswahili tunasema Makazi pia kuna *Housing Policy* na kweli kama nilivyosema, Ibara ya 60 katika Ilani ya CCM ilikuwa inatambua *Housing Policy* na Serikali yake imejiandaa, tuko katika mchakato wa kumaliza *Housing Policy*. Kwa hiyo, kwa ufanunuzi *Human Settlement Development Policy* ndiyo ilikamilika, tunasema ni Sera ya Makazi ambayo inajumuisha Mipango Miji lakini *Housing Policy* ambayo itaingiza vipengele vingi vya ujenzi bado ndiyo tunafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba hili jambo ni muhimu, hali halisi ya Wizara yangu mnaifahamu, bajeti ni finyu sana. Kwa mfano, mchakato huu kidogo ulikuwa umesimama kutokana na hali halisi ya sasa hivi inayotukabili lakini labda kwa sababu ya uharaka wa mambo ambayo wote tunakubaliana, itabidi sasa katika hii bajeti inayokuja suala la kumalizana na *Housing Policy* kusudi tuweke Sheria inayoweza ku-*regulate Real Estate* ifanyiwe kazi. Kwa sasa hivi tuna *Human Settlement Development Policy*, ni tofauti na Sera ya Nyumba. Sera ya Nyumba inaingiza zaidi *aspects* za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, asubuhi nilitangaza kwamba kuna wachezaji wetu na viongozi wao wa timu ya *Villa Squad Sports Club* ya Kinondoni. Wakati ule nadhani walikuwa ama hawajafika ama walikosa nafasi hapa, sasa wameingia. Tuombe msimame mtupungie mikono, ahsante sana. (Makofi)

Tunajua kesho mnacheza, kwa hiyo Waheshimiwa wengine watakuwepo. Wengine bahati mbaya hivi leo tunaahirisha mambo yetu, lakini watakaokuwepo mnakaribishwa, hawa ndugu watacheza na Timu ya Polisi ya Dodoma. Kwa hiyo, kesho kutakuwa na mchezo mzuri. Ahsante sana, poleni na safari na tunawatakia kheri katika mchezo mtakaocheza. (Makofi)

Halafu Waheshimiwa Wabunge, hapa nimepata tangazo kutoka Utawala wa Bunge kwamba niwatangazie Wabunge wote kwamba kampuni ya *Serengeti Breweries Limited* ambao ni wadau wakuu kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa katika nyanja ya michezo, wameandaa tamasha kwa lengo la kuukaribisha mwaka 2012 na kuzindua bidhaa yao mpya. Tamasha hilo litafanyika katika ukumbi wa *Royal Village* leo tarehe 10 Februari, 2012. Kutokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Kampuni hii na Bunge letu, wanawakaribisheni wote kushiriki kwenye tamasha hilo, kutakuwa na burudani mbalimbali, chakula, vinywaji na muziki wa Bendi ya Ali Choki itatumbuiza. Hawakusema muda, kwa hiyo, mnakaribishwa sijui saa ngapi. (Makofi)

Nina tangazo lingine muhimu. Waheshimiwa Wabunge, ninyi wenyewe mme-note hapa kwamba katika Maazimio yetu tuliyokuwa tumefanya wakati ule kwamba katika Bunge la Tano Serikali ingekuja na utekelezaji wa Maazimio ya Kamati Ndogo ya Gesi na Kamati Teule. Ile ya Gesi tumefanya lakini Kamati Teule hatukufanya. Serikali iliniletea barua kuomba, nisome kama ilivyo: Waheshimiwa Wabunge mtatambua kwamba katika Mkutano huu wa Sita tulipanga kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Serikali kuhusu Maazimio ya Bunge ya Kamati Teule iliyochunguza uhalali wa utaratibu wa Wizara kuchangisha fedha za kupitisha bajeti Bungeni na Serikali kuahidi kufanyia kazi na kuyatolea taarifa katika Mkutano huu

wa Sita. Hata hivyo, nimepokea barua kutoka Serikalini ikiomba kuongezewa muda hadi Mkutano wa Saba. Kwa kuzingatia uzito wa maswali yaliyopo katika taarifa ya Kamati Teule iliyoshughulikia masuala hayo na ili Serikali iweze kushughulikia kikamilifu na kwa usahihi na kutoa majibu ya maswali ya Maazimio yote kwa uhakika, nimekubali Serikali iongezewe muda, wafanyie kazi maswali hayo ili iwasilishe majibu ya Maazimio yote kwa uhakika katika Mkutano wa Saba wa Bunge la mwezi Aprili, 2012.

Mapendekezo ya Kamati Teule yalihusu Mamlaka ya Rais kwa Watendaji Wakuu walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mengine yalikuwa mahusiano kati ya Watendaji Wakuu na Mawaziri, mahusiano ya Mihimili miwili, Serikali na Bunge. Kwa hiyo, imeonekana haya mambo yanatakiwa kufanyiwa utafiti mwingi zaidi wa kisheria kwa upande wa Serikali. Kwa hiyo, nimekubali kwamba walete kikao kijacho cha Bunge.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge naomba nitishe shughuli hizi mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.08 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Katibu!

KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba, shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano wa Sita, ulionza terehe 31 Januari, 2012 zimekamiliika. Naomba kutoa Taarifa.

SPIKA: Katibu!

KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu! *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, leo tumefika mwisho wa Mkutano wa Sita wa Bunge lako Tukufu. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukamilisha kwa wakati majukumu yaliyopangwa katika kipindi hiki kwa ufanisi. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wenu mkubwa mliouonesha ndani na nje ya Bunge letu Tukufu katika kufanikisha shughuli za Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali na Wabunge Wenzangu, kutoa rambirambi kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa familia, jamaa na marafiki kwa msiba mkubwa uliotokana na vifo vya Waheshimiwa Wabunge, Marehemu Regia Estelatus Mtema, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA) na Marehemu Jeremia Solomon Sumari, Mbunge wa Arumeru Mashariki (CCM) vilivyotokea baada ya Mkutano wa Tano wa Bunge. Vilevile, natoa rambirambi kwa kumpoteza mfanyakazi wa Bunge, Marehemu Nicodemus Senge aliyepoteza maisha katika kipindi hicho. Mtakumbuka pia kwamba katika muda huo, tulipata msiba wa Marehemu Mzee Steven Galinoma aliyemaliza muda wake wa kuwa Mbunge wa Bunge hili mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kupitia Bunge lako Tukufu kutoa salaam za rambirambi na pole nyingi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu wote waliopoteza maisha kutokana na majanga mbalimbali ikiwemo mafuriko yaliyotokea Dar es Salaam na Mbeya na ajali mbalimbali zilizotokea katika kipindi kilichopita. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, kwa takribani miezi nane iliyopita hususan kuanzia Mkutano wa Tano wa Bunge, tumekuwa na Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamekuwa wakisumbuliwa na maradhi mbalimbali. Kati ya Waheshimiwa Wabunge hao, yupo Mheshimiwa Profesa Mark James Mwandosya, Mbunge wa Rungwe Mashariki na Waziri wa Maji. Yupo pia Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, Mbunge wa Kyela na Naibu Waziri wa Ujenzi ambao hadi sasa wanaendelea kupatiwa

matibabu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awasaidie waweze kupona haraka na kurudia katika afya zao.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Sita tunaouhitimisha leo, jumla ya Maswali 119 ya Msingi na mengine 290 ya nyongeza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge yalipata majibu ya Serikali. Vilevile, jumla ya Maswali Nane (8) ya Msingi na Manne (4) ya nyongeza kupitia utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yalijibiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu Miswada ifuatayo ilisomwa kwa Mara ya Kwanza, Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania wa Mwaka 2011 (*The Tanzania Livestock Research Institute Bill, 2011*) na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2012 (*The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2012*).

Mheshimiwa Spika, aidha, Miswada ifuatayo ilisomwa na kujadiliwa katika hatua zote, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Fedha Haramu wa Mwaka 2012 (*The Anti-Money Laundering (Amendments) Bill, 2012*) na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 (*The Constitutional Review (Amendments) Bill, 2011*).

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia limeridhia Azimio la Bunge kuhusu Mkataba wa Vijana wa Afrika (*The African Youth Charter*) wa Mwaka 2006. Aidha, lilijadili Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147. Hata hivyo, pamoja na kujadili, Azimio hili halikupitishwa kwa vile ilibainika kwamba, halina maslahi kwa mwananchi wa kawaida na hivyo kurejeshwa kwa ajili ya tafakuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walipokea Kauli ya Serikali kutoka kwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu mgomo wa Madaktari. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali imechukua hatua mbalimbali za kumaliza mgomo huu. Aidha, imeshughulikia baadhi ya madai ya Madaktari na mengine yanaendelea kushughulikiwa. Madaktari wetu wamerejea kazini leo na kuendelea kutoa huduma za fiba na hivyo kuokoa maisha ya wagonjwa wasio na hatia ili wasiteseke na pia kuokoa maisha yao. Serikali itaendelea kushirikiana na vyombo vyote kuhakikisha tatizo hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii na Waheshimiwa Wabunge wote kwa nia njema mliyoionesha katika kuhakikisha mgomo huu unafikia tamati. Niwashukuru pia, makundi mbalimbali ya jamii wakiwemo Viongozi wa Dini, Madaktari wa Jeshi, Madaktari Bingwa, Wauguzi ambao pamoja na hali yote ilivyokuwa, walionesha nia ya kuwasaidia wananchi ambao walihitaji huduma wakati wa mgomo huu. Niwashukuru pia wananchi wote kwa uvumilivu wao. Ni dhahiri tumejifunza mengi na wajibu wetu kama Serikali ni kuhakikisha kwamba hali kama hii haijirudii tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipata fursa ya kupokea na kujadili Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge lililotokana na Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi Nchini. Aidha, Waheshimiwa Wabunge walipokea Hoja Binafsi za Wabunge kuhusu Hali ya Zao la Mkonge Nchini na kuazimia kwamba Mwaka 2012 uwe Mwaka wa kupanda Mkonge na Hoja Binafsi ya Kuitaka Serikali ilete Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Upangaji wa Nyumba (*Rental Housing Act*) kwenye Mkutano ujao wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya katika siku zote za Mkutano huu hivyo kuweza kupitisha Miswada hiyo na kuridhia Maazimio niliyotaja. Aidha, nawashukuru kwa michango yenu wakati wa kujadili Taarifa zilizowasilishwa hapa Bungeni. Ni dhahiri mjadala ulikuwa na hoja nzuri za kuishauri Serikali ipasavyo. Serikali itazingatia ushauri huo kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba yangu hii ningependa kuzungumzia mambo machache yanayohusu hali ya Chakula Nchini, mwenendo wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Ufugaji Nyuki. Aidha, nitazungumzia kuhusu Hali ya Usalama Nchini; uendelezaji wa Sayansi na Mafunzo ya Ufundi Nchini, dhana na umuhimu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na matokeo ya Tathmini ya Mpango wa kuzijengea uwezo na kuzipatia Ruzuku ya Maendeleo Mamlaka za Serikali za

Mitaa. Mwisho nitazungumzia matokeo ya maamuzi ya Serikali katika Uondoaji Ushuru kwenye Mafuta ya Taa na Uchakachujaji wa Mafuta.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Hali ya Chakula; moja ya faida za Mapinduzi ya Kilimo zilizoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010 ni kuipatia kila familia, Kijiji na Tarafa chakula cha kutosha ili kukomesha njaa. Matokeo ya tathmini ya Hali ya Chakula iliyofanyika mwezi Desemba 2011 kwa ajili ya upatikanaji wa chakula msimu wa 2010/2011, inaonesha kwamba uzalishaji wa mazao ya chakula uliweza kufikia tani milioni 12.97 ikiwemo tani milioni 7.03 za nafaka na tani milioni 5.94 za mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula nchini kwa mwaka 2011/2012, ni jumla tani milioni 11.53. Kwa mujibu wa takwimu hizo, Taifa linatarajia kujitoshesha kwa chakula na kupata ziada ya tani milioni 1.44. Hata hivyo, tathmini inaonesha kuwa ziada hiyo ilitokana na mazao yasiyo ya nafaka kwani uhaba wa nafaka uliokuwepo ulikuwa kiasi cha tani 204,821.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa ziada ya chakula Kitaifa, yapo maeneo ambayo yanakabiliwa na uhaba wa chakula. Uhaba huo ulikuwepo zaidi kwenye baadhi ya Mikoa iliyokabiliwa na ukame. Mikoa yenye uhaba wa chakula ni pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam ambao unategemea chakula kutoka Mikoani. Aidha, maeneo mengine yaliyokuwa na upungufu wa nafaka yapo katika Halmashauri 45 za Mikoa 11 ya Arusha, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Mwanza, Tabora, Shinyanga, Manyara, Mara, Kagera na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, taarifa tulizozipata katika miezi ya Januari na Februari 2012 zinaonesha kuimarika kwa hali ya chakula nchini katika baadhi ya maeneo yaliyoonekana awali kuwa na uhaba wa chakula. Hali ya mazao mashambani inaonekana kuwa katika hatua mbalimbali za ukuaji na mvua zinaendelea kunyesha vizuri, hasa kwa Mikoa ile ambayo inapata mvua za vuli. Hivyo, kwa sasa hali ya chakula inaendelea kuimarika katika maeneo mengi na mavuno ya mazao ya vuli yanatarajiwa kuchangia asilimia 22 ya uzalishaji wa chakula nchini. Matarajio yetu ni kuwa upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2011/2012 utakuwa wa kuridhisha hasa iwapo mvua za masika zitanyesha vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuondolewa kwa zuio la kuuza mahindi nje ya nchi. Itakumbukwa kuwa mwezi Julai 2011, Serikali ilisitisha kwa muda usafirishaji na uuzaji wa mahindi nje ya nchi kwa lengo la kujihakikishia upatikanaji wa chakula cha kutoshesha mahitaji ya ndani ya nchi. Zuio hilo lilifuatia ukame mkubwa uliotokea katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli, hasa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini iliyofanyika mwezi Novemba, 2011, inaonesha kuwepo kwa ziada ya mahindi katika Mikoa ya Ruvuma, Rukwa na Mbeya. Aidha, taarifa za tathmini za msimu wa kilimo wa 2011/2012, zimeweza Serikali kubaini kuwa, hatari ya kuwepo njaa katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Shinyanga na Mara imeondoka kutokana na mvua nzuri za vuli zinazoendelea; mahindi mengi bado yapo mikononi mwa wakulima katika Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Iringa na Mbeya; Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) hautaweza kuwafikia wakulima wote katika muda muafaka na kununua mahindi yao na wakulima wanahitaji fedha kwa ajili ya kununua pembejeo kwa ajili ya msimu wa kilimo 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzingatia hali hiyo, Serikali imeamua kuondoa zuio lililokuwa limewekwa kwa muda la kusitisha usafirishaji na uuzaji wa mahindi nje ya nchi. Hata hivyo, pamoja na kuondoa zuio hilo, nisisitize kwamba usafirishaji na uuzaji wa mahindi nje ya nchi kiholela na kwa njia ya magendo kupitia njia zisizoruhusiwa, hautakubalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahimiza wakulima na wafanyabiashara kwa pamoja kutumia fursa hii kuuza mahindi, kununua na kusafirisha popote nchini na nje ya nchi kwa kuzingatia taratibu na Sheria zilizopo. Ni matumaini yangu kuwa wafanyabiashara wote wenye nia ya kufanya biashara ya mahindi ndani na nje ya nchi watazingatia maelekezo ya Serikali kuwa bei ya kununulia mahindi isiwe chini ya shilingi 350/= kwa kilo na kuwalipa wakulima fedha taslimu badala ya kuwakopa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kuondolewa kwa zuio hili kutaleta changamoto nyingi hasa katika maeneo ya mipakani na yale yenye uhaba mkubwa wa chakula. Hivyo, natoa wito kwa viongozi wa Mikoa na Wilaya katika maeneo yenye ziada ya chakula kutoa taarifa na kuwahamasisha wafanyabiashara ili wajitokeze kununua, kusafirisha na kuuza mahindi kwenye Mikoa yenye uhaba wa

chakula na nje ya nchi. Aidha, viongozi katika ngazi zote wahakikishe kuwa utaratibu mzima wa kununua mahindi unasimamiwa kwa umakini mkubwa ili kuwanufaisha wakulima wengi maskini walioko Vijijini. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inaagizwa kutoa Mwongozo mahsusi kuhusu utaratibu wa usafirishaji na uuzaji wa mahindi nje ya nchi kuanisha wajibu na majukumu ya Watendaji katika kila ngazi kuanzia kwenye Vijiji, Wilaya hadi Mkoani ili kuepuka urasimu usio wa lazima kwa wakulima na wafanyabiashara watakaoshiriki kwenye zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa pembejeo za kilimo. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Aya ya 33 (f) inasisitiza umuhimu wa kuimarisha mashamba ya mbegu ya Serikali ili kuongeza uzalishaji mbegu bora za mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta na kuzisambaza kwa walengwa wazitumie. Katika maandalizi ya msimu wa kilimo kwa mwaka 2011/2012, Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa mpango wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo muhimu za kilimo zikiwemo mbegu unafanikiwa. Lengo ni kuwafikishia wakulima pembejeo kwa wakati ili kuwahi msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa azma hiyo, hadi kufikia Desemba 2011 jumla ya tani 23,437 za mbegu bora za nafaka (mahindi na mtama) zilikuwa zimepatikana na kusambazwa katika sehemu mbalimbali nchini sawa na asilimia 78 ya mahitaji. Aidha, kiasi cha tani 246,454 cha aina mbalimbali za mbolea kilikuwa kimeingizwa nchini na kusambazwa Mikoani katika kipindi hicho. Kiasi kingine cha tani 129,711 za mbolea kinatarajiwa kuingizwa nchini mwishoni mwa mwezi huu wa Februari 2012 ili kukamilisha jumla ya tani 400,000 zinazotosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya maandalizi ya kilimo katika msimu huu, chini ya Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo kupitia Mfumo wa Vocha, Serikali imefanikiwa kusambaza kwa wakulima jumla ya tani 18,157 za mbegu za mpunga na mahindi; tani 180,000 za mbolea, miche ya kahawa milioni 10 na miche ya mhai milioni 10. Aidha, tani 19,475 za mbegu za pamba na lita milioni 3.342 za madawa ya pamba pamoja na tani 64,000 za madawa ya korosho zimesambazwa kwa wakulima. Vilevile, lita 16,000 za viuatilifu na kilo 1,400 dawa za kudhibiti panya zimeingizwa nchini. Napenda kulijulisha Bunge lako kuwa jumla ya vocha milioni 5.4 zimekwishachapishwa na kusambazwa katika Mikoa 20 yenye Wilaya 96 kwa ajili ya kuwapatia wakulima. Jumla ya Mawakala wa Pembejeo za Kilimo wapatao 3,855 kutoka Mikoa mbalimbali nchini wamekwishapatiwa mafunzo ya uendeshaji wa biashara pamoja na matumizi sahihi na hifadhi salama ya pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwataka Viongozi wa Mikoa na Wilaya nchini pamoja na Maafisa Ugani na Watendaji wa Vijiji pamoja na Kamati zinazosimamia mpango huu, kuhakikisha vocha zinawafikia wakulima walengwa na Mawakala walioteuliwa wanawafikishia wakulima pembejeo kwa wakati na kuziua kwa bei iliyopangwa. Serikali haitasita kuwachukulia hatua Viongozi, Maafisa Ugani, Mawakala na Watendaji wa Vijiji wasio waaminifu watakaovuruga mpango wa Serikali wa usambazaji wa vocha za ruzuku ya pembejeo za kilimo. Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 6.0 ambazo zimetumika kuwalipa Mawakala wote wa Pembejeo za Mazao ya Chakula. Aidha, Mawakala wa Pamba wanasubiri upatikanaji wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 4.53. Ni nia ya Serikali kulipa madeni yote mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, matayarisho kwa ajili ya mvua za masika. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2011/2012, Serikali imejipanga kutumia mvua za masika vizuri kwa kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma muhimu za kilimo zimewafikia wakulima mapema na kwa wakati. Katika kufanikisha hilo, hadi kufikia tarehe 10 Novemba, 2011, jumla ya tani 20,987.64 za mbegu bora za mazao ya nafaka na mikunde zimewafikia wakulima. Aidha, ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa msimu 2011/2012 ambapo jumla ya vocha 5,400,000 zimekwisha sambazwa kwa wakulima 1,800,000 wanaozalisha mahindi na mpunga katika Mikoa 20. Lengo la Serikali ni kuwanufaisha wakulima 4,000,000 ifikapo mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ili kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima, Serikali imeajiri Wataalam 4,499 katika mwaka 2011/2012 ambapo kati yao 2,793 wamepangwa kwenye Halmashauri za Wilaya nchini. Jumla ya Wataalam 1,514 hawakupata ajira na 1,084 wanaotarajiwa kumaliza Vyuoni mwaka huu wataombewa kibali cha ajira Serikalini kwa pamoja. Nitoe wito kwa Halmashauri kuwapokea kwa dhati na kuwatumia Wataalam hawa vizuri kwa kuwapanga katika maeneo ya uzalishaji hususan Vijiji vya pembezoni na Skimu za Umwagiliaji ili waweze kutoa ushauri kwa wakulima wengi na hivyo kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa zana za kilimo ni nzuri. Hadi kufikia tarehe 30 Januari, 2012 kulikuwa na matrekta makubwa zaidi ya 1,619 na matrekta madogo zaidi ya 554. Aidha, matrekta makubwa 67 na *power tiller* 90 yameagizwa na makampuni na yanatarajiwa kuingia nchini ifikapo mwezi Machi, 2012. Katika hatua nyingine, Serikali imepunguza bei ya matrekta yanayosambazwa na *SUMA – JKT* kutoka asilimia 15 hadi 36. Kwa mfano, trekta la *Farmtrac 50 Hp* limepunguzwa bei kutoka shilingi milioni 25 hadi milioni 16. Lengo la punguzo hilo ni kuwezesha wakulima kupata matrekta hayo kwa urahisi zaidi. Matumaini yetu ni kwamba wakulima watatumia fursa hii kujiunga kivitundi kununua matrekta haya. Vituo vya mauzo vipo Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, na Mbeya. Makakati wa mauzo ni pamoja na kupunguza bei, kutangaza bei moja katika Vyombo vya Habari na kuandaa Vipindi vya Televisheni.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuangalia upya ushuru wa mazao na kodi mbalimbali katika kilimo. Ushuru wa mazao unatozwa kwa mujibu wa Kifungu 7(1)(g) cha Sheria ya Fedha ya Serikali ya Mitaa ya mwaka 1982. Kiwango cha ushuru unatozwa na Halmashauri ni kati ya asilimia 3 hadi 5 ya bei ya mkulima na kuchangia asilimia 60 hadi 80 ya mapato ya ndani ya Halmashauri husika. Hata hivyo, kiasi kinachorejeshwa na Halmashauri kuendeleza sekta ya kilimo kutokana na vyanzo hivyo ni kati ya asilimia 2 hadi 6. Hivyo, Halmashauri zina changamoto kubwa ya kuona namna ya kuongeza bajeti kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu mzima wa kukusanya na kusimamia mapato yatoakanayo na kodi za mazao imekuwa na changamoto nyingi. Baadhi ya changamoto hizo ni kutokuwepo kwa uwazi na usimamizi madhubuti ambako kumesababisha kuwepo kwa kero na kutokuaminiana baina ya mlipaji na aliyelipwa. Aidha, kiwango cha ushuru kinachotozwa hakizingatii gharama za uzalishaji hivyo, kupunguza motisha kwa wakulima na uwekezaji na hivyo kupunguza uwekezaji katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanyika kuhusu kodi katika mazao ya kilimo unaonesha kwamba zipo kodi nyingi zinazotozwa na kuathiri uzalishaji wa kilimo. Kodi hizi, baadhi ni Ushuru wa Forodha kwa Vipuri vya Mitambo na Matrekta, ushuru wa vifungashio, ushuru wa VAT kwa mbegu kutoka nje, kodi ya kuendeleza ujuzi, ushuru wa makampuni, kodi ya zuio na kodi ya mafuta ya kuendesha mitambo.

Vilevile, kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu wa Serikali kuangalia upya utaratibu wa utozaji wa ushuru wa mazao ili kuweka uwiano ambapo Halmashauri zitaendelea kupata mapato bila ya kuathiri mapato ya wakulima na uwekezaji katika kilimo. Utaratibu wa kutoza ushuru ni vizuri uzingatie gharama za uzalishaji na faida badala ya utaratibu wa kutoza kwenye mazao ghafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchunguzi huo, tayari Serikali imeweza kuondoa baadhi ya kodi hizo. Hata hivyo, kodi zilizobaki bado hazimvutii mkulima au mwekezaji. Hivyo, upo umuhimu wa kufanya mabadiliko ya mfumo wa ukusanyaji wa ushuru ili kuweka viwango ambavyo havitamfanya mkulima kupata hasara na hivyo kuongeza uzalishaji katika kilimo. Aidha, kuna umuhimu wa kuimarisha usimamizi katika kutoza ushuru ikiwa ni pamoja na kutumia vipimo kama mzani katika mauzo ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inajivunia kwa kuwa na idadi kubwa ya rasilimali ya mifugo ikiwemo ng'ombe milioni 21.3, mbuzi milioni 15.2, na kondoo milioni 6.4. Vilevile wapo kuku wa asili milioni 35 na wakisasa milioni 23 na nguruwe milioni 1.9. Pamoja na rasilimali hizo nyingi, wafugaji wetu wengi bado hawajaweza kuzingatia ipasavyo kanuni za ufugaji bora ili kuzalisha mifugo yenye ubora wa hali ya juu na tija kubwa. Ili kuongeza ubora wa mifugo na nyama inayozalishwa, Serikali inatekeleza mpango wa kuhamasisha na kutoa elimu kwa wafugaji juu ya teknolojia ya kunenepesha mifugo. Wengi wetu tunafahamu kuwa unenepeshaji mifugo unayo faida kubwa ikiwa ni pamoja na mfugaji kupata bei nzuri ya mifugo iliyonenepeshwa na soko linalohitaji nyama bora. Faida hizo ambazo baadhi ya wafugaji wamezitambua kutokana na elimu inayotolewa, utekelezaji wa mpango huu umeleta matumaini mapya kwa wafugaji wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2011 jumla ya ng'ombe 49,900 wamenenepeshwa ikilinganishwa na ng'ombe 37,200 walionenepeshwa katika kipindi kama hicho mwaka 2010. Unenepeshaji huo ulifanyika katika mikoa 11 ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Tabora, Singida, Arusha, Manyara, Rukwa, Iringa, Morogoro na Pwani. Unenepeshaji uliwezesha ng'ombe kuongezeka uzito wakati wa kuchinja kutoka wastani wa kilo 230 hadi kilo 350 kwa ng'ombe mmoja. Ili

kuendeleza mpango huu, Serikali hivi sasa inaendelea na utoaji wa elimu ya unenepeshaji wa mifugo kwa lengo la kuwawezesha wafugaji kuzalisha nyama bora kwa ajili ya masoko makubwa yanayoibuka hususan yale ya hoteli za kitalii, migodi na maduka makubwa ya vyakula mbalimbali (*Super market*). Ni matumaini yetu kuwa hatua hii itapunguza kiwango cha uingizaji wa nyama kutoka nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mpango huu, naiagiza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuharakisha kusambaza mwongozo unaohusu unenepeshaji mifugo na kanuni za ufugaji bora wa mifugo kwenda kwenye Halmashauri zote nchini ili ziweze kutoa msukumo na elimu kwa wafugaji kuhusu kanuni za ufugaji bora na faida za kunenepesha mifugo yao. Katika mwongozo huo, wafugaji pia waelimishwe kuhusu uzalishaji na hifadhi ya malisho ili waweze kujihakikishia kuwa na vyakula vya mifugo wakati wa kiangazi. Aidha, natoa rai kwa Wakuu wa Mikoa wote wawapangie viongozi mbalimbali wa Kitaifa ratiba za kutembelea mashamba darasa ya mifugo iliyonenepeshwa wakati wa ziara zao ili watoe maelekezo muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 30 Desemba, 2011 Serikali iliwataka wafugaji wote wanaoishi katika Bonde la Kilombero ambalo ni eneo la *Ramsar* chini ya Mkataba wa Kimataifa wa tarehe 25 Februari, 2002 unaokataza kufanyika kwa shughuli zozote za kilimo na mifugo katika maeneo ya hifadhi yanayotambulika Kimataifa kuondoka.

Mheshimiwa Spika, wafugaji waliohamia kwenye vijiji vinavyozunguka eneo la Bonde la Kilombero walipewa *notice* ya siku 14 ya kuanzia tarehe 1 hadi 14 Januari, 2012 wawe wameondoka kwenye Bonde la Kilombero. Aidha, wafugaji waliohamia kihalali wanatakiwa kufuga kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji ikiwa ni pamoja na kufuga mifugo kulingana na ukubwa wa eneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile baadhi ya wafugaji pia ni wakulima katika eneo hilo, Serikali imesikia kilio cha wananchi wa Kilombero ambao wameathirika na zoezi hili na hivyo imeamua kutoa muda wa ziada kwa wafugaji na wakulima kuvuna mazao yao ya msimu wa vuli na yale yatakayopandwa kipindi cha mvua za masika. Kwa mantiki hiyo, zoezi la kuwaondoa na kuwahamisha wafugaji kutoka Bonde la Kilombero limesogezwa mbele hadi mwezi Agosti na Septemba, 2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda ieleweke kuwa dhamira ya Serikali ya kutekeleza zoezi hili ni ili kuhifadhi mazingira kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa wafugaji na wananchi wote kuheshimu na kutokuvamia vyanzo vya maji na maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye maeneo hayo, tunaporudi Majimboni mwetu tutumie muda huo kuwaasa wananchi, hasa wale wanaotakiwa kuhamisha mifugo yao kutumia muda wa ziada uliotolewa na Serikali kufanya maandalizi muhimu ya kuhamisha mifugo yao. Aidha, nichukue nafasi hii kuupongeza uongozi wa Wilaya ya Kilombero ambao umekwishatenga jumla ya ekari 67,872.3 katika vijiji 24 nje ya eneo la *Ramsar* kwa ajili ya wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kuwaomba viongozi katika maeneo mbalimbali nchini kutumia sheria na mpango wa matumizi bora ya ardhi kutenga maeneo ya malisho ya mifugo na kuzingatia sheria na mpango huu. Ninapenda kuwahimiza wananchi wote hususan wafugaji wahamaji kufuata utaratibu huu ili kupata makazi ya kudumu kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa kisasa na ulio endelevu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tunaporudi Majimboni mwetu hasa kwenye maeneo yenye matatizo na migogoro ya ardhi tutumie muda huo kuwaasa wafugaji umuhimu wa kuchunga mifugo katika maeneo yaliyotengwa kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi inayo fursa kubwa ya kupunguza umaskini miongoni mwa wananchi wengi waliopo vijijini. Hata hivyo, mchango wa sekta hii kwa Pato la Taifa umekuwa bado mdogo wa wastani wa asilimia 1.5 licha ya fursa zilizopo. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 inaelekeza Serikali kuiendeleza sekta ya uvuvi ili iwe ya kisasa zaidi na iweze kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye Pato la Taifa. Kwa kutambua hali hiyo, maelekezo hayo nitaelezea kidogo hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kulinda rasilimali ya samaki katika sekta hiyo kama sehemu ya kukuza sekta ya uvuvi nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uvuvi haramu na usiozingatia Sheria ya Uvuvi ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta ya uvuvi. Ili kuhakikisha uvunaji endelevu wa rasilimali hii, Serikali imeanzisha vituo 20 vya ulinzi shirikishi wa rasilimali ya uvuvi nchini. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2011 zimefanyika jumla ya

doria 3,288 ambapo zana haramu zipatazo 816,957 ikijumuisha nyavu na makokoro zilikamatwa na watuhumiwa 385 walikamatwa na kushitakiwa. Ni dhahiri kwamba doria hizi zimekuwa na umuhimu mkubwa wa kulinda rasilimali za uvuvi katika maziwa na bahari. Aidha, matokeo ya juhudi hizi ni kuongezeka kwa wingi na ubora wa samaki wanaovuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka na biashara haramu ya uvuvi ninatoa wito kwa Wizara za Kisekta, Mifugo na Uvuvi, Mambo ya Ndani, Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kushirikiana kwa karibu ili kuimarisha zoezi la doria katika maziwa na mito na pia katika mipaka ya nchi yetu. Kwa kufanya hivyo, tutawahakikishia wananchi ajira, kipato na lishe bora kutokana na mazao ya samaki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa upatikanaji wa samaki na viumbe wengine wamekuwa wakipungua siku hadi siku katika maji ya asili kama bahari, maziwa na mito, Serikali imeamua kutekeleza mkakati wa Taifa wa ukuzaji endelevu wa viumbe kwenye maji. Viumbe wanaokuzwa ni pamoja na samaki na ukulima wa mwani. Mkakati huo unajulikana kama *National Aquaculture Development Strategy*. (Makofi)

Katika utekelezaji wa mkakati huo, hadi kufikia Desemba, 2011 jumla ya vifaranga milioni 1.74 vimezalishwa, sawa na asilimia 58 ya lengo la kuzalisha vifaranga milioni 3.0 mwaka 2011/2012 na hivyo kupunguza mahitaji makubwa ya vifaranga yanayokadiriwa kufikia milioni 4.8. Aidha, sekta binafsi (Kampuni ya Alphakrust) katika kipindi hicho imezalisha vifaranga vya kamba miti milioni 1.8. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa zinazokabili mpango huo ni kuhamasisha sekta binafsi na wadau wengine kushiriki kikamilifu katika uzalishaji wa vifaranga wa samaki katika sehemu mbalimbali nchini ili huduma hiyo iweze kuenea kwa kasi na kuwezesha wafugaji samaki wengi kupata vifaranga kwa bei nafuu. (Makofi)

Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, tayari kuna vituo vya Serikali vya kuzalisha vifaranga vya Kikanda vilivyoko Rulula Songea, kwa ajili ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini; Kituo cha Sikonge kwa ajili ya Kanda ya Magharibi; Vituo vya Mwanza, Bukoba na Musoma kwa ajili ya Kanda ya Ziwa Victoria; Kituo cha Karanga kwa ajili ya Kanda ya Kaskazini; Kituo cha Kingolwira kwa ajili ya Kanda ya Mashariki; na Kituo cha Mtama kwa ajili ya Kanda ya Kusini. Nitoe wito kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuendelea kushirikiana na Halmashauri husika kuimarisha vituo hivyo ili viweze kutoa elimu na vifaranga bora kwa wananchi wanaojihusisha na ufugaji wa samaki na viumbe wengine wa majini.

Vilevile Halmashauri zote nchini zione umuhimu wa kuanzisha miradi ya ufugaji wa samaki kama shughuli mbadala za kuongeza kipato kwa wananchi wa maeneo yao. Ni dhahiri kwamba kuwashirikisha wananchi wengi katika ufugaji wa samaki kutaimarisha kipato na lishe katika kaya na kujenga uchumi endelevu kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla wake. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge nasi katika Majimbo yetu tushiriki kuhamasisha wananchi na wadau wengine kuhusu faida za kuendeleza uvuvi kwa kuanzisha mabwawa ya ufugaji samaki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sekta ya nyuki inayo fursa ya kuchangia Pato la Taifa na kuondoa umaskini. Hii inatokana na ukweli kwamba ufugaji na nyuki nchini unaweza kufanywa katika misitu yenye ukubwa wa hekta milioni 38.8 na kwenye maeneo ya mashamba ya kilimo na kuweza kuzalisha tani 138,000 za asali na 9,200 za nta kwa mwaka. Aidha, ufugaji wa nyuki katika jamii nyingi umeendelea kuwa chanzo cha ajira na kuongeza kipato cha wananchi wengi. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 inaelekeza Serikali kuongeza msukumo katika kuendeleza ufugaji nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta kibiashara. (Makofi)

Napenda tena kusisitiza kwamba ufugaji nyuki ni biashara iliyo rahisi na nyepesi kuwezesha wananchi kupata kipato kikubwa na cha haraka. Biashara na soko la asali na nta linaongezeka siku hadi siku kutokana na matumizi yake kama dawa na chakula. Kwa sasa bei ya asali imekuwa inaongezeka kwa kasi ambapo kwa soko la ndani bei ya lita moja ya asali inauzwa kwa shilingi 10,000 hadi 12,000 ikilinganisha na shilingi 8,000 kwa lita mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango wa ufugaji nyuki nchini, kuanzia kipindi cha mwaka 2011/2012 inakadiriwa kuzalisha jumla ya tani 9,000 za asali yenye thamani ya shilingi bilioni 27 na tani 600 za nta zenye thamani ya shilingi bilioni 3.0. Hata hivyo, uzalishaji huo ni asilimia 6.5 tu ya uwezo wa uzalishaji hapa nchini, kiasi ambacho kimeongezeka kutoka wastani wa asilimia 3.5 mwaka 1998. Aidha, katika kipindi cha kuanza Julai hadi Desemba 2011 jumla ya tani 229.9 za asali na tani 292 za nta zimeuzwa katika soko la Ulaya, Marekani, Japan, Falme za Kiarabu na Oman. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo mzuri wa biashara ya uuzaji wa asali na nta katika soko la ndani na nje, natoa tena wito kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wote kuwahamasisha wananchi juu ya faida na umuhimu wa kuanzisha ufugaji wa nyuki na kuwekeza katika uchakataji, ufungashaji, usafirishaji na uuzaji wa mazao ya nyuki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati Tanzania inapiga hatua katika ufugaji wa nyuki na uzalishaji wa mazao yake, baadhi ya wafanyabiashara wameanza kupata vikwazo kuhusu ubora wa bidhaa hizo. Ili kuondokana na hofu ya kuzalisha asali na nta yenye kemikali kama *nicotine*, wafugaji wa asali wanashauriwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji nyuki ikiwa ni pamoja na kuweka mizinga umbali wa kilomita 7 kutoka kwenye maeneo ya viwanda na mashamba ya kilimo yanayotumia kemikali kwa wingi. Vilevile, ili kulinda soko la bidhaa za nyuki, Shirika la Viwango tayari limeandaa viwango vya ubora wa asali ya Tanzania. Viwango hivyo vinatumika kuitangaza asali ya Tanzania ndani na nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba wadau wa kuzalisha asali na nta wameandaa maonesho ya bidhaa za nyuki yatakayofanyika katika viwanja vya Mwalimu Nyerere (Saba Saba) Dar es Salaam kuanzia tarehe 3 hadi 6 Oktoba, 2012. Maonesho haya ni juhudi za sekta binafsi kwa kushirikiana na Wakala wa Biashara (TANTRADE) kuanza kuitangaza asali ya Tanzania ndani na nje ya nchi. (Makofi)

Aidha, Wakala wa Biashara (TANTRADE) wataandaa Banda Maalum la asali wakati wa Maonesho ya Saba Saba ya mwaka 2012 ili kutoa fursa zaidi kwa wajasiriamali kupata ufahamu juu ya maonesho hayo. Nitoe wito kwa Watanzania wote hususan wadau wa zao la nyuki, wazalishaji wa asali waanze kujiandaa kushiriki maonesho hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuongeza soko na kutoa fursa kwa wadau wa nyuki kuwekeza zaidi katika uzalishaji na biashara ya asali.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa wito kwa wazalishaji na wasafirishaji wa asali na nta nje ya nchi kupeleka sampuli ya bidhaa zao Shirika la Viwango (TBS) kabla ya kuisafirisha. Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ihakikishe inasogeza huduma za upimaji wa sampuli karibu na wazalishaji. (Makofi)

Pia upo umuhimu wa Mikoa na Halmshauri kuimarisha usimamizi wa biashara ya asali na nta ili ifanyike kwa kuzingatia Sheria na taratibu zilizowekwa na kudhibiti wafanyabiashara wasio waaminifu wanaoharibu Soko la asali ya Tanzania hususan katika maeneo ya mpakani. Halmshauri pia zina wajibu wa kuwaelimisha wafanyabiashara wa asali na nta ili wajisajili katika Wilaya husika na kufanya ununuzi wa asali na nta kwa uwazi na kulipia kodi na ushuru wa Serikali. Katika kuimarisha ushirika na vikundi vya wazalishaji wa bidhaa za nyuki, natoa wito kwa Halmshauri zote kutenga fedha za kutosha kuendeleza sekta ya nyuki ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kuimarisha vyama hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia kushamiri kwa matatizo ya uhamiaji haramu nchini. Taarifa zinaonesha kuwa tatizo la uhamiaji haramu nchini linajitokeza katika sura nne kama ifuatavyo:-

(i) Wapo wahamiaji haramu ambao ni matokeo ya vurugu za kisiasa katika nchi zao;

(ii) Kundi lingine ni wahamiaji wa kawaida wanaoingia nchini bila kufuata sheria na taratibu. Wengi wao wanatokea nchi jirani; kama vile Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Msumbiji wakiwa na dhamira ya kutafuta maisha;

(iii) Wapo wahamiaji haramu ambao huingia nchini kihalali lakini hujishughulisha na kazi ambazo hawakuruhusiwa. Wengine mara vibali vinapoisha muda huamua kuishi nchini bila kufuata utaratibu; na

(iv) Kundi la nne na la mwisho ni wahamiaji haramu wa mkupuo hususan wanaotoka nchi za Ethiopia, Eritrea, Somalia na nchi za Asia; Pakistani na Bangladeshi wakiwa na lengo la kwenda Afrika Kusini na nchi za Ulaya au Amerika kutatufa maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matukio mbalimbali ya kukamatwa wahamiaji haramu katika mikoa ya mipakani na kwingineko yanaashiria kushamiri kwa tatizo la uhamiaji haramu. Wahamiaji haramu kutoka Ethiopia, Eritrea na Somalia wamekuwa wakitumia mipaka ya mikoa inayopakana na Kenya kuingia nchini kama njia ya kupita kuelekea Afrika Kusini na nchi nyinginezo za Ulaya na Amerika. Kati ya mwezi Desemba, 2011 na Januari, 2012 jumla ya wahamiaji haramu 728 walikamatwa kwa kuingia nchini kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Spika, kabla na baada ya uchaguzi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* kulikuwa na ongezeko kubwa la wahamiaji haramu wanaoingia nchini kupitia Mikoa ya Rukwa na Kigoma. Katika kipindi hicho wahamiaji 94 walikamatwa mkoani Rukwa na wengine 114 walikamatwa mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kasi ya matukio ya uhamiaji haramu, Serikali imeendelea kuimarisha Idara ya Uhamiaji kwa kuipatia vitendea kazi kama magari na vyombo vya kisasa vya mawasiliano ili kuimarisha misako na doria mipakani na mikoa ya kati.

Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha ushirikiano wa karibu na nchi jirani, kwa lengo la kudhibiti wimbi la wahamiaji haramu. Serikali itaendelea kuimarisha elimu hamasishi kwa umma kuhusu uraia ili viongozi na wananchi wasaidie kutoa taarifa za wahamiaji haramu popote walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba Serikali itaendelea kuwachukulia hatua mbalimbali za kisheria wahamiaji wote wanaokamatwa ikiwa ni pamoja na kuwaondosha nchini. Aidha, itaendelea kuwachukulia hatua wote watakaothibitika kuwasaidia wahamiaji kuingia nchini na kupita kuelekea nchi nyingine au kuishi nchini bila kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Natoa wito kwa viongozi wa ngazi zote, wananchi kwa ujumla na majeshi yetu yote kushirikiana katika juhudi hizi za kuhakikisha kuwa Taifa letu linakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikisisitiza umuhimu wa kukuza sayansi na teknolojia nchini kama nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Msisitizo huu umewekwa bayana katika sera ya sayansi na teknolojia ya mwaka 1996. Malengo makuu ya sera hiyo ni:-

(i) Kuendeleza sayansi na teknolojia kama nyenzo ya maendeleo ya uchumi, uboreshaji wa maisha ya watu na kulinda uhuru wa nchi;

(ii) Kuendeleza kujitegemea kisayansi na Kiteknolojia katika utekelezaji wa uchumi kwa kukuza utafiti wa maendeleo;

(iii) Kuendeleza na kuhamasisha sekta za umma na binafsi za uzalishaji kuendeleza sayansi na teknolojia;

(iv) Kukuza ushiriki wa wanawake katika sayansi na teknolojia; na

(v) Kuanzisha na kuimarisha taasisi za Taifa za sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza sera ya sayansi na teknolojia, Serikali imedhamiria kwa dhati kuanzisha na kuimarisha taasisi za Taifa za sayansi na teknolojia nchini. Dhamira hii imesisitizwa pia katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016). *(Makofi)*

Katika mpango huo, Serikali imeazimia kujenga miundombinu ya kisasa katika taasisi mahsusi za kitaifa za sayansi na teknolojia. Lengo ni kuinua ubora wa ufundishaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu

katika shughuli za utafiti na matumizi ya matokeo ya utafiti (R&D), kuwezesha uanzishwaji na matumizi ya teknolojia mpya katika sekta za uzalishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ya kutekeleza sera ya sayansi na teknolojia ni pamoja na kuanzishwa kwa taasisi za sayansi na teknolojia hapa nchini zinazolenga katika kutekeleza mpango wa maendeleo wa miaka mitano. Tumeanzisha Taasisi ya Nelson Mandela ya Arusha (Nelson Mandela African Institute of Science and Technology) inayojengwa Arusha. (Makofi)

Aidha, taasisi hii ni mojawapo kati ya taasisi nne katika Bara la Afrika zilizobuniwa na Mzee Nelson Mandela kwa ajili ya kujenga uwezo wa sayansi, uhandisi na teknolojia kwa manufaa ya vizazi vijavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, taasisi hii kupitia wataalam wa nchi za Afrika, itatumika kuwapatia wataalam mbalimbali ujuzi na uwezo wa kuwa wabunifu kwa ajili ya maendeleo ya sayansi na teknolojia ya Bara la Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Taasisi nyingine kama hii zipo Abuja, Nigeria; Cape Town, Afrika ya Kusini na Ouagadougou na Burkina Faso. Kwa mujibu wa mpango huo wa miaka mitano hadi kufikia mwaka 2015. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sayansi ya Nelson Mandela inatakiwa iwe imezalisha tafiti zisizopungua 50 zinazolenga sekta za uzalishaji kutokana na Shahada za Uzamili na Uzamivu zitakazosimamiwa na Taasisi hiyo. Taasisi inafundisha masomo ya fani mbalimbali zinazoendana na shule na Idara za Taasisi hiyo zifuatazo:-

- (i) Shule ya Sayansi Uhai na Uhandisi Baiolojia;
- (ii) Shule ya Hisabati, Sayansi na Uhandisi Ukokotoaji na Mawasiliano;
- (iii) Idara ya Sayansi na Uhandisi Nishati Endelevu;
- (iv) Idara ya Sayansi na Uhandisi Rasilimali Maji na Mazingira;
- (v) Idara ya Mafunzo ya Biashara na Sayansi Jamii; na
- (vi) Idara ya Sayansi na Uhandisi Malighafi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatua tuliyopiga katika kuanzisha Taasisi hii inatia faraja kubwa na imetuletea heshima kubwa Tanzania. Tayari Taasisi imefanikiwa kutayarisha mitaala kwa kutumia wataalam wa ndani kwa kushirikiana na wadau wa nje ya nchi, hivi sasa Taasisi imeshadahili wanafunzi 83 wa Shahada za Uzamili na Uzamivu tangu mwezi Oktoba, 2011. Tayari wanafunzi waliopo mmoja anatoka Burundi na waliobaki ni Watanzania. Lengo ni kudahili wanafunzi kutoka eneo la nchi za Afrika ya Mashariki. Kati ya wanafunzi hao, 53 wanasomea Shahada za Uzamili (Msc) na 30 wanasomea Shahada za Uzamivu (Ph.D). Aidha, Taasisi imeajiri watumishi 103 ambao 28 kati yao ni wahadhiri. (Makofi)

Napenda kutumia fursa hii kumpongeza Makamu Mkuu wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha Profesa Burton L. M. Mwamila kwa kazi nzuri anayofanya. Napenda pia kuyapongeza Mashirika ya Hifadhi za Jamii kwa kukubali kutoa mikopo iliyowezesha kufika hapa tulipofika. Aidha, naipongeza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Uongozi wa Mkoa wa Arusha kwa kazi yao nzuri ya usimamizi na uwezeshaji kwa Chuo hiki. Nawashukuru sana! (Makofi)

Tunajua changamoto bado ni kubwa za kuendelea kujenga Taasisi hii kufikia upeo uliowekwa wa kuzalisha wahitimu 1,800 wa Shahada za Uzamili na 1,550 wa Shahada za Uzamivu ifikapo mwaka 2021. Naziomba Taasisi zetu zinazosaidia kujenga Taasisi hii pamoja na wadau wengine kuongeza nguvu ili tukamilishe mapema ujenzi wa Taasisi hii na hatimaye kutimiza malengo ya kuendeleza mafunzo ya sayansi na ufundi nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuendeleza mafunzo ya ufundi nchini. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010 inasisitiza umuhimu wa kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa

Maendeleo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Vilevile, Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2011/2012 hadi 2015/2016 umetoa kipaumbele katika ukuzaji wa rasimali watu nchini.

Mpango huo unabainisha kwamba katika watu wenye uwezo na wanaofanya kazi nchini, ni asilimia tatu tu wana ujuzi wa hali ya juu (*highly skilled*), asilimia 13 wana ujuzi wa kiwango cha katikati na asilimia 84 wana ujuzi wa kiwango cha chini. Kiwango hiki ni cha chini ikilinganishwa na watu wanaofanya kazi katika nchi zenye kipato cha kati (*medium income countries*) ambapo wenye ujuzi wa hali ya juu ni asilimia 12, ujuzi wa kiwango cha katikati ni asilimia 33 na wenye ujuzi wa kiwango cha chini ni asilimia 55. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uwiano huu wa kiwango cha chini cha watu wenye ujuzi wa kufanya kazi, unamaanisha kuna umuhimu sekta ya umma na sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya kutoa mafunzo ya elimu ya kati na ya juu ili kukuza ujuzi wa rasimali watu nchini yenye uwezo wa kukabiliana na changamoto za soko la ajira nchini na ukanda wa Afrika ya Mashariki. Kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano imedhamiria kuwekeza zaidi kwenye utoaji wa elimu ya juu na mafunzo ya ufundi ili kuchochea ukuzaji wa uchumi. (*Makofi*)

Hadi mwaka 2011 idadi ya vyuo vya Serikali vya Ufundi Sanifu vinavyotoa mafunzo ya wataalam wa kati ni vitatu yaani Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, Taasisi ya Ufundi na Teknolojia ya Mbeya na Chuo cha Ufundi Arusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Januari, 2012 nilipata fursa ya kutembelea Chuo cha Ufundi cha Arusha, wakati wa Mahafali ya Chuo hicho na kujionea jitihada kubwa zinazofanywa na uongozi wa Chuo hicho za kubuni na kuanzisha programu mbalimbali zinazoendana na wakati na mahitaji ya nchi. Kwa mfano, chuo kimeanzisha programu mpya za Sayansi za Maabara ili kukabiliana na upungufu wa wataalam wa ufundi katika shule za sekondari na programu ya uhandisi ujenzi na umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, imebainika kwamba nchi yetu inahitaji kuinua idadi na kiwango cha ubora wa kada ya mafundi sanifu na mafundi stadi wa fani mbalimbali ili waweze kukidhi mahitaji ya soko jipya la ajira linaloendana na teknolojia mpya zinazobadilika kila wakati. Aidha, kuna mahitaji pia ya kupata wataalam katika kuendeleza mafunzo ya ufundi na stadi yanayoendana na uchimbaji madini na vito, uendelezaji wa gesi asili, biashara na viwanda mbalimbali. Tunahitaji kuwekeza katika kuanzisha taaluma ya wahandisi, mafundi sanifu na mafundi mchundo katika vyuo vya hapa nchini ili kupata wataalam na mafundi wanaohitajika katika kufanikisha shughuli za kutafuta, kuchimba, kuzalisha, kusafisha na kusafirisha gesi asili. tayari makampuni binafsi ya uzalishaji wa gesi asili nchini hivi sasa wanaajiri wahandisi na mafundi kutoka nchi ambazo zina utaalum huo. Ni vizuri nasi kama nchi tutumie fursa zinazojitokeza kuandaa wataalam wetu katika fani hizo. (*Makofi*)

Napenda kutumia fursa hii kukipongeza Chuo cha Ufundi Arusha kwa ubunifu na hatua ambazo wameanza kuchukua za kutekeleza Sheria ya Madini ya mwaka 2010, inayoelekeza umuhimu wa kujenga uwezo wa ndani wa kukata na kung'arisha madini ya vito. Hili ni jambo zuri linalopaswa kuigwa na vyuo vingine vya ufundi nchini kwa kubaini mahitaji ya stadi mbalimbali za ufundi zinazohitajika katika tasnia za kisekta nchini. Wito wangu sasa ni kwa vyuo vyote vya Ufundi kuendelea kuwa wabunifu kwa kuanzisha programu mbalimbali kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Aidha, nawahimiza Wizara husika na sekta binafsi kushirikiana katika kukidhi mahitaji ya mafundi sanifu na mafundi stadi nchini. Tukifanya hivi tutaongeza ajira kwa mafundi wetu na kuboresha ujuzi unaohitajika katika tasnia husika na hatimaye kuinua ubora wa bidhaa zitakazozalishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu matokeo ya tathmini ya mpango wa kuzipatia ruzuku za maendeleo na ruzuku za kujenga uwezo Serikali za Mitaa kwa mwaka 2011/2012, Serikali imekuwa ikiendesha tathmini ya mpango wa kuzipatia ruzuku za maendeleo, ruzuku za kujengea uwezo pamoja na ruzuku za kisekta Mamlaka za Serikali za Mitaa kila mwaka. Madhumuni ya zoezi hilo ni kuona ni kwa namna gani Mamlaka hizo zinavyozingatia vigezo vya utawala bora katika utoaji huduma na kupeleka maendeleo kwa wananchi. Halmashauri zinazofuzu vigezo na masharti yaliyowekwa katika tathmini hiyo hupatiwa ruzuku ya maendeleo na ya kisekta kwa asilimia 100 wanayostahili. Halmashauri zisizofuzu hupewa 25% ya ruzuku ya maendeleo na ruzuku ya kisekta 50%. Aidha, kwa upande wa tathmini ya kupatiwa ruzuku ya kujenga uwezo, Halmashauri, zinazofuzu hupatiwa ruzuku hiyo kwa 100%, na zilizoshindwa zinawekwa chini ya uangalizi wa Sekretarieti ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyozingatiwa katika zoezi hilo ni hivi vifuatavyo:-

Kwanza, masharti ya msingi (*minimum conditions*), katika eneo hili Halmashauri zilipimwa kwa kuangalia namna ambavyo zinasimamia na kutumia ruzuku inayopelekwa kwa shughuli mbalimbali katika mamlaka hizo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Fedha za Serikali za Mitaa. Aidha, inazingatia mahusiano yaliyopo kati ya Halmashauri na mamlaka za msingi za Serikali za Mitaa hususan katika kupeleka fedha za maendeleo katika ngazi za vijiji na kata. (Makofi)

Pili, kupima utendaji wa Halmashauri (*performance measures*), katika eneo hili Halmashauri zinapimwa kwa kuangalia namna ambavyo mamlaka hizo zinazingatia Sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali katika maeneo ya uendeshaji na usimamizi wa Halmashauri, ikiwa ni pamoja na ukusanyaji na usimamizi wa mapato, kuzingatia uwazi na uwajibikaji, maendeleo ya rasilimali watu, uzingatiaji sheria ya manunuzi, na pia usimamizi na ufuatiaji wa utekelezaji miradi ya maendeleo. (Makofi)

Tatu, kigezo kilichotumika katika zoezi la tathmini ni hoja zilizomo katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia vigezo nilivyovitaja hapo juu, katika mwaka 2011/2012 zoezi hilo lilifanyika kuanzia tarehe 14 Februari, 2011 hadi tarehe 16 Machi, 2011 ambapo jumla ya Halmashauri 132 zilipimwa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya upimaji huo yameonesha kwamba kwa kiasi kikubwa Halmashauri nyingi zimefanya vizuri katika zoezi hilo na hivyo kustahili kupatiwa ruzuku chini ya mfumo huo. Naomba nitumie muda wako mfupi kuelezea matokeo hayo. (Makofi)

Katika vigezo vya masharti ya msingi (*minimum conditions*) kati ya Halmashauri 132 zilizofanyiwa tathmini, Halmashauri 128 zilifuzu vigezo vilivyowekwa, Halmashauri nne zilishindwa kufaulu. Halmashauri ambazo hazikufuzu katika kigezo hiki ni Halmashauri za Wilaya ya Rombo, Kishapu, Bagamoyo na Kilosa. Halmashauri zilizofuzu zitapata ruzuku ya maendeleo na ya kisekta kwa 100% ya stahili yake, wakati zilizoshindwa zitapata asilimia 25 ya stahili yake pamoja na ruzuku ya kisekta kwa 50%. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sababu zilizosababisha Halmashauri hizo kushindwa katika kigezo hiki ni pamoja na kuwepo kwa taarifa za matumizi mabaya ya fedha (hususani katika Halmashauri za Kishapu, Kilosa na Bagamoyo), kutozingatiwa kwa taratibu za manunuzi hasa katika kuunda Bodi ya Zabuni na kupatah isiyoridhisha kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Mkuu wa Serikali mwaka 2009. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ruzuku ya kujenga uwezo wa halmashauri (*capacity building grant*), kati ya Halmashauri 132 zilizopimwa, Halmashauri 123 sawa na asilimia 93.18 zilifuzu kupata ruzuku hiyo, wakati Halmashauri tisa hazikufuzu. Halmashauri ambazo hazikufuzu ni Rombo, Ulanga, Masasi, Newala, Tandahimba, Bukombe, Kilindi na Manispaa ya Kigoma Ujiji na Tabora. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sababu zilizosababisha Halmashauri hizi kutofuzu kupata ruzuku ya kujenga uwezo ni pamoja na kutowasilisha ushahidi unaoonesha kuwa mpango wa kujengewa uwezo wa Halmashauri uliidhinishwa na Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri. Halmashauri zote zilizofuzu zitapata 100% ya ruzuku ya kujenga uwezo, wakati Halmashauri zilizoshindwa zitakuwa chini ya uangalizi wa Sekretarieti ya Mkoa. Natoa wito kwa uongozi wa mkoa husika kuzisimamia ipasavyo Halmashauri hizo ili ziweze kurekebisha upungufu uliojitokeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tathmini katika kigezo cha utendaji wa Halmashauri (*performance measures*) kimeonesha kuwa hali ya utendaji wa Halmashauri inaendelea kuimarika na kuboreka zaidi. Matokeo yanaonesha kuwa Halmashauri 110 sawa na 83.33% ya Halmashauri 132 zilizopimwa zilifuzu vizuri sana; Halmashauri mbili sawa na 1.52% zilifuzu katika kiwango cha vizuri, Halmashauri 16 sawa na 12.12% zilifuzu katika kiwango cha wastani na Halmashauri nne sawa na 3.03% zilifanya vibaya.

Pamoja na kwamba matokeo ya tathmini yanaonesha kuboreka kwa hali ya utendaji katika Halmashauri, jambo la muhimu ambalo wananchi wangependa kuona ni kuongezeka kwa ufanisi katika

utoaji wa huduma muhimu zinazotolewa na Halmashauri ikiwa ni pamoja na kupata maisha bora. Hivyo, natoa wito kwa Halmashauri zote zihakikishe kwamba huduma muhimu zinaimarika mijini na vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika tathmini hii inaonesha kuwa idadi ya hati safi zimepungua kutoka hati 61 sawa na 46% katika mwaka 2007/2008 hadi hati 54 sawa na 42% mwaka 2008/2009. Aidha, hati zenye mashaka zimeongezeka kutoka hati 71 sawa na 54% katika mwaka 2007/2008 hadi hati 74 sawa na 58% katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, tayari hatua za kinidhamu dhidi ya watendaji wakuu walioshindwa kufikia vigezo vilivyowekwa zimechukuliwa na Serikali. Kwa mfano, watendaji katika Halmashauri za Bagamoyo, Kilosa, Kishapu na Rombo waliosababisha Halmashauri kukosa ruzuku ya maendeleo wamechukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kuvuliwa madaraka. Aidha, wakurugenzi wa Halmashauri ya Kilindi, Rombo, Ulanga, Bukombe, Masasi, Newala, Tandahimba na Halmashauri za Manispaa za Kigoma na Tabora waliosababisha Halmashauri zao kushindwa kufuzu vigezo kwenye eneo la kujenga uwezo wameandikiwa barua za onyo na wametakiwa kuhakikisha kwamba Halmashauri hizo zinajirekebisha ili hatimaye ziweze kufanya vizuri katika upimaji ujao. (Makofi)

Vilevile Makatibu Tawala katika mikoa yote wametakiwa kuongeza kasi katika usimamizi. Naomba nitoe wito kwa Makatibu Tawala ambapo kuna Halmashauri zilizoshindwa kufuzu vigezo hususan Mtwara, (Masasi, Newala na Tandahimba); Kigoma (Manispaa ya Kigoma), Kilimanjaro (Rombo), Morogoro (Ulanga), Pwani (Bagamoyo), Shinyanga (Bukombe), Tabora (Manispaa ya Tabora) na Tanga (Kilindi) kusimamia kwa karibu sana wao binafsi utekelezaji wa mpango kazi wa kila Halmashauri na kuhakikisha kuwa Halmashauri zinaendelea na zoezi la kujipima (*self assessment*) na kuzingatia masuala ya utawala bora kila robo mwaka kabla upimaji mwingine haujafanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, zoezi hili la tathmini ni muhimu na lenye kuhitaji umakini na kujitoa kwa hali ya juu. Masuala yanayopimwa ni ya kiutendaji na usimamizi wa kila siku katika Halmashauri zetu. Hivyo ni dhahiri kuwa masuala hayo yakizingatiwa ipasavyo kiwango cha ufanisi katika Halmashauri zetu kitaongezeka. Nawaagiza watendaji katika Halmashauri kuwa waadilifu na kuwajibikaji ipasavyo. Aidha, uongozi wa mikoa kupitia sekretarieti usimamie ipasavyo Halmashauri hizo. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge katika Halmashauri zenu kuhakikisha kuwa zoezi hilo linafanywa kwa umakini na uadilifu mkubwa. (Makofi)

Mwisho, napenda kutoa pongezi za dhati kwa mikoa ambayo baadhi ya Halmashauri zake zimefanya vizuri wakati wa zoezi la upimaji. Mikoa hii ni pamoja na Arusha, Dar es salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Lindi, Singida, Manyara, Mara, Mbeya, Mwanza, Rukwa na Ruvuma. Nawasihi waendeleo kusimamia maeneo yao kwa umakini zaidi ili waweze kufanya vizuri zaidi katika tathmini zijazo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio ya kuongezeka mapato ya mfuko wa barabara baada ya kudhibiti uchakachuaji wa mafuta, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka, mnamo mwaka 2009 Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na EWURA pamoja na TRA walibaini kuwa kuna wastani wa kiasi cha lita milioni 112 cha mafuta ya taa kinachoingizwa nchini kila mwaka ambacho ni zaidi ya mahitaji halisi ya nishati hiyo. Kiasi hiki cha ziada ndicho kilichohisiwa kuhusika katika uchakachuaji wa mafuta ya petroli ambao uliwaingizia wafanyabiashara faida maradufu na kuikosha mapato Serikali. Serikali ilikadiriwa kupoteza kiasi cha shilingi bilioni 22.5 kama mapato ya mfuko wa barabara na kiasi cha shilingi bilioni 35.5 kama ushuru wa bidhaa. Kutokana na upotevu huu wa mapato, Serikali kupitia Bajeti ya mwaka 2011/2012 iliamua kuchukua hatua ya kuongeza ushuru kwenye mafuta ya taa wa kiasi cha shilingi 400.30 kama njia ya kuongeza mapato pamoja na kudhibiti uchakachuaji wa mafuta. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kufuatia uamuzi huo wa kijasiri, tathmini ya awali inaonesha kuongezeka kwa mapato ya mfuko wa barabara nchini. Aidha, uagizaji wa mafuta ya taa nchini umepungua kwa kiasi kikubwa jambo linaloonesha kuwa kiasi hicho cha nyongeza ya mafuta ya taa kilikuwa kinatumika siyo kwa malengo ya kuwafikia watumiaji bali kwa ajili ya uchakachuaji kwa kuchanganywa na mafuta ya dizeli pamoja na petroli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo za matumizi ya mafuta nchini zinaonesha kupungua kwa matumizi ya mafuta ya taa. Kwa mujibu wa takwimu hizo, kwa mfano, inaonesha katika mwezi Januari, 2011 kiasi cha mafuta ya taa kilichotumika kilikuwa lita milioni 20.1. Katika miezi ya Agosti, Septemba na

Oktoba mara baada ya kupitisha Bajeti ya mwaka 2011/2012, ambapo mafuta ya taa yaliongezwa bei, matumizi ya mafuta ya taa nchini yalishuka hadi kufikia wastani wa lita milioni 9.0 ambayo ni sawa na punguzo la zaidi ya 50%.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya Mfuko wa Barabara nchini, takwimu zinaonesha kuongezeka kwa mapato dhidi ya makisio yaliyokuwepo. Mfano, katika nusu ya mwaka huu wa fedha (Desemba, 2011) makusanyo yalikuwa yamefikia kiasi cha shilingi bilioni 214.2 ikilinganishwa na makisio ya shilingi bilioni 157.72. kiasi hiki cha makusanyo ni sawa na 67.7% ya Bajeti ya mwaka 2011/2012 ambayo ni shilingi bilioni 316.551. Ikiwa ongezeko hili la mapato litaendelea kuna matarajio ya kuvuka malengo tuliyojiwekea kwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 407.1 na hivyo kuwa na ziada ya shilingi bilioni 90.6. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ya kuongezeka kwa mapato ya mfuko wa barabara pamoja na udhibiti wa uchakachujaji mafuta yanatokana na uamuzi wa busara chini ya uongozi wa Serikali ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuongeza ushuru wa mafuta ya taa ili bei ya mafuta ya taa ilingane na bei ya dizeli. Wote mtakubalina nami kwamba uamuzi huu ulikuwa mgumu na wa kijasiri hasa tukizingatia kuwa mafuta ya taa yanatumika kwa ajili ya kupikia na kupata mwanga kwa watu wa kipato cha chini hasa wanaoishi vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, matumaini yangu ni kuwa fedha hii iliyopatikana kupitia Mfuko wa Barabara itasaidia zaidi katika matengenezo na ukarabati wa barabara na kuendeleza miradi ya maendeleo nchini. Hata hivyo, bado tunahitaji kuongeza vyanzo vya mapato ya mfuko ili kukidhi mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kukubali kufanya maamuzi haya magumu. Aidha, nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri wenu uliompelekea Mheshimiwa Rais kukubali maamuzi haya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya tuliyoanza kuyapata, bado tunazo changamoto katika eneo hili. Taarifa zilizopo zinaonesha bado kuna upotevu wa mapato unaotokana na kuuzwa nchini kwa mafuta yanayoagizwa kwa ajili ya soko la nchi jirani. Taarifa hizo zinaonesha kuwa, karibu 20% ya mafuta hayo yanayoagizwa kwa lengo la soko la nchi jirani hutumika nchini. Hali hii inaashiria udanganyifu kwa baadhi ya wafanyabiashara wa mafuta nchini ambao kwa makusudi huagiza mafuta wakidai ni kwa ajili ya soko la nchi jirani huku lengo lao ni kuuza nchini.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba hii ni kasoro kubwa ambayo tunapaswa kuendelea kuidhibiti. Tumeanza kuchukua hatua kwa kuweka vinasaba (rangi) katika mafuta yanayotumika hapa nchini ili kuyatofautisha na yale yanayoagizwa kwa ajili ya nchi jirani.

Napenda kuiagiza Wizara ya fedha kutumia vyombo vyake vya TRA kwa kushirikiana na EWURA kufanyia kazi kasoro hii mapema na kutoa maoni kuhusu namna bora zaidi ya kudhibiti hali hii. Ni matumaini ya Serikali kwamba tafizo hili litapata suluhu mapema iwezekanavyo na kwamba hali ya uchakachujaji wa mafuta haijirudii tena. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kusisitiza maeneo muhimu yafuatayo:-

Kwanza, tathmini ya hali ya chakula inaonesha dalili nzuri za kuwepo kwa chakula cha kutosha katika maeneo mengi nchini. Pamoja na kuondolewa kwa zuio la kuuza mahindi nje ya nchi, ni vizuri kuendelea kutumia chakula kilichopo kwa uangalifu. Wafanyabiashara waepuke kusafirisha mahindi nje ya nchi kiholela na kwa njia ya magendo na wazingatie sheria na taratibu zilizowekwa. (Makofi)

Pili, tumeanza vizuri maandalizi ya msimu wa kilimo kwa kutumia mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kupitia mfumo wa vocha. Viongozi katika ngazi zote kuanzia watendaji wa vijiji, kamati zinazosimamia mpango huu, uongozi wa Wilaya, Mikoa na Wizara wahakikishe wakulima wanapata pembejeo kwa wakati. (Makofi)

Tatu, tunazo fursa nzuri ya kutumia rasilimali ya mifugo ambayo ipo kwa kiasi kikubwa hapa nchini. Tuwaelimishe wananchi hususan wafugaji kuhusu kanuni za ufugaji bora wenye tija. Tuanzishe mashamba

darasa ya mifugo katika Halmashauri na Majimbo yetu kuonesha umuhimu wa kutumia mifugo tuliyonayo kwa tija zaidi na hivyo kujiletea maisha bora. *(Makofi)*

Nne, vilevile tunayo fursa ya kuanzisha ufugaji wa samaki na viumbe wa majini. Tutumie fursa hii kuhamasisha wananchi kupenda shughuli za uvuvi kwa njia halali na ufugaji samaki ili kujipatia kipato na lische bora. Aidha, tuendelee kuwahamasisha wananchi juu ya faida na umuhimu wa kuanzisha ufugaji wa nyuki na kuendesha ushiriki wa wafugaji nyuki. Tuwashirikishe wananchi katika kutumia kanuni bora za ufugaji wa zao hili. Halmashauri zitenge fedha na kuweka mikakati ya kukuza shughuli za ufugaji nyuki katika maeneo yao. *(Makofi)*

Tano, bado tunalo tatizo la uhamiaji haramu hapa nchini. Tuwahamasishe wananchi waone umuhimu wa kutoa taarifa za wahamiaji haramu popote walipo. Wale wote wanaosaidia kuwepo kwa wahamiaji haramu nchini wachukuliwe hatua. Tushirikiane na vyombo vya ulinzi usalama kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa salama. *(Makofi)*

Sita, tunalo jukumu la kuhakikisha kwamba tunashiriki kikamilifu kuinua soko la ajira nchini kwa kutoa elimu ya juu ya mafunzo ya ufundi na stadi kwa vijana wetu kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi.

Saba, tumeweka utaratibu wa kupima Halmashauri kwa vigezo mbalimbali ikiwemo vigezo vya msingi, utendaji wa Halmashauri na kuangalia taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Tusimamie watendaji katika kila Halmashauri watimize wajibu wao kuhakikisha kwamba hazikosi ruzuku ya maendeleo. Kila Mkurugenzi wa Halmashauri awajibike kujipima mwenyewe utendaji wake kabla ya upimaji wa jumla katika Halmashauri yake. *(Makofi)*

Nane, tumeanza kupata mafanikio ya kuongezeka kwa mapato kutokana na biashara ya mafuta. Hata hivyo, bado tunayo changamoto katika biashara hii hususan kwenye mafuta yanayoagizwa kwa ajili ya soko la nchi jirani. Ni vizuri kutafuta njia bora zaidi ya kutuwezesha kuzuia upotevu wa mapato unaotokana na baadhi ya wafanyabiashara ambao kwa makusudi huuzwa mafuta hayo ndani ya nchi badala ya nje ya nchi.

Tisa, wote tunafahamu hali iliyojitokeza kuhusu mgomo wa madaktari ambao umetugusa wote takriban kipindi chote tulichokaa hapa Bungeni wakati wa mkutano huu. Tunashukuru sakata hili sasa lina mwelekeo mzuri baada ya makubaliano ya msingi. Ninachowaomba sasa wote twende tupeane moyo wa kufanya kazi na kuwasaidia wenzetu hususan wagonjwa ambao maisha yao yanategemea huduma ya madaktari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapofikia mwisho wa Mkutano huu wa Sita, pamoja na kumshukuru Mwenyezi Mungu tunayo sababu ya msingi ya kuwashukuru pia wote walioshiriki katika kutoa huduma muhimu na hatimaye kufanikisha mkutano huu. *(Makofi)*

Nitumie fursa hii kutoa shukrani za dhati kwako wewe Mheshimiwa Spika kwa kutuongoza kwa busara na umakini kukamilisha vikao vyote vilivyopangwa. Aidha, namshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Niruhusu nimshukuru Katibu wa Bunge na wasaidizi wake kwa kutuwezesha kufanya kazi hii vizuri. Niwashukuru pia wataalam wa Wizara zote, askari, madereva, wanahabari na wasaidizi wengine wote kwa kutoa mchango mkubwa katika kufanikisha Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunahitimisha Mkutano wa Tano wa Bunge hili, tulimuomba Mwenyezi Mungu atujalie tumalize mwaka 2011 salama na kufikia mwaka 2012. Leo tunahitimisha Mkutano huu wa Sita tukiwa tumejiwekea malengo ya kutekeleza kwa mwaka 2012. Naomba kusisitiza kwamba bado tuna changamoto nyingi za mambo ya kufanya kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Ni jukumu la kila mmoja wetu bila ya kujali itikadi ya vyama vya siasa wala dini kutimiza wajibu wake katika kufikia malengo tuliyojijwekea kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Nimalizie kwa kuwatakiya nyote safari njema ya kurejea katika maeneo yenu ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 10 Aprili, 2012, saa tatu asubuhi, litakapokutana kwenye ukumbi huu hapa Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza tunakushukuru sana kwa hotuba hiyo ndefu na pia napenda niseme kwamba pia sisi tunapenda kushukuru kwamba katika kikao hiki tumefanikiwa kufanya mambo mengi sana pamoja, na inaonyesha kabisa Bunge linaendelea kukua, kama angekuwa mtoto anatambaa sasa amesimama, bado tuna hatua ndefu sana ya kuendelea, lakini kizuri ni kwamba kila mtu ni vizuri tuendeleee kujua kanuni zetu. Ni kanuni zetu tu peke yake ndio zifatusaidia kuwa na mwenendo mzuri ndani ya Bunge hili. Kwa sababu tupo watu wa aina nyingi, kuna rika mbalimbali na uelewa tofauti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kila mtu ajitahidi vilevile kuendelea kuzifahamu Kanuni, jinsi tutakavyofahamu Kanuni, tutajua kwamba tunaweza kufanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Lakini bado niendeleee kusisitiza kwamba tukiwa humu ndani ya nyumba hii sisi ni Wabunge, sio watu wa vyama fulani fulani. Tukifanya michezo ya vyama kweli wanaotuangalia inakuwa kwa kweli haipendezi sana.

Waheshimiwa Wabunge, tukiwa ndani ya Bunge humu tujitahidi kadri inavyowezezana kuonekana kama sisi ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni watunga sheria. Maana hatuwezi kutunga sheria inayokuwa ya chama fulani, haiwezekani hizi sheria za nchi.

Kwa hiyo, hili tunaendelea kuliondoa nawashukuru sana katika umoja wetu kupitisha Marekebisho ya Katiba. Wakati wote ndani ya siasa lazima kuwepo na uvumilivu wa kisiasa na zaidi tukiwa humu ndani kauli zitakuwa tofauti kati yetu na ni lazima wavumilie kwa sababu wewe ukisema ukumbuke na mwenzio labda umemwudhi na yeye avumilie na wewe ukisema avumilie hivyo hivyo. *(Makofi)*

Sasa kila mtu akijiona yeye ya kwake itabidi yasikike basi sababu ya kutunga sheria haipo. Utasema mawazo yako lakini wenzio watachangia kuonekana kwamba ama sio kukosoa sana kufikiria upande mwingine. *(Makofi)*

Mimi nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge, hizo ndizo mila na desturi za Mabunge yote, anaposema mwenzio msikilize hoja yake. Kama wewe una hoja nzito zaidi basi wewe utatoa hiyo na wenzako pia wakusikilize. Mwisho tunakubaliana kwa utaratibu ambao umewekwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijauliza hoja ya kuahirisha Bunge naomba nitoe taarifa kwamba Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 inatutaka kuwachagua Wawakilishi wa Bunge katika vyombo vingine wakiwemo Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Aidha, Ibara ya 50 ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inataka Bunge letu kufanya uchaguzi huo. *(Makofi)*

Hivyo, napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba katika Mkutano wa Saba wa Bunge tutafanya Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa tarehe ambayo itakayopangwa. *(Makofi)*

Taarifa na tangazo yaani *notice* ya mchakato wa uchaguzi huu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki itatolewa baadaye na Katibu wa Bunge, kwa sababu wenzetu wa Afrika Mashariki wameleta mabadiliko ya utaratibu kidogo. Kwa hiyo hili tutayafanyia kazi halafu Katibu atatoa *notice* kwa wananchi wale wanaotaka kugombea. Lakini sisi tutafanya kazi ya uchaguzi Bunge la Saba. Kwa hiyo, nataka hii ifahamike maana yake mmekuwa mmeona watu wanapitapita ukweli kwamba mwezi Aprili ndipo tutafanya uchaguzi. Lakini *notice* kamili kwa wananchi tutaitoa. Kwa hiyo, Katibu atafanya hivyo. *(Makofi)*

Halafu pia napenda kutangaza kwamba Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Wabunge wa *caucus* ya CCM anasema niwatangazie Wabunge wote wa CCM kuwa watakuwa na kikao leo saa mbili usiku kule *White House* kwenye Makao Makuu ya CCM. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo niombe nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake, pia niwashukuru nyie Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyofanya kipindi hiki, yote yaliyotokea sio ugomvi wala nini, ndiyo hali halisi ya kuendesha Bunge. Hakuna ugomvi na kama kuna mtu amemwudhi mwenziwe basi msameheane, hakuna kugombana wala kuudhiana yaliyotokea hapa yanabakia humu humu ndani mkitoka hapo ninyi wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ofisini kwetu hatuna tangazo lingine sasa naomba tusimame kwa ajili ya wimbo wa Taifa. *(Makofi)*

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa uliigwa)

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 10 Aprili, 2012 saa tatu asubuhi)